

**UREJELEANO KATIKA UTUNZI WA KAMUSI ZA KISWAHILI:
UCHANGANUZI LINGANISHI WA KAMUSI TEULE ZA LUGHA
MOJA**

MWETERI ISIAH MAITHULIA

C50/OL/CTY/32792/2016

Tasnifu hii imewasilishwa kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika, Shule ya Elimu,

Chuo Kikuu cha Kenyatta

MEI 2021

IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa kwa madhumuni ya shahada yoyote katika chuo kikuu chochote.

MWETERI ISAIAH MAITHULIA

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa madhumuni ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Kiswahili.

DAKTARI LEONARD CHACHA MWITA

PROFESA IRERI MBAABU

TABARUKU

Ninaitabaruku tasnifu hii kwa marehemu babangu Thomas Maithulia, mamangu Rosana Kaario, mke wangu mpendwa, Lucy Kendi, watoto wangu Ian Mugambi, Lauren Makena na Lorna Mwendwa.

SHUKRANI

Ninamshukuru Maulana kwa kunijalia afya na uwezo wa kuhitimisha kazi hii. Shukrani za dhati zimwendee mke wangu mpenzi Lucy Kendi kwa kuniunga mkono na kunisaidia kwa kila hali na mali. Asante sana kwa kuwaelewesha watoto wetu kuwa nilihitaji kujifungia chumbani ili nihitimishe kazi ya mwalimu. Ninamshukuru mwajiri wangu, Oxford University Press, kwa sehemu ya ufadhili, pamoja na kunipa ruhusa wakati wowote nilipohitajika chuoni. Shukrani za dhati pia ziwaendee wanafunzi wenzangu Michael Muingi, Christant Kiilu na Caroline Getate ambao kwao kazi hii ilirahisika. Pia, ninawashukuru walimu wangu Prof. Ileri Mbaabu, Prof. Kitula Kingéi, Prof. Catherine Ndung'o, Dkt Leonard Chacha Mwita, Dkt Pamela Ngugi, Dkt Richard Wafula, Dkt Miriam Osore, Dkt Jacktone Onyango na Dkt Joseph Gakuo, ambao kwao ninajivunia shahada hii. Mwisho kabisa ninawashukuru wasimamizi wangu, Prof. Ileri Mbaabu na Dkt Leonard Chacha Mwita, kwa kunishika mkono na kunielekeza kwa upendo wa mzazi. Nyote Mwenyezi Mungu awakirimie.

YALIYOMO

IKIRARI.....	ii
TABARUKU	iii
SHUKRANI.....	iv
YALIYOMO	v
ORODHA YA VIFUPISHO	xi
UFAFANUZI WA ISTILAH.....	xiii
IKISIRI.....	xiv
ABSTRACT	xv
SURA YA KWANZA	1
UTANGULIZI	1
1.0 Usuli wa Mada.....	1
1.1 Suala la Utafiti	6
1.2 Malengo ya Utafiti.....	6
1.3 Maswali ya Utafiti	7
1.4 Sababu za Kuchagua Mada.....	7
1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti	9
1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ya Utafiti	9
1.6.1 Leksikografia	10
1.6.2 Urejeleano	14
1.7 Misingi ya Kinadharia	18

1.8	Mbinu za Utafiti.....	21
1.8.1	Muundo wa Utafiti.....	21
1.8.2	Eneo la Utafiti.....	21
1.8.3	Sampuli na Usampulishaji.....	22
1.8.3.1	Jumuiya.....	22
1.8.3.2	Usampulishaji.....	23
1.8.4	Mbinu za Ukusanyaji Data.....	25
1.8.4.1	Udondoaji wa moja kwa moja wa data.....	25
1.8.4.2	Mahojiano na wachapishaji.....	26
1.8.4.3	Hojaji kwa watumiaji wa kamusi.....	26
1.8.5	Uchanganuzi wa Data.....	27
1.8.6	Uwasilishaji wa Matokeo.....	27
1.8.7	Maadili ya Utafiti.....	28
	SURA YA PILI.....	29
	VIPENGELE VYA UREJELEANO KATIKA KAMUSI TEULE ZA	
	KISWAHILI.....	29
2.0	Utangulizi.....	29
2.1	Dhana za Kimsingi kuhusu Urejeleano.....	29
2.1.1	Chanzo cha Urejeleano.....	30
2.1.2	Anwani ya Urejeleano.....	31
2.1.3	Alama ya Urejeleano.....	32

2.1.4 Uhusiano wa Kiurejeleano.....	33
2.1.5 Urejeleano Mzunguko	34
2.1.6 Urejeleano Uliokufa	35
2.2 Vipengele vinavyoweza Kuhusishwa kupitia Urejeleano	37
2.2.1 Vibandala.....	37
2.2.2 Visawe	43
2.2.3 Vinyume	47
2.2.4 Wingi wa nomino	49
2.2.5 Methali, Nahau na Misemo	51
2.3 Hitimisho	52
SURA YA TATU	53
MISHABAHA NA TOFAUTI ZA MATUMIZI YA UREJELEANO	
KATIKA KAMUSI TEULE	53
3.0 Utangulizi	53
3.1 Vibandala.....	54
3.2 Visawe	61
3.3 Vinyume	67
3.4 Umoja na wingi wa nomino.....	68
3.5 Vifungu vya maneno	72
3.5.1 Nahau.....	72
3.5.2 Misemo	76

3.5.3 Methali	78
3.6 Hitimisho	83
SURA YA NNE	84
ATHARI YA UREJELEANO NA MAPENDEKEZO YA KUBORESHA	
UREJELEANO	84
4.0 Utangulizi	84
4.1 Athari	85
4.1.1 Athari Chanya.....	85
4.1.1.1 Athari Chanya kwa Wachapishaji	85
4.1.1.2 Athari Chanya kwa Watumiaji wa Kamusi	88
4.1.2 Athari Hasi.....	89
4.1.2.1 Athari Hasi kwa Wachapishaji	90
4.1.2.2 Athari Hasi kwa Watumiaji wa Kamusi	94
4.1.2.2.1 Athari Hasi katika Taarifa za Kisarufi.....	94
4.1.2.2.1.1 Athari Hasi kutokana na Kubadilisha Kategoria ya neno.....	95
4.1.2.2.1.2 Athari Hasi kutokana na Kubadilisha Ngeli za maneno.....	96
4.1.2.2.2 Athari Hasi kutokana na Uainishaji Potovu wa Vibadala na Visawe	96
4.1.2.2.3 Athari Hasi kutokana na Urejleano Uliokufa	98
4.1.2.2.4 Athari Hasi kutokana na Urejleano Mzunguko	99
4.1.2.2.5 Athari Hasi kutokana na Urejleano katika Kidahizo kilekile	100

4.1.2.2.6 Athari Hasi kutokana na Urejeleano Usiobainisha Anwani Mwafaka ya Urejeleano	101
4.1.2.2.7 Athari Hasi kutokana na Urejeleano wa Upande Mmoja	102
4.2 Mapendekezo ya Kuboresha Urejeleano katika Kamusi za Kiswahili za Lugha Moja.....	105
4.2.1 Msingi wa Urejeleano uwe Nadharia ya Miundomedio	105
4.2.2 Kuepuka Uradidi.....	106
4.2.3 Kuwe na Urejeleano wa Pande zote mbili.....	107
4.2.4 Kuwe na Utafiti Mwafaka kuhusu Uhusiano wa Maneno.....	108
4.2.5 Kuwe na Umakinifu zaidi katika Udurusu na Uhariri wa Miswada.....	109
4.2.6 Kuwe na Usawazishaji wa Vipengele vyote kabla ya Uchapaji wa Kamusi.....	110
4.3 Hitimisho	111
SURA YA TANO	113
MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI.....	113
5.0 Utangulizi	113
5.1 Muhtasari wa Utafiti	113
5.2 Matokeo ya Utafiti.....	115
5.2.1 Vipengele vya Urejeleano katika Kamusi Zilizochanganuliwa.....	115
5.2.2 Mifanano na Tofauti za Matumizi ya Urejeleano.....	116
5.2.3 Athari ya Urejeleano.....	116

5.2.4 Namna ya Kuboresha Urejeleano katika Kamusi za Kiswahili za Lugha	
Moja.....	118
5.3 Mapendekezo ya Utafiti.....	118
5.3.1 Ishara tofauti za Urejeleano	118
5.3.2 Matumizi ya Lugha Kienzo	119
5.3.3 Uainishaji wa Homonimu na Polisemi	119
5.3.4 Matumizi ya Programu za Kompyuta.....	119
5.4 Hitimisho	120
MAREJELEO	121
VIAMBATISHO	126
KIAMBATISHO CHA KWANZA: MIFANO ZAIDI YA DATA	126
KIAMBATISHO CHA PILI: KIONGOZI CHA MAHOJIANO.....	142
KIAMBATISHO CHA TATU: HOJAJI KWA WATUMIAJI WA KAMUSI.....	143
KIAMBATISHO CHA NNE: MAKADIRIO YA MATUMIZI.....	145

ORODHA YA VIFUPISHO

BAKITA	Baraza la Kiswahili la Taifa
BAKIZA	Baraza la Kiswahili la Zanzibar
EAEP	East African Educational Publishers
ITLC	Inter-Territorial Language Committee
JKF	Jomo Kenyatta Foundation
k.m.	kwa mfano
k.v.	kama vile
KEK	Kamusi Elezi ya Kiswahili
<i>ki/kih.</i>	kihishishi
kis.	kisawe
KKK	Kamusi Kuu ya Kiswahili
KKS	Kamusi ya Kiswahili Sanifu
<i>kl/kiel</i>	kielezi
kt	kitenzi
LPL	Longhorn Publishers Limited
mat.	matumizi
ms/mse	msemo

mt	methali
n.k.	na kadhalika
nh	nahau
nm	nomino
OUP	Oxford University Press
TATAKI	Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
TUKI	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
VM	Vide Muwa
vis.	visawe

UFAFANUZI WA ISTILAHU

Antonimu	neni lililo na maana ambayo ni kinyume cha neno jingine
Kibadala	neni linalotofautiana kidogo na jingine kitahajia na kimatamshi lakini lenye maana sawa na hilo
Kidahizo	neni linaloingizwa katika kamusi na kutolewa fasili
Kitomeo	kidahizo na taarifa zote zinazoandamana nacho
Polisemi	neni lenye maana zaidi ya moja
Sinonimu/Visawe	maneno tofauti yenye maana sawa
Tahajia	jinsi ya kuendeleza neno
Urejeleano	mbinu ya kuonesha uhusiano uliopo baina ya vipashio tofauti

IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza jinsi kipengele cha urejeleano kilivyoshughulikiwa katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu Toleo la Tatu* (2013), *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2015) na *Kamusi Elezi ya Kiswahili* (2016). Nadharia ya miundomedio (mediestructures) iliuelekeza utafiti huu, ambao ulilenga kubaini vipengele vya urejeleano katika kamusi teule, kulinganisha na kulinganua matumizi ya urejeleano katika kamusi hizo, kujadili athari ya urejeleano katika kamusi hizo na hatimaye kupendekeza, kutegemea matokeo ya utafiti, namna ya kuboresha urejeleano katika kamusi za Kiswahili za lugha moja. Asilimia kubwa ya utafiti ilifanywa maktabani kwa kunukuu vipengele vinavyofaa kuhusishwa kwa kurejelea kutoka katika kamusi teule, na nyanjani kupitia mahojiano. Wachapishaji na watumiaji wa kamusi walihojiwa na maoni yao kujumuishwa katika utafiti huu. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kuiegemeza kwenye mihimili ya nadharia ya miundomedio na matokeo kutolewa kwa njia ya maelezo. Utafiti huu utaleta mwanga mpya katika kukishughulikia kipengele cha urejeleano katika kamusi za Kiswahili za lugha moja.

ABSTRACT

This research aimed at analysing the way cross-referencing has been used in three monolingual Kiswahili dictionaries, namely *Kamusi ya Kiswahili Sanifu Toleo la Tatu* (OUP, 2013), *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (LPL, 2015) and *Kamusi Elezi ya Kiswahili* (JKF, 2016). The research was guided by mediostructures theory and aimed to meet the following objectives: identify elements of cross-referencing in the selected dictionaries, comparing and contrasting the use of cross-referencing in the said dictionaries, discussing the effects of cross-referencing in the dictionaries, and proposing, based on the findings of the research, how to better apply cross-referencing in Kiswahili monolingual dictionaries. The biggest part of the research was carried out in the library as it involved going through the selected Kiswahili monolingual dictionaries and picking out aspects of the dictionaries that can be cross-referenced. Publishers and the end users of the dictionaries were interviewed and their views integrated in the research. The data collected was analysed on the backdrop of the mediostructures theory and the findings presented in a qualitative approach. This research will bring light into how to effectively apply cross-referencing in the development of Kiswahili monolingual dictionaries.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0 Usuli wa Mada

Mada ya utafiti huu ina msingi wake katika taaluma ya leksikografia. Kulingana na Svensen (1993:1), “leksikografia ni tawi la isimu tumikizi linalohusu kuchunza, kukusanya, kuchagua na kueleza vipashio kutoka kwenye kanzi ya maneno ya lugha moja au zaidi.” Anasema kuwa kwa kawaida taaluma hii hufasiriwa kama “uundaji wa kamusi”, hali ambayo inasisitiza zaidi zao la mchakato huo; yaani kamusi. Mdee (1997) akimnukuu Wiegand (1984) anasema kuwa leksikografia ni kazi ya kisayansi ya kutunga kamusi. Bergenholtz na Gouws (2012) wanasema kuwa leksikografia imeainishwa katika taaluma mbili zinazohusiana: leksikografia kiutendaji inayohusu uundaji, uandishi na uhariri wa kamusi; na leksikografia kinadharia inayohusu uchanganuzi na usawiri wa uhusiano wa kisemantiki, kisintaksia na miundo iliyomo ndani ya leksimu za lugha, uundaji wa nadharia zinazohusu vipengele na miundo inayounganisha data za kamusi, na jinsi ambavyo watumiaji wa kamusi wanavyoweza kuzipata data hizo. Utafiti huu utajikita katika kategoria ya kwanza ya leksikografia kiutendaji.

Akimnukuu Zgusta (1971), Mdee (1997) anasema kuwa kamusi ni kitabu cha marejeo chenye msamiati uliokusanywa kutoka kwa wazungumzaji fulani, na kupangwa kwa utaratibu maalum, kisha kufafanuliwa kwa namna ambayo

msomaji anaweza kuelewa. Maneno yanayoingizwa katika kamusi huorodheshwa kwa mpangilio fulani. Kulingana na Mdee, maneno haya yanaweza kupangwa kwa kuzingatia utaratibu wa kialfabeti ambapo majina yanayoanza kwa herufi moja huwekwa katika orodha moja, au kwa mpango wa kikoaleksimu (kundi la maneno yenye uhusiano wa kimaana) ambapo maneno yanayohusiana kimaana huorodheshwa pamoja. Mdee anasema kuwa uorodheshaji wa kikoamaana ulitumiwa na Peter Mark Roget alipotunga thesauru yake mwaka wa 1852, na McArthur alipotunga kitabu chake kilichoitwa *Longman Lexicon of Contemporary English* mnamo 1981. Kulingana na Mdee, kasoro ya mpangilio wa kialfabeti ni kwamba maneno yasiyo na uhusiano wa kimaana hufuatana, na yale yaliyo na uhusiano wa kimaana k.v. mbuzi, paka, kondoo na ng'ombe (wote ni wanyama) hutokea kwenye sehemu tofauti kwenye kamusi na hivyo kumnyima mtumiaji wa kamusi kuuona uhusiano huu. Hata hivyo, mpangilio wa kialfabeti ndio uliokubalika katika kuorodhesha maneno ya kamusi kwani mpangilio huu humrahisishia mtumiaji kupata neno analolitafuta.

Kamusi zinaweza kuainishwa kwa kuzingatia vipengele mbalimbali, kikiwemo kile cha idadi ya lugha zilizotumiwa katika kamusi (Mdee, 1997). Kwa msingi huu, kamusi huweza kuwa wahidiya au thaniya. Kamusi wahidiya ni kamusi iliyoandikwa kwa lugha moja tu, kama vile Kiswahili au Kiingereza, na huwalenga wazawa wazungumzaji wa lugha hiyo na wakati mwingine huwafaa wanaojifunza lugha hiyo kama lugha ya pili au ya kigeni, kama vile *Kamusi ya*

Kiswahili Sanifu (2013), *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2015), *Kamusi Elezi ya Kiswahili* (2016), *Kamusi ya Karne ya 21*, *Kamusi la Kiswahili Fasaha* (2010), *Kamusi Teule ya Kiswahili* (2014) na *Kamusi Pevu ya Kiswahili* (2016). Kamusi thaniya ni ile iliyotumia lugha mbili, yaani vidahizo huandikwa kwa lugha moja na maelezo ya maana kutolewa kwa lugha nyingine, kama vile *A Standard Swahili-English Dictionary* (1939), *A Standard English-Swahili Dictionary* (1939), *Kamusi ya Kiswahili-Kiingereza* (2014), *A Concise English-Swahili Dictionary* (2002) na *English-Swahili Dictionary* (2006).

Kamusi pia huweza kuainishwa kutegemea viwango vya watumiaji wanaolengwa. Kuzingatia kigezo hiki kuna kamusi zinazowalenga watumiaji wa kiwango cha juu kuanzia shule za upili kwenda juu au watumiaji wa kawaida kwa jumla, kama zilizotajwa hapa juu; zinazowalenga watumiaji wa kiwango cha kati, kama vile wanafunzi wa shule za msingi, kama vile *Kamusi ya Shule za Msingi* (2007) na *Kamusi Sanifu ya Msingi* (2016); na zile zinazowalenga watumiaji wanaoanza kujifunza lugha, kama vile *Kamusi ya Watoto* (2011) na *Kamusi Bora ya Watoto* (2015).

Kamusi inaweza kuitwa “matini zinazowasilisha taarifa” (Svensen, 1993:2). Hata hivyo, ina vipengele vinavyoitofautisha na matini nyingine kama hizo. Kwa kawaida kamusi huwa haiwasilishi matini kwa msuko wa moja kwa moja ila imegawanywa katika maelfu ya sura fupifupi zinazojulikana kama vitomeo, ambavyo hupangwa bila kufuata utaratibu wa mada bali mpangilio wa kiabjadi

kutegemea tahajia ya vitomeo. Kimsingi, huu ni utaratibu wa kamusi ambao aghalabu sio utaratibu wa kawaida katika matumizi ya kila siku ya maneno ya lugha. Hii ni kwa sababu, maneno mbalimbali ya lugha huwa na uhusiano na ni jukumu la watunzi wa kamusi kuuonesha uhusiano huo ambao huweza kuoneshwa kupitia urejeleano. Gouws na Prinsloo (2005:178) wanasema kwamba “urejeleano ni mbinu ya kileksikografia inayoweza kutumiwa kuonesha uhusiano kati ya vipengele tofauti vya kamusi”. Pia wanamnukuu Wiegand (1996c:11) anayesema kuwa “urejeleano huunganisha vipengele vilivyowakilishwa katika sehemu tofautitofauti za kamusi katika viwango mbalimbali vya kileksikografia ili kuunda mtandao”. Wanasema kuwa mbinu ya urejeleano inaweza kumwelekeza mtumiaji wa kamusi kutoka matini moja kwenda nyingine, kwa mfano, kutoka matini iliyo katika sehemu ya utangulizi, ndani ya kamusi au mwishoni mwa kamusi palipo na viambatisho, au baina ya vidahizo katika kamusi. Maoni haya yanaungwa mkono na Alberts (2007) anayesema kuwa urejeleano ni mbinu ya kileksikografia ambayo inaweza kutumiwa kuonesha uhusiano baina ya vipengele mbalimbali vya kamusi na hivyo kuleta muumano wa kimatini katika kamusi.

Utafiti huu ulilenga kuchunguza kamusi wahidiya kwani kamusi zilizoteuliwa kutafitiwa zote ni za lugha moja – Kiswahili. Kamusi yoyote ile huwa na maneno mbalimbali yanayojumuisha kategoria zote. Maneno haya yanapoingizwa katika kamusi huunda vidahizo na hatimaye vitomeo. Taarifa zinazojumuishwa katika kitomeo, kando na fasili, ni kama vile matamshi,

kategoria ya neno (iwapo neno hilo ni nomino, kitenzi, kiwakilishi, kivumishi au kielezi), wingi na ngeli za nomino, uelekezi wa kitenzi (elekezi au sielekezi), mnyambuliko wa kitenzi pale unapokubalika, nahau, na misemo au methali inayoandamana na kidahizo.

Wakati mwingine vidahizo tofauti huweza kuwa na uhusiano wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja, kama vile kuweza kuwa na umbo jingine la kidahizo hicho, kuwa na kidahizo kingine ambacho kina tahajia tofauti lakini kina maana sawa na hicho, na uhusiano wa ukinzani au kinyume. Itakuwa vyema iwapo watunzi wa kamusi watamwelekeza mtumiaji wa kamusi kuuona uhusiano uliopo baina ya vidahizo kama hivi. Pia, vipashio mbalimbali vilivyoingizwa kwenye kidahizo kimoja huenda vikawa vinahusiana na vingine katika vidahizo tofauti kwa namna moja au nyingine. Kwa mfano, methali huundwa kwa maneno tofauti ambayo, aghalabu huwa yameshughulikiwa kama vidahizo tofauti katika kamusi. Methali *Kenda karibu na kumi*, kwa mfano, imeundwa kwa maneno manne (kenda, karibu, na, kumi) ambayo huenda yote yameingizwa kama vidahizo katika kamusi. Utafiti huu ulilenga kuibua mwanga kuhusu namna ya, kwa mfano, kuishughulikia methali kama hii pale watunzi wa kamusi wanapoamua kuiingiza kwenye kamusi ya lugha. Je, tuiingize methali hii katika vidahizo vyote vinne? Iwapo la, tutaiingiza wapi na kwa kuzingatia kigezo kipi? Na iwapo tutaiingiza katika kidahizo kimoja tu, kuna jinsi ambavyo tunaweza kupahusisha ilipoingizwa na maneno mengine yanayoiunda?

1.1 Suala la Utafiti

Katika uundaji wa kamusi, wanaleksikografia husisitiza iktisadi, pamoja na lugha kienzo. Mbinu nyingine muhimu inayoweza kuchangia dhana ya iktisadi ni urejeleano, iwapo utafanywa kwa umakinifu unaostahili. Kwa mujibu wa Gouws na Prinsloo (2005), urejeleano haujatumiwa inavyostahili katika kamusi nyingi za lugha za Kiafrika. Kiswahili, kama lugha walizozishughulikia waandishi hawa, ni lugha ya Kibantu. Lugha hii pia imeandikiwa kamusi nyingi za lugha moja na itakuwa vyema kuchunguza iwapo kamusi hizo zimeepuka makosa hayo ya kiurejeleano au la. Utafiti huu umeonesha ni vipashio vipi vinavyoweza kuhusishwa kupitia urejeleano, namna urejeleano huu unastahili kuhusisha vipashio hivyo, pamoja na kutathmini ubora wa mchakato huo katika kamusi zilizoteuliwa.

1.2 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulikusudiwa kutimiza mambo manne:

- i. Kubaini vipengele vya urejeleano vilivyotumiwa katika kamusi teule za Kiswahili (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu, Kamusi Kuu ya Kiswahili, Kamusi Elezi ya Kiswahili*).
- ii. Kulinganisha na kulinganua matumizi ya urejeleano katika kamusi teule za Kiswahili.
- iii. Kujadili athari ya urejeleano kama ulivyotumiwa katika kamusi teule za Kiswahili.

- iv. Kupendekeza, kutegemea matokeo ya utafiti, namna ya kuboresha urejeleano katika kamusi za Kiswahili za lugha moja.

1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulielekezwa na maswali yafuatayo:

- i. Ni vipengele vipi vya urejeleano vilivyotumiwa katika kamusi teule za Kiswahili?
- ii. Je, kamusi teule zimekishughulikia kipengele cha urejeleano kwa namna sawa, na iwapo la, tofauti zinazojitokeza ni zipi?
- iii. Je, urejeleano, kama ulivyoshughulikiwa katika kamusi teule za Kiswahili, una athari gani kwa mtumiaji na mchapishaji wa kamusi?
- iv. Ni kwa namna gani tunaweza kuboresha urejeleano katika kamusi za Kiswahili za lugha moja?

1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Wataalamu wengi wamefanya tafiti mbalimbali kuhusu vipengele vya kamusi za Kiswahili na kupendekeza jinsi vinavyopaswa kuwasilishwa. Hata hivyo, kwa ufahamu wangu, hadi sasa hakuna utafiti, hasa wa kulinganisha kamusi mbalimbali, uliofanywa kuhusu kipengele cha urejeleano katika kamusi za Kiswahili. Utafiti huu umependekeza jinsi matumizi ya mbinu ya urejeleano yanaweza kuboreshwa ili kufanikisha kuwepo kwa kamusi zenye taarifa nyingi

bila kuchukua nafasi kubwa, pamoja na kunogesha taarifa atakazozipata mtumiaji wa kamusi. Kwa kawaida mtumiaji hutumia kamusi kwa kuwa kuna maelezo anayoyatafuta kuhusiana na neno fulani. Hata hivyo, pale ambapo urejeleano umefanywa kwa njia inayofaa, kando na taarifa alizozikusudia, mtumiaji wa kamusi ataweza kupata taarifa zaidi, kwa mfano iwapo neno hilo lina kabadala, neno au maneno mengine yenye maana sawa na hilo, pamoja na nahau zinazotumia neno husika. Udurusu wa juujuu wa kamusi ya Kiingereza ya lugha moja, *Oxford Advanced Learner's Dictionary 9th Edition* unaonesha kuwa waandishi wamekitumia kipengele cha urejeleano kuhusisha vipengele vingi vikiwemo visawe, antonimu, vidadala, misemo, methali na jinsia. Urejeleano huu unaonekana kufanywa kwa umakinifu wa hali ya juu, jambo ambalo humwacha mtumiaji wa kamusi hii akiwa amepata taarifa anuwai zinazohusiana na kidahizo fulani.

Kamusi totauti zilizoandikiwa lugha moja, kwa kiwango kikubwa, zinastahili kuzingatia msingi sawa kuwasilisha dhana fulani kwa namna zile zile ili kuepuka kuwakanganya watumiaji wa kamusi hizo. Hata hivyo, hali hii haionekani kuwa hivyo katika kamusi zilizoteuliwa kwani kuna namna tofauti za kukiangazia kipengele cha urejeleano, jambo ambalo linamwacha mtumiaji wa kamusi bila kujua ni namna gani vipengele fulani vinaweza kuhusishwa.

Ukubwa wa kamusi aghalabu huelekezwa na idadi ya vidahizo katika kamusi pamoja na taarifa zinazolingizwa chini ya kila kidahizo ili kuunda vitomeo. Hii

inamaanisha kuwa iwapo vidahizo ni vingi kamusi itakuwa kubwa na vivyo hivyo iwapo ni vichache bila shaka kamusi itakuwa ndogo. Hata hivyo, kama ilivyotajwa kwingine katika tasnifu hii, lugha ya Kiswahili huwa na vibadala na pia visawe – kamili na visivyo kamili. Kulingana na Svensen (1993) na Gouws na Prinsloo (2005), maneno haya yataingizwa katika kamusi lakini ni makosa kuyapa umuhimu sawa kama vidahizo. Utafiti huu hivyo basi umebainisha baadhi ya maneno haya na jinsi yalivyoshughulikiwa katika kamusi teule na, pia kupendekeza namna ya kuyarejelesha ili kumpunguzia mtunzi/mchapishaji nafasi ambayo aghalabu huandamana na gharama ya juu.

1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Kama ilivyoelezwa katika kurasa 2 na 3 za tasnifu hii, kamusi za lugha moja za Kiswahili ni nyingi. Hata hivyo, kamusi zifuatazo zinazowalenga watumiaji wa kiwango cha juu ndizo zilizochaguliwa kwa ajili ya utafiti huu:

- *Kamusi ya Kiswahili Sanifu Toleo la 3* (2013)
- *Kamusi Kuu ya Kiswahili Toleo* (2015)
- *Kamusi Elezi ya Kiswahili* (2016)

1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ya Utafiti

Kipengele cha urejeleano kimewavutia wataalamu kadha waliokianguzia katika maandishi mbalimbali. Urejeleano ni kipengele kimoja tu katika taaluma pana ya leksikografia na hivyo ni vigumu kukitaja kipengele hiki bila kuitaja

leksikografia. Kwa sababu hii, sehemu hii itarejelea yaliyoandikwa katika mada mbili pana: Leksikografia kwa jumla, na urejeleano.

1.6.1 Leksikografia

Katika kitabu chao, Gouws na Prinsloo (2005) wameangazia vipengele vingi vinavyohusika katika uundaji wa kamusi ikiwemo miundo mbalimbali ya matini zinazoiunda kamusi, kama vile muundomakro (muundo na ukubwa wa kamusi kutegemea idadi ya vidahizo), muundomaikro (taarifa zote zinazoandamana na kidahizo) na muundomedio, yaani urejeleano. Katika kitabu hiki, waandishi hawa wamekishughulikia kipengele cha urejeleano katika anwani “Urejeleano kama Mbinu ya Kileksikografia” katika mtandao mpana wa utunzi wa kamusi. Waandishi hawa wameangazia kwa mapana nadharia ya urejeleano (miundomedio) kama ilivyopambanuliwa na mwasisi wayo – Wiegand (1996), na wakafafanua vipengele vinavyohusishwa katika urejeleano na mchakato mzima wa urejeleano. Pia, wameeleza aina mbalimbali za urejeleano, kama vile urejeleano wa ndani na urejeleano wa nje. Waandishi hawa wametumia mifano kutoka kwa kamusi za Kiingereza za lugha moja na hata zile za lugha mbili. Kwa kuwa hiki ni kitabu, waandishi hawajajikita katika kuchanganua kamusi yoyote kwa kina bali wanaelekeza jinsi urejeleano unavyopaswa kushughulikiwa. Kitabu hiki kilikuwa mhimili mkuu katika utafiti huu kwani kimeieleza kwa kina nadharia ya miundomedio, ambayo ndiyo iliyotumiwa katika utafiti huu.

Svensen (1993) ameandika kuhusu mchakato mzima wa uundaji wa kamusi kamilifu na akaeleza umuhimu na aina za urejeleano pamoja na vipengele vinavyoweza kuhusishwa kwa kuvirejelesha. Kitabu hiki pia kilikuwa daraja muhimu katika kuafikia malengo ya utafiti huu.

Alberts (2007) katika makala yake ameangazia kwa jumla vipengele ambavyo huunda kamusi itakayomridhisha mtumiaji. Ameeleza kwa kina miundo mitatu ya kamusi, yaani muundo makro, muundo maikro na muundomedio. Ameeleza umuhimu wa muundomedio (urejeleano) katika kuhusisha vipengele vilivyo katika sehemu tofauti katika kamusi. Makala haya yalichangia pakubwa katika kuafikia malengo ya utafiti huu.

Prinsloo (2009) ameangazia changamoto wanazokumbana nazo watunzi wa kamusi za lugha za Kibantu za Afrika Kusini kuhusiana na uteuzi wa vidahizo vinavyotokana zaidi na nomino na vitenzi. Hii ni kwa sababu vingi vya vitenzi vya Kibantu huchukua viambishi, ikikumbukwa kuwa katika matumizi ya kawaida ya lugha, mizizi ya vitenzi hutumiwa kwa nadra sana ikilinganishwa na vitenzi vilivyoambishwa. Pia, nyingi za nomino za Kibantu huwa na maumbo tofauti katika umoja na wingi, jambo ambalo mara nyingi ni tofauti na ilivyo lugha ya Kiingereza. Hivyo basi, tatizo kwa watunzi wa kamusi hizi huwa ni: je, wataingiza maumbo yote mawili katika kamusi na kuyatolea maana? Kulingana na makala hii, iwapo hili litafanyika kutakuwa na uradidi wa taarifa nyingi pamoja na kutumia nafasi kubwa hali inayokinzana na kanuni

ya iktisadi katika utunzi wa kamusi. Mwandishi anasema kuwa watunzi wa kamusi aliyokuwa akiihakiki ya *Oxford Northern Sotho School Dictionary* walifuata mkondo mwafaka wa kuyaingiza maumbo ya wingi ya nomino kama vidahizo bila kuyatolea fasili na badala yake wakayahusisha na yale ya umoja kwa kutumia mbinu ya urejeleano. Kwa mfano, katika uk. 13: Mfano 1:

[**ba'sadi**, n. pl., of **mosadi**, women.]

[**mo'sadi**, n. a woman, a wife ...]

Kiswahili, kama lugha ya Kibantu, pia huwa na changamoto kama hizi katika uteuzi wa vidahizo vya kuingizwa katika kamusi. Hivyo makala hii itachangia pakubwa kuelekeza mtazamo huu katika kamusi zilizoteuliwa katika utafiti huu.

Katika makala yake, Geeraerts (2016) anasema kuwa leksikografia ni tawi la isimu tumikizi, na kinadharia huhusishwa na leksikolojia, na hatimaye semantiki leksia kwa kuwa kimsingi hueleza maana za maneno. Mwandishi huyu ameeleza kwa kina uhusiano uliopo kati ya semantiki na leksikografia, hasa semantiki miundo na jinsi ambavyo maneno huunda mfumo na hatimaye “uwanja wa kileksia” na kwa hivyo makala hii ilirejelewa kufanikisha utafiti huu.

Nkomo (2008) alifanya utafiti kuhusu kielelezo cha kinadharia cha lugha kwa matumizi maalum (Leksikografia ya Kidebele katika kamusi ya isimu na

msamiati wa kifasihi). Katika utafiti huu, Nkomo amerejelea kamusi nyingi za taaluma mbalimbali kama vile muziki, fasihi, matibabu, kamusi ya viwanda, na elektroniki. Utafiti huu umeangazia namna ya kuingiza vibadala na sinonimu katika kamusi hizi. Anatoa mfano wa “little finger” katika kamusi ya Kindebele ya Muziki, kidahizo ambacho anasema kina visawe sita na kimeingizwa pale kwa kuwa kidole hiki hutumiwa katika upigaji wa gita. Nkomo anapendekeza kuwa watunzi wanastahili kuwa makini kwani baadhi ya lugha hizi za Kibantu bado zinaendelea kusanifishwa na hivyo maneno yaliyosanifishwa tu ndiyo yanayostahili kuingizwa kwenye kamusi na uhusiano uliopo kuoneshwa kupitia urejeleano.

Kiango (2006) alifanya utafiti uliolenga kubainisha namna ya kuviingiza vinyambuo-nomino katika kamusi za Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yalionesha njia tatu za kileksikografia zilizotumiwa kuvishughulikia vinyambuo-nomino vya vitenzi katika kamusi sita zilizokuwa zimeteuliwa katika utafiti huo. Njia hizo ni: kama kitomeo kamili, si kitomeo kamili, na kitomeo kamili chenye mrejeano. Njia ya tatu ndiyo iliyo na uhusiano wa moja kwa moja na utafiti wetu na hivyo utafiti huu wa Kiango ulikuwa wa manufaa kwetu. Anaeleza kuwa njia hii ilitumiwa na Madan (1903) na Rechenbach (1968) pale ambapo urejeleano wa kulinganisha ulipotumika. Kwa mfano katika uk. 69:

lima, v. hoe, the only native mode of cultivation, hence generally ‘cultivate, work land’ (cf. mlimo, mkulima, kilimo).

1.6.2 Urejeleano

Gouws (1998) ameanzizia urejeleano kama mbinu ya kileksikografia inayomwezesha mwanaleksikografia kuunganisha maneno yanayohusiana kwa namna mbalimbali na hivyo kumpa mtumiaji fursa ya kupata taarifa zaidi.

Nkomo (2007) ameanzizia urejeleano katika kamusi ya lugha moja ya Kindebele ambayo inawalenga wazungumzaji wa Kindebele pamoja na wanafunzi katika shule za sekondari, vyo vya kati na vya juu. Katika makala hii mwandishi anaonesha jinsi watunzi wa kamusi hii ya Kindebele waliweza kuokoa nafasi kwa kutumia urejeleano. Kwa mfano, anamnukuu mmoja wa wahariri wa kamusi hii akisema kuwa urejeleano uliwawezesha kuingiza vidahizo elfu ishirini katika kamusi ya kurasa mia sita. Hata hivyo, katika makala hii, Nkomo anaona kuwa urejeleano haukumakinikiwa ipasavyo kwani bado kuna visawe vilivyo na fasili zilizorudiwarudiwa katika vidahizo husika kama vile **ikhe-hla/ixhegu** (mwanamume mzee), **abalozi/idlozi** (mhenga/wahenga), na vidadala kama vile **isingake-thiso/isingathekiso** (isitiari), pale ambapo kila moja ina fasili ile ile (uk. 378). Kulingana na Nkomo, nadharia ya miundomedio inaelekeza kuwa fasili iwekwe katika kidahizo kimoja kilicho na matumizi mapana na kuonesha uhusiano baina ya vidahizo vingine na pale ilipo fasili kwa njia ya urejeleano ili kuokoa nafasi katika kamusi na pia kuepuka uradidi. Kindebele ni lugha ya Kibantu kama ilivyo lugha ya Kiswahili na kwa sababu hii zina sifa mbalimbali

zinazolingana, kama vile wingi wa vidadala na visawe. Kwa sababu hiyo, makala hii ilikuwa nguzo muhimu katika kufanikisha utafiti huu.

Tarp (1999) ameeleza zaidi vipengele vinavyostahili kuhusishwa katika nadharia ya urejeleano, kama vile uhakiki wa kamusi zilizochapishwa na uundaji wa dhana za urejeleano ambazo zinaweza kutumiwa katika uundaji wa kamusi. Anatoa mfano wa kamusi ya kidhahania ya lugha mbili (Kijerumani–Kiingereza) ili kuonesha mfano wa urejeleano unaostahili kuepukwa kwani unamzungusha mtumiaji wa kamusi bila kumkidhia mahitaji yake. Anatoa mfano huu wa visawe vya Kijerumani (uk. 119):

Aufzug *m* lift

Fahrstuhl *m* lift

Lift *m* lift

Kulingana na Tarp, urejeleano wa aina hii, ambao huenda ukakumbana nao katika kamusi zilizochapishwa, humtamausha anayeitumia kamusi. Anasema kwamba mfano kama huu ni msingi wa kuihakiki kamusi bali sio mhimili wa nadharia ya urejeleano. Tarp anaeleza taratibu zinazoelekeza urejeleano, pamoja na pale unapostahili na usipostahili. Kwa msingi huu, makala hii ilichangia pakubwa katika utafiti huu kwani ilitupa mizani ya kupimia vipengele vya urejeleano katika kamusi teule za Kiswahili.

Siepmann (2006) ameangazia jinsi ya kuyaingiza mafungu ya maneno, kama vile methali, nahau na misemo, katika kamusi. Akimnukuu Petermann (1983), anasema kuwa mafungu haya yanapaswa kuingizwa katika kila neno linaloliunda fungu hilo lakini fasili kuingizwa mara moja tu katika neno moja na urejeleano kutumiwa kuyahusisha maneno mengine na fungu husika. Uteuzi wa kidahizo ambapo fasili huingizwa kutategemea maneno yaliyoliunda fungu hilo. Kwa mfano, iwapo kuna nomino, fasili iwekwe katika nomino, iwapo kuna nomino zaidi ya moja, fasili iingizwe katika nomino ya kwanza. Iwapo hakuna nomino, utaratibu wa kitenzi, kielezi, kivumishi, na kuendelea, ufuatwe. Makala hii ilielekeza uchanganuzi wa methali, nahau na misemo kutoka kwenye kamusi teule katika utafiti huu.

Grimes (1984) anasema kuwa urejeleano humsaidia mwanaleksikografia kufikisha tamati hali ambapo maelezo yamerejeleshwa. Kulingana naye urejeleano huu humwelekeza mtumiaji kwa dhana nyingine zinazohusiana na kidahizo ambacho ni chanzo cha urejeleano. Pia, anazungumzia dhana nyingine ya kipekee inayosema kwamba urejeleano huhakikisha kuwa maneno yote yaliyotumiwa kutoa fasili za vidahizo nayo yameingizwa katika kamusi kama vidahizo. Utafiti huu ulitumia kigezo hiki kubaini iwapo mfumo wa urejeleano katika kamusi zilizochanganuliwa unamfikisha mtumiaji wa kamusi katika tamati aliyoikusudia.

Kiango (1996) anaeleza namna ya kushughulikia vibadala, misemo, nahau na methali katika kamusi. Ni dhahiri kwamba makala yake imejikita katika ‘walivyokubaliana kufanya’ katika toleo la pili la *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* ambayo ilichapishwa 2004. Kulingana naye, kamusi inapaswa kuingiza kibandala kilichokubalika kuwa sanifu pekee na kuvipuuza vingine. Hata hivyo, mwandishi huyu hajatuambia namna ya kuvishughulikia vibadala viwili ambavyo vina uzito sawa, au pale ambapo watunzi wa kamusi wanapoona umuhimu wa kuviingiza vibadala vyote katika kamusi. Katika kuingiza methali, nahau na misemo anapendekeza kuzingatia neno la msingi au la kwanza. Hata hivyo, hapa hajaelekeza namna ya kuyarejelesha maneno mengine yanayoziunda tungo hizi. Kiango (1996) anasema kuwa wako wanaleksikografia wanaopendekeza kuingiza methali, nahau au msemu chini ya kila neno linalotajwa katika mtungo huo. Hata hivyo, anasema kuwa utaratibu huu umeonekana kuwa huchukua nafasi kubwa katika kamusi kwa sababu ya kurudiarudia.

Modiba (2011) alifanya utafiti uliohusu kuhakiki na kulinganisha urejeleano katika kamusi ya lugha moja ya Kisotho cha Kaskazini na ile ya lugha mbili – Kisotho cha Kaskazini na Kiingereza. Katika utafiti huu, anaonesha kuwa watunzi wa kamusi husika hawakuushughulikia urejeleano kwa kuzingatia kanuni na nadharia za kileksikografia. Utafiti huu hata hivyo, umeangazia urejeleano katika vipengele viwili tu: sinonimu na antonimu.

Ni dhahiri kuwa maandishi haya yameangazia dhana ya urejeleano kwa namna moja au nyingine na hivyo yalitegemewa sana katika utafiti huu. Hata hivyo, mengi ya maandishi haya yamejikita katika vipengele vichache ambavyo vinaweza kuhusishwa katika urejeleano, kama vile visawe na vibadala. Utafiti huu, hata hivyo, ulihusisha vipengele zaidi kama ilivyokwisha kutajwa kwingineko katika tasnifu hii. Pia, baadhi ya tafiti hizi zimeshughulikia kamusi za lugha zaidi ya moja kinyume na utafiti huu ulioshughulikia kamusi za lugha moja tu. Hatimaye, tafiti hizi zimeshughulikia kamusi za lugha mbalimbali, ila hamna ule ulioshughulikia kamusi za Kiswahili, kama utafiti huu ulivyofanya.

1.7 Misingi ya Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya miundomedio (mediostuctures). Nadharia hii iliasisiwa na Herbert Hierst Wiegand, mwanaleksikografia Mjerumani mnamo mwaka wa 1996. Kulingana na Wiegand, kamusi ni chombo kinachobeba matini za aina mbalimbali ambazo zinahusiana kwa namna moja au nyingine. Mwanaleksikografia huyu aliona haja ya kuwepo msingi madhubuti wa kuonesha uhusiano uliopo baina ya matini hizi. Wiegand alipendekeza kuwepo kwa masharti ya urejeleano ambayo aliyaaanisha kama yale yanayohusiana na mada za kamusi, na yale yanayohusiana na muundo wa kamusi. Masharti yanayohusiana na mada za kamusi yanahusu uhusiano uliopo baina ya kauli mbili za kiisimu na kujidhihirisha katika viwango vyote vya maelezo vya kileksikografia, viwe vya kifonolojia, kimofolojia, semantiki ya leksia, na vinginevyo. Masharti ya pili ya kiurejeleano yanayohusu muundo wa

kamusi yanajikita katika mpangilio au muundo wa vipengele mbalimbali vya kamusi.

Tarp (1999) aliendeleza nadharia ya miundomedio kupitia uhakiki wake wa yale yaliyokwishaandikwa na Wiegand. Kulingana na Tarp, masharti yaliyozungumziwa na Wiegand yalikuwa muhimu sana ili kuiunda nadharia ya miundomedio. Hata hivyo, kwa maoni ya Tarp, ili nadharia ya miundomedio ya kileksikografia ikamilike ni sharti ihusishe uhakiki wa kamusi zilizochapishwa tayari, pamoja na uundaji wa dhana na kanuni za kiutendaji kwa lengo la kuboresha kamusi zitakazochapishwa baadaye. Ili kufanikisha hili, Tarp anasema kwamba ni muhimu kujumuisha dhana za kiuamilifu za kamusi pamoja na muundo wa usambazaji katika nadharia ya miundomedio.

Nadharia ya miundomedio huvitazama vipengele vya kamusi kama viungo vinavyohusiana na vinavyouunda muundo mzima wa kamusi. Vipengele hivi vya kimuundo vinaweza kuwa katika kitomeo kimoja au zaidi, vikawa katika sehemu ya utangulizi ya kamusi au katika kurasa za mwisho ambapo kuna habari zaidi.

Mihimili ya Nadharia ya Miundomedio

Gouws na Prinsloo (2005) wakimnukuu Wiegand (1996c) wanaifafanua mihimili ifuatayo ya nadharia hii:

- i. Ni sharti kuwepo na chanzo cha urejeleano. Hiki ni kidahizo ambacho kutoka kwacho mtumiaji anaelekezwa pahali pengine palipo na taarifa inayohusiana na kidahizo hicho.
- ii. Kuwepo kwa anwani ya urejeleano. Hiki ni kidahizo ambacho huwa na taarifa ya ziada ambayo mtumiaji alielekezwa kuipata. Kuna aina mbili za anwani hii ya urejeleano: anwani ya ndani ya urejeleano na anwani ya nje ya urejeleano. Anwani ya ndani ya urejeleano huwa chini ya kile kile kidahizo ambacho ndicho chanzo cha urejeleano. Anwani ya nje ya urejeleano huwa ya aina mbili: huwa nje ya kidahizo ambacho ni chanzo cha urejeleano, na pia inaweza kuwa katika matini yaliyo nyuma ya kamusi k.v. majedwali au taarifa nyingine ambazo zina uhusiano na chanzo cha urejeleano.
- iii. Kuwepo kwa alama ya urejeleano. Alama hii huwa ni kiashiria ambacho watunzi wameafikiana kitamwelekeza mtumiaji wa kamusi pale palipolengwa na hivyo kuwa kama daraja la kuonesha uhusiano wa kiurejeleano baina ya chanzo cha urejeleano na anwani ya urejeleano. Kwa mfano, kuna wale ambao hutumia ishara ya mshale, kidole, na misimbo mingine mbalimbali huku wengine wakitumia maneno, au vifupisho vya maneno, kama vile **taz** (tazama), **pia**, **taz pia**, na **linga** (linganisha).
- iv. Mwanaleksikografia humwelekeza mtumiaji wa kamusi kutoka kwa chanzo cha urejeleano kuelekea kwenye anwani ya urejeleano.

Mihimili hii yote kwa hakika ndiyo msingi wa kipengele cha urejeleano na hivyo ilitufaa sana kuufanikisha utafiti huu.

1.8 Mbinu za Utafiti

Sehemu hii inaangazia muundo wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za kukusanya data, uchanganuzi wa data, pamoja na uwasilishaji wa matokeo.

1.8.1 Muundo wa Utafiti

Kwa mujibu wa Kothari (2004), muundo wa utafiti unajumuisha dhana kama vile *nini, wapi, lini, kwa kiasi gani, na kwa namna gani* kuhusu suala la utafiti. Huu ni mpangilio wa hali ya kukusanya na kuchanganua data kwa namna ambayo inalenga kuunganisha umuhimu wa utafiti na iktisadi katika mchakato wote. Kwa kuwa data ya utafiti huu ilinukuliwa kutokana na kamusi zilizoteuliwa, basi utafiti huu, kwa kiwango kikubwa ulifanyiwa maktabani.

1.8.2 Eneo la Utafiti

Kothari (2004) anasema kuwa kuna aina tatu za utafiti ambazo aghalabu huelekeza mbinu za utafiti pamoja na eneo la utafiti, ambazo ni utafiti wa maktabani, utafiti wa nyanjani na utafiti wa maabarani. Anasema kuwa utafiti wa maktabani unahusu uchanganuzi wa kumbukumbu za kihistoria na ule wa nyaraka mbalimbali. Utafiti huu ulifanyiwa maktabani na nyanjani. Maktabani,

kamusi teule zilipitiwa na data kunukuliwa moja kwa moja. Pia, vitabu mbalimbali, makala na hata tasnifu zilizoandikwa kuhusiana na mada hii zilipitiwa. Mahojiano pia yalitumiwa kupata maoni ya wachapishaji na hojaji zikatumiwa kupata maoni ya watumiaji wa kamusi za Kiswahili.

1.8.3 Sampuli na Usampulishaji

Kulingana na Kothari (2004), mara nyingi si rahisi kuchunguza kila kitu katika jumuiya. Hata hivyo, anasema kuwa kuna uwezekano wa kupata matokeo faafu kwa kuchunguza sehemu tu ya jumuiya yote.

1.8.3.1 Jumuiya

Kulingana na Mugenda na Mugenda (2003), jumuiya ni wahusika wote walio na sifa zinazofanana, ambazo ni tofauti na za wengine. Kothari (2004) naye anasema kuwa jumuiya ni jumla ya wahusika wote ambao taarifa inatakikana kutoka kwao. Hii inamaanisha kuwa kijumla kuna wahusika tofauti ambao wana sifa tofauti, lakini wanaolengwa katika utafiti huwa wale walio na sifa zinazohusiana. Katika utafiti wetu tulibainisha kuwa kuna kamusi anuwai za Kiswahili za lugha.

Kuna kamusi kadha za Kiswahili za lugha moja ambazo zimechapishwa hadi sasa. Kuna zile ambazo zinawalenga watumiaji walio na kiwango cha chini cha umilisi wa lugha ya Kiswahili, kiwango cha wastani na cha juu. Zile

zinazowalenga wa kiwango cha chini ni kama vile *Kamusi ya Watoto* (OUP: 2011) na *Kamusi Bora ya Watoto* (LPL: 2015). Zinazowalenga watumiaji wa kiwango cha kati ni kama vile *Kamusi ya Shule za Msingi* (OUP: 2007), *Kamusi Sanifu ya Msingi* (OUP: 2016) na *Kamusi Angaza kwa Shule za Msingi* (EAEP: 2011). Kamusi ya kwanza ya Kiswahili ya lugha moja ya kiwango cha juu kuchapishwa ilikuwa *Kamusi ya Kiswahili* iliyoandikwa na F. Johnson na kuchapishwa mwaka wa 1935. Hii ilifuatwa na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, iliyochapishwa mwaka wa 1981. Kamusi hii ilitungwa na TUKI na kuchapishwa na OUP. *Kamusi ya Maana na Matumizi* ilichapishwa mwaka wa 1992. Toleo la pili la Kamusi ya Kiswahili Sanifu lilichapishwa mwaka wa 2004. Kamusi nyingine zilizofuata ni kama vile *Kamusi ya Karne ya 21* toleo la kwanza (LPL: 2011), *Kamusi la Kiswahili Fasaha* (OUP: 2010), *Kamusi ya Karne ya 21 toleo la pili* (LPL: 2013), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu* (OUP: 2013), *Kamusi Teule ya Kiswahili* (EAEP: 2014), *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (LPL: 2016), *Kamusi Elezi ya Kiswahili* (JKF: 2016), na *Kamusi Pevu ya Kiswahili* (VM: 2016).

1.8.3.2 Usampulishaji

Usampulishaji uliotumiwa kuteua kamusi zilizotafitiwa ni ule wa kimakusudi. Kothari (2004) anasema kuwa katika usampulishaji wa kimakusudi, sampuli huteuliwa kwa kudhamiria kwa sababu watafiti wana imani kuwa sampuli hiyo itawakilisha jumuiya nzima na kutimiza malengo ya utafiti. “Usampulishaji wa kimakusudi humruhusu mtafiti kutumia sampuli zilizo na taarifa zinazohitajika

kwa mujibu wa utafiti wake” (Mugenda na Mugenda (2003:50). Kulingana na waandishi hawa, sampuli za utafiti huteuliwa kwa sababu zina sifa zinazohitajika. Kulingana na Kothari (2004), sampuli inastahili kuwa ya kiwango cha kadri; si kubwa mno na si dogo sana. Hata hivyo, vyovyote vile sampuli haistahili kuwa chini ya asilimia 30 ya jumua inayochunguzwa. Huu ndio msingi ulioelekeza ukubwa wa sampuli yetu.

Kamusi zilizochanganuliwa katika utafiti huu ni tatu pekee: *Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu* (2013), *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2016), na *Kamusi Elezi ya Kiswahili* (2016). Hizi ni kamusi za kiwango cha juu zinazowalenga wanafunzi wa shule za sekondari kwenda juu. Kuna sababu mbili muhimu zilizoelekeza uteuzi wa kamusi hizi tatu miongoni mwa zote zilizochapishwa hadi sasa, ambazo ni waandishi wa kamusi zilizoteuliwa na wachapishaji wa kamusi hizo. Kwa jumla kamusi zote zilizochapishwa hadi sasa zimeandikwa na taasisi, kama vile TUKI/TATAKI, mabaraza kama vile BAKITA na BAKIZA, na watu binafsi – kwa pamoja au hata mmoja peke yake. Katika utafiti huu, tuliteua kamusi moja iliyochapishwa na taasisi, nyingine na baraza na ya mwisho na watu binafsi. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* imeandikwa na TUKI/TATAKI, ambayo ni taasisi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, inayoshughulikia masuala ya Kiswahili ikiwemo uundaji na usanifishaji wa istilahi za Kiswahili. *Kamusi Kuu ya Kiswahili* imeandikwa na BAKITA, ambalo ni baraza linaloshughulikia uundaji na usanifishaji wa istilahi za Kiswahili. Tilitaka kuona namna waandishi hawa wawili, ambao wanahusika sana katika maendeleo ya Kiswahili, wamelishughulikia suala la urejeleano. *Kamusi Teule ya Kiswahili* imeandikwa na wataalamu kadha wa

lugha ya Kiswahili kwa pamoja. Katika kuangalia aliyechapisha kazi hizi, *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* imechapishwa na shirika la uchapishaji la OUP, ambalo ni idara ya uchapishaji ya Chuo Kikuu cha Oxford, Uingereza. *Kamusi Kuu ya Kiswahili* imechapishwa na LPL, ambalo ni shirika la kibinafsi, huku *Kamusi Elezi ya Kiswahili* ikichapishwa na JKF, ambalo ni shirika la serikali ya Kenya. Tulikusudia pia kuona jinsi wachapishaji hawa ambao wana misingi na sera tofauti walivyoushughulikia mchakato mzima wa uhariri na uchapishaji.

Kwa maoni yetu, kamusi hizi ziliwakilisha zile nyingine katika kategoria hii kwani masuala yaliyoibuliwa na utafiti huu yanapiga mwangwi katika kamusi nyingine zilizochapishwa hadi sasa.

1.8.4 Mbinu za Ukusanyaji Data

Data iliyotumiwa katika tasnifu hii ilipatikana kupitia mbinu tatu, yaani kusoma na kudondoa data moja kwa moja kutoka katika kamusi zilizoteuliwa, mahojiano na wachapishaji, na hojaji kwa watumiaji wa kamusi.

1.8.4.1 Udondaji wa moja kwa moja wa data

Kiwango kikubwa cha data ya uchunguzi ilinukuliwa moja kwa moja kutoka katika kamusi zilizoteuliwa na hivyo basi ilihitaji mtafiti kuzipitia kamusi hizi na kudondoa data iliyofaa kufanikisha malengo ya utafiti. Data iliyokusanywa

ni mifano ya vipengele vyote ambavyo vinaweza kuhusishwa kupitia urejeleano vikiwemo **vibadala, visawe** au **sinonimu, antonimu, wingi** na **umoja wa nomino, nahau, misemo,** na **methali**. Mifano ya vipengele hivi iliwekwa kwenye mizani ya mihimili ya nadharia ya miundomedio ili kuhakiki ufanisi wa mbinu hiyo katika kamusi teule.

1.8.4.2 Mahojiano na wachapishaji

Mahojiano, kama mbinu ya ukusanyaji data, yalitumiwa kupata maoni ya wachapishaji kuhusu vipengele ambavyo huchangia gharama ya uchapishaji wa vitabu, na mbinu ambazo huweza kutumiwa kupunguza gharama ya uchapishaji. Kiongozi cha mahojiano hayo kipo katika sehemu ya viambatisho ya tasnifu hii, kama Kiambatisho cha Pili.

1.8.4.3 Hojaji kwa watumiaji wa kamusi

Hojaji ilitumiwa kupata maoni ya watumiaji wa kamusi. Kwa kuwa kamusi zilizoteuliwa ni zile za kiwango cha juu, hojaji iliwalenga walimu na pia wanafunzi wa shule za upili. Hojaji iliyotumiwa ipo katika sehemu ya viambatisho ya tasnifu hii, kama Kiambatisho cha Tatu.

1.8.5 Uchanganuzi wa Data

Mugenda na Mugenda (2003) wanasema kuwa data inayokusanywa kutoka nyanjani huwa ghafi na huwa vigumu kuifasiri, na hivyo basi inahitaji kusafishwa, kusimbwa, kuingizwa kwenye tarakilishi na hatimaye kuchanganuliwa. Kulingana na Kothari (2004), uchanganuzi wa data unarejelea uhariri, usimbaji au usimbuaji, uainishaji, na upangaji wa data iliyokusanywa, kupitia kama vile majedwali, ili kurahisisha jinsi ambavyo itashughulikiwa. Data zilizokusanywa kutoka katika kamusi zilizoteuliwa zilichambuliwa na kuchanganuliwa kwa kuzingatia mihimili ya nadharia na katika mizani ya malengo ya utafiti. Data hizi ni mifano ya vidadala, sinonimu, antonimu, wingi na umoja wa nomino, methali, nahau na misemo, ambayo ilinukuliwa moja kwa moja kutoka katika kila kamusi iliyoteuliwa. Pia, kauli za wahojiwa kuhusu jinsi ukubwa wa kitabu unavyoathiri gharama ya uchapishaji zilinukuliwa.

1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Kothari (2004) anasema kuwa baada ya kukusanya na kuchanganua data, ni muhimu mtafiti aeleze matokeo ya utafiti kwa umakinifu ili yasije yakapotosha au yasije yakawa yale yasiyotokana na utafiti. Anasema kuwa ni kupitia ufasiri wa data ndipo mtafiti anaweza kueleza uhusiano unaojitokeza kati ya matokeo ya utafiti na suala la utafiti. Data zilizokusanywa katika utafiti huu ziliwasilishwa kwa njia ya maelezo na majedwali ili ziweze kueleweka na kubainika wazi.

1.8.7 Maadili ya Utafiti

Kulingana na Mugenda na Mugenda (2012), maadili katika utafiti yanahusu uadilifu unaomwongoza mtafiti anapofanya utafiti hasa pale washiriki ni binadamu. Utafiti huu ulifanywa kwa kuzingatia maadili ya kiwango cha juu. Kwanza, waliohojiwa waliulizwa iwapo walikuwa radhi kujibu maswali na katika muda na mahali walipochagua wenyewe. Hakuna yeyote aliyeshurutishwa kutoa jibu iwe katika mahojiano au hojaji. Faragha ya washiriki pia iliheshimiwa na wakahakikishiwa kuwa taarifa ambazo wangetoa hasingetumiwa kwa shughuli nyingine isipokuwa kufanikisha utafiti huu.

SURA YA PILI

VIPENGELE VYA UREJELEANO KATIKA KAMUSI TEULE ZA KISWAHILI

2.0 Utangulizi

Sura hii imeangazia vipengele vya kamusi ya Kiswahili ambavyo vinaweza kuhusishwa kupitia urejeleano. Kamusi zote tatu zilizochanganuliwa zimejumuisha vipengele hivyo kwa kiwango kikubwa. Tumevibainisha vipengele hivyo na tukadondoa mifano michache ya moja kwa moja ya vipengele hivi kutoka kwenye kamusi teule. Pia, kwa kifupi, tumeonesha namna watunzi wa kamusi hizi walivyoushughulikia urejeleano wa vipengele hivi katika mtazamo wa nadharia ya miundomedio. Kama itakavyobainika, kuna baadhi ya vipengele ambavyo havikuhusishwa kupitia urejeleano katika kamusi hizi.

2.1 Dhana za Kimsingi kuhusu Urejeleano

Katika Sura ya Kwanza, tumesikia kulingana na Gouws na Prinsloo (2005) kuwa urejeleano ni mbinu ya kileksikografia ambayo kwayo watunzi wa kamusi huweza kuonesha uhusiano uliopo kati ya vipengele tofauti vya kamusi. Dhana za kimsingi kuhusu urejeleano zinatokana moja kwa moja na nadharia ya urejeleano, yaani miundomedio. Gouws na Prinsloo (2005)

wanazieleza dhana zifuatazo kama zilivyofafanuliwa na Wiegand (1996c:11), ambaye ndiye mwasisi wa nadharia hiyo.

2.1.1 Chanzo cha Urejeleano

Chanzo cha urejeleano ni kile kidahizo ambacho kutoka kwacho, mtumiaji wa kamusi huelekezwa katika sehemu nyingine iliyo na taarifa zaidi kukihusu. Kwa mfano, huenda ikawa maana ya neno fulani imeshughulikiwa katika neno jingine lililo na uhusiano wa kisawe au kibadala na kwa sababu hiyo, ili kuepuka uradidi watunzi wakaona hakuna haja ya kuiingiza maana ile tena. Hebu tutazame mifano hii kutoka katika kamusi teule.

Mfano 1:

(a) **ndovu** /ndɔvu/ nm (-) [a-/wa-] taz. **tembo**¹. (KKS 2014: 427)

(b) **runinga** /ru'ninga/ nm. (∅) {i-/z-} taz. **televisheni** (KKK 2015:


896)

(ch) **lumbwi** /lumbwi/ nm (a-wa) taz. **kinyonga**. (KEK 2016: 363)

Kulingana na mifano hii, maneno *ndovu*, *runinga* na *lumbwi* ni chanzo cha urejeleano. Kutoka kwa vadahizo *ndovu*, *runinga* na *lumbwi*, mtumiaji wa kamusi anaelekezwa kwenye vadahizo vingine katika kamusi, yaani **tembo**¹, **televisheni** na **kinyonga**, mtawalia, ambavyo ni visawe vya maneno hayo.

Hapo ndipo ambapo mtumiaji wa kamusi anatarajiwa kupata maelezo yanayohusiana na alichokuwa akikitafuta.

2.1.2 Anwani ya Urejeleano

Katika chanzo cha urejeleano, mtumiaji huelekezwa kwenye kidahizo kingine ambapo anaweza kupata taarifa zaidi kuhusu dhana aliyokuwa akiitafuta. Pale anapoelekezwa mtumiaji wa kamusi ndipo panapojulikana kama ‘anwani ya urejeleano’. Kulingana na Gouws na Prinsloo, kuna aina tatu za anwani ya urejeleano: (i) anwani ndani ya kitomeo kilekile chenye chanzo cha urejeleano, (ii) anwani katika kidahizo kingine tofauti katika kamusi, iwe katika orodha ya vidahizo (a – z) au katika viambatisho vya kamusi iyo hiyo, na (iii) anwani nje ya kamusi hiyo. Katika mfano ulio hapo juu, *tembo*¹, *televisheni* na *kinyonga*, ni anwani za urejeleano kwani ndipo mtumiaji wa kamusi ameelekeza kutoka kwenye chanzo cha urejeleano yaani *ndovu*, *runinga* na *lumbwi*, mtawalia ili kupata taarifa zaidi. Anwani hizi zote zimo ndani ya kamusi katika vidahizo tofauti. Mifano ya urejeleano katika viambatisho vya kamusi inapatikana katika KKS pale ambapo katika mizizi ya vimilikishi *-ake* (uk. 8), *-ako* (uk. 9), *-angu* (17), *-ao* (uk. 18), *-enu* (uk. 103), na *-etu* (uk. 103), mtumiaji anapata ishara hii ‘ taz. Jedwali A uk. 673’. Hapa anaelekezwa, kwa kutumia ishara ya urejeleano, kutazama ‘Jedwali A’ katika ukurasa wa 673 ili kupata taarifa zaidi kuhusu vimilikishi hivyo.

2.1.3 Alama ya Urejeleano

Alama ya urejeleano ni msimbo unaotumiwa kuhusisha chanzo cha urejeleano na anwani ya urejeleano. Kwa maneno mengine, hiki huwa kiunzi kati ya vidahizo hivi viwili na huwa kama kielekezi kwa mtumiaji wa kamusi cha kumwezesha kupata taarifa zaidi za kileksikografia. Kulingana na Gouws na Prinsloo (2005) na Alberts (2007), kamusi tofautitofauti hutumia alama mbalimbali za urejeleano. Kuna watunzi wa kamusi ambao hutumia michoro kama vile \blacktriangleleft , \rightarrow , \Rightarrow na \blacktriangleright , huku wengine wakitumia maneno, kama vile *taz.* (tazama), na *ling.* (linganisha). Svensen (1993:195) anasema kuwa “kauli kama ‘taz. xxx’ inaweza kumaanisha kuwa ‘fasili ya neno, au kirai haikuingizwa hapa; badala yake itafute katika xxx’”. Hebu tuone alama za urejeleano zilizotumiwa kwenye mifano ifuatayo kutoka kwenye kamusi teule.

Mfano 2:

(a) **ndovu** /ndɔvu/ nm (-) [a-/wa-] **taz.** \blacktriangleleft **tembo**¹. (KKS 2014: 427)

(b) **runinga** /ru'ninga/ nm. (Ø) {i-/z-} **taz.** **televisheni** (KKK 2015: 896)

(ch) **lumbwi** /lumbwi/ nm (a-wa) **taz.** **kinyonga**. (KEK 2016: 363)

Katika mfano wa (a) tunaona KKS imetumia ‘**taz.** \blacktriangleleft ’ kama alama ya urejeleano. Katika kidahizo *ndovu* maana haikutolewa na mtumiaji wa kamusi anaelekezwa, kupitia alama ya urejeleano, kutazama kidahizo *tembo*¹ ambapo fasili imetolewa. Katika (b) na (ch), KKK na KEK zimetumia ‘**taz.**’ kama

alama ya urejeleano. Katika KKK na KEK, vidahizo *runinga* na *lumbwi*, mtawalia havikutolewa fasili bali kupitia alama ya urejeleano ‘**taz.**’, mtumiaji anaelekezwa katika vidahizo *televisheni* na *kinyonga* mtawalia vilivyotolewa fasili. Vilevile, kama tulivyoona, KKS imetumia alama nyingine ‘**ṭaz.**’ hasa pale ambapo watunzi wanamwelekeza mtumiaji wa kamusi kupata taarifa katika majedwali yaliyoambatishwa nyuma ya kamusi.

2.1.4 Uhusiano wa Kiurejeleano

Ili vidahizo vihusishwe kupitia urejeleano, ni sharti kuwe na uhusiano baina ya vidahizo hivyo. Uhusiano huu ndio huitwa uhusiano wa kiurejeleano na huoneshwa kwa kupitia alama ya urejeleano. Uhusiano huu unaweza kuwa wa kama vile wa kbadala, kisawe au hata wa kinyume. Gouws na Prinsloo (2005:181) wanasema kuwa “tatizo moja halisi wanalokumbana nalo watumiaji wa kamusi zilizopangwa kiabjadi ni lile la kuzitenganisha dhana za kileksia zinazohusiana”. Wanamnukuu Bolinger (1985:69) anayesema kuwa leksikografia ni kazi isiyokuwa na uhalisia, ambayo “inahusu utengaji wa maneno kutoka kwa miktadha yao ya kawaida, na kuyapanga katika safu – karoti na vitunguu, na bitiruti na *salsify* karibukaribu – huku mizizi ikiwa imekatwa kama ya figili ili kuziwezesha mboga hizi kuwekwa pamoja, katika utaratibu ambao haukupangwa na hali halisi ya mambo, bali kwa utaratibu wa mabaharia Wafinisia waliofanya biashara na Wagiriki kipindi kirefu kilichopita”. Gouws na Prinsloo wanamnukuu Bolinger akisema kuwa muda mwingi wa mwanaleksikografia unatumiwa kujaribu kurekebisha makosa haya

kupitia kuonyesha uhusiano uliopo baina ya maneno hayo. Wanasema kuwa upangaji wa kamusi kialfabeti unakiuka mahusiano ya kisemantiki yaliyopo baina ya vitomeo vya kileksia. Kulingana na wanaleksikografia hawa, urejeleano ni mbinu muhimu ya kujaribu kuyarejesha mahusiano ya kileksia, kama vile ya vibadala, visawe, kinyume na hiponimu.

2.1.5 Urejeleano Mzunguko

Huu ni aina ya urejeleano ambao humzungusha mtumiaji wa kamusi bila kumfaidi. Kutoka katika chanzo cha urejeleano, mtumiaji wa kamusi huelekezwa kwenye anwani ya urejeleano kama kawaida ya urejeleano. Hata hivyo, katika anwani ya urejeleano mtumiaji wa kamusi hapati taarifa zaidi na badala yake hurejeshwa palepale katika chanzo cha urejeleano. Ili kufafanua urejeleano mzunguko, Gouws na Prinsloo (2005:179) wanaunukuu mfano ufuatao kutoka *The Dictionary of Lexicography (DL)*:

circular reference \Rightarrow reference circularity

reference circularity \Rightarrow circular reference

Kama inavyobainika katika mfano huu, chanzo cha urejeleano ni *circular reference*. Kutoka hapa, kupitia alama ya urejeleano, \Rightarrow , mtumiaji wa kamusi anaelekezwa katika anwani ya urejeleano, *reference circularity*. Kutoka kwenye chanzo cha urejeleano, na kupitia alama ya urejeleano, mtumiaji wa kamusi anatarajia kupata maelezo kuhusu *circular reference* katika *reference circularity*. Hata hivyo, mtumiaji anarejeshwa kwenye chanzo cha urejeleano

bila kupata maelezo aliyoyatarajia. Mfano kama huu wa urejeleano mzunguko unapatikana katika *Kamusi Kuu ya Kiswahili* katika vidahizo vifuatavyo:

Mfano 3:

ngeo /'ŋgɛ:wɔ/ *nm.* (Ø) {i-/z-} taz. **ngeu** (KKK: 792)

ngeu /'ŋgɛ:u/ *nm.* (Ø) {i-/z-} taz. **ngeo** (KKK: 793)

afueni /afu'weni/ *nm.* (Ø) {i-} taz. **ahueni** (KKK: 12)

ahueni² /ahueni/ *nm.* (Ø) {i-} taz. **afueni** (KKK: 15)

Katika mifano hii, mtumiaji wa kamusi anayetafuta maana za maneno *ngeo* na *afueni* anaelekezwa kutazama vibadala *ngeu* na *ahueni*, mtawalia. Hata hivyo, katika anwani hizi za urejeleano hakuna maelezo yanayopatikana pale bali mtumiaji wa kamusi anarejeshwa kwenye chanzo cha urejeleano. Katika utaratibu kama huu, vidahizo vyote vimeshughulikiwa kama chanzo cha urejeleano bali katika anwani ya urejeleano hakuna kilichotarajiwa.

2.1.6 Urejeleano Uliokufa

Gouws na Prinsloo (2005) wanasema kuwa mojawapo ya makosa ya kimsingi ambayo wakati mwingine hufanywa na wanaleksikografia ni kufanya urejeleano katika anwani ambayo haikuingizwa kwenye kamusi. Wanautaja

urejeleano wa aina hii kama urejeleano uliokufa. Kuna mifano ya urejeleano wa aina katika baadhi ya kamusi zilizochanganuliwa.

Mfano 4:

harusi /harusi/ *nm* (i-zi) **taz. arusi.** (KEK: 187)

arusi – lingekuwa katika uk. 24 lakini halikuingizwa.

chwale /tʃwale/ *nm* (i-zi) **taz. chuwale.** (KEK: 89)

chuwale – lingekuwa katika ukurasa 89 lakini halikuingizwa.

chudere /tʃu'dere/ *nm.* (*ma-*) {*a-/wa-*} **taz. chaudere.** (KKK: 145)

chaudere – lingekuwa katika ukurasa 122 lakini halikuingizwa.

kalab /kalab/ *nm.* (\emptyset) {*a-/wa-*}. **taz. kelb.** (KKK: 366)

kelb – lingekuwa katika ukurasa 393 lakini halikuingizwa.

Lililoingizwa ni neno *kelbu*.

Kulingana na wanaleksikografia hawa, urejeleano huu wote umekufa kwa sababu anwani za urejeleano *arusi*, *chuwale*, *chaudere* na *kelb* hazikuingizwa kwenye kamusi kama vidahizo.

2.2 Vipengele vinavyoweza Kuhusishwa kupitia Urejeleano

Kuna vipengele vingi ambavyo huunda kamusi. Baadhi ya vipengele hivi huwa na uhusiano wa namna fulani na hivyo basi huwa vyema iwapo uhusiano kama huu utaoneshwa kwa watumiaji wa kamusi. Uhusiano huu unaweza kuoneshwa vyema zaidi kupitia kipengele cha urejeleano. Svenson (1993), Gouws na Prinsloo (2005), na Kiango (1996) wamevifafanua vipengele kama vifuatavyo ambavyo vinaweza kuhusishwa kupitia urejeleano: vibadala, visawe, vinyume, wingi wa nomino, methali, misemo na nahau. Vipengele hivi vimefafanuliwa hapa kimoja baada ya kingine na vikadondolewa mifano ya moja kwa moja kutoka kwenye kamusi teule.

2.2.1 Vibadala

Kulingana na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2014: 214), *kibadala* ni “neni linalotofautiana kidogo na neno jingine kimatamshi lakini lenye maana sawa na hilo”. Lugha ya Kiswahili ina vibadala vingi. Kulingana na Kiango (1996) ni kibadala kilicho sanifu tu ambacho kinastahili kuingizwa kwenye kamusi. Hata hivyo, kama ilivyoielezwa katika Sura ya Kwanza, Kiango hakusema jinsi vibadala vilivyoingizwa kwenye kamusi vinastahili kuhusishwa. Iwapo maneno yamekubaliwa kuwa sanifu na kuingizwa kwenye kamusi, ni dhahiri kuwa kuna jumuiia za watu zinazoyatumia maumbo hayo tofauti. Hivyo, kukosa kuliingiza umbo moja huenda kukawa kikwazo kwa watumiaji wanaolijua umbo lililoachwa. Hii inaonesha umuhimu wa kuyaingiza maumbo yote kwenye kamusi. Hata hivyo, itakuwa vyema iwapo watunzi wa kamusi

watalichagua umbo moja, walipe sifa za kitomeo kamili ili liweze kuwa anwani ya urejeleano kwa maumbo yale mengine (Svensen, 1993, na Gouws na Prinsloo, 2005).

Kulingana na Svenson (1993), tofauti za maendeleo ya vibadala zinaweza kutokana na sababu za kimtindo au kijiografia. Anasema kuwa kama mbinu ya kupunguza nafasi inayotumiwa na maelezo, fasili inaweza kutolewa katika neno moja na hatimaye kuhusishwa kwenye kabadala kupitia urejeleano. Watunzi wa kamusi zilizochanganuliwa kwa kiwango kikubwa wamejaribu kuzingatia utaratibu huu. Hata hivyo, kama itakavyobainika katika sura zinazofuata, katika vidahizo vingi urejeleano huu haukuegemezwa kwenye mihimili ya kinadharia. Pia, ikumbukwe kuwa kuna vipengele vilivyo na mifano mingi sana kiasi kwamba hatungeweza kuionesha yote hapa. Hivyo basi iliyo hapa ni mifano michache tu. Katika kamusi zilizochanganuliwa, vibadala vimeoneshwa kwa kutumia neno **pia**. Kwa mfano:

Mfano 5:

barobaro /ba:rɔ'ba:rɔ/ nm (ma-) {a-/wa-} **pia barubaru, bera** kijana

wa kiume balehe mwenye nguvu za mwili na uwezo wa kuzaa

vis.: ghuramu, hirimu (KKK: 69)

barubaru /baru'baru/ nm (ma-) {a-/wa-} **taz. barobaro** (KKK: 69)

benki /benki/ **pia banki** /banki/ *nm* (-) [i-/zi-] shirika la fedha

linalohifadhi na kukopesha fedha: ~ ya biashara; ~ ya nyumba;

~ **ya Dunia** shirika la fedha la kimataifa linalotoa mikopo kwa nchi wanachama. (KKS: 38)

banki /banki/ *nm* (-) [i-/zi-] **taz. benki.** (KKS: 31)

danadana³ /danadana/ *nm* (i-zi) **pia danedane** ngoma inayochezwa

kwa kutumia vijiti ambavyo hugonganishwa wakati wa kucheza. (KEK: 94)

danedane /danedanɛ/ *nm* (i-zi) **taz. danadana**³. (KEK: 94)

Mifano hii imezingatia utaratibu uliopendekezwa wa kuvishughulikia vibadala kiurejeleano. Vibadala *barubaru*, *banki* na *danedane* vimepewa hadhi ya chanzo cha urejeleano, pale ambapo mtumiaji wa kamusi anaelekezwa, kupitia ishara za urejeleano ‘taz.’ na ‘**taz.**’ kwenye anwani za urejeleano, *barobaro*, *benki* na *danadana*³ mtawalia, palipo na maelezo. Pia, katika anwani ya urejeleano tunaoneshwa ule uhusiano uliopo kati ya vidahizo hivi viwili kupitia neno **pia**.

Hebu tuone namna watunzi walivyovishughulikia vibadala katika mfano ufuatao.

Mfano 6:

tezo /'tɛ:zɔ/ nm (Ø) {i-/zi-} **pia chezo** aina ya kifaa kidogo chembamba

kinachofana na jembe kwa umbo na ambacho hutumiwa na seremala au mchonga vinyago kuchongea miti au mbao ili kutengeneza vifaa vyake (KKK: 1001)

chezo /'tʃɛzɔ/ nm (ma-) {i-/zi-} aina ya chombo cha muziki chenye

bomba mithili ya filimbi ambacho hupigwa kwa kupulizwa wakati wa nyimbo za ibada kanisani

(KKK: 132)

Kulingana na mfano huu, ni dhahiri kwamba dhana zinazoibuliwa na vibadala hivi ni tofauti. Kuna uwezekano kuwa kidahizo *chezo* kilikusudiwa ama kuwa polisemi (maana zaidi ya moja) au homonimu (maendelezo sawa lakini maana tofauti). Kulingana na utaratibu wa urejeleano, iwapo maneno haya ni vibadala, hakungekuwa na fasili katika kidahizo *chezo*. Badala yake kungekuwa na ishara ya urejeleano ambayo ingemwelekeza mtumiaji wa kamusi kwenye chanzo cha urejeleano, yaani *tezo*.

Hebu tuone namna tofauti watunzi walivyovishughulikia vibadala katika mfano ufuatao.

Mfano 7:

loga /'lɔga/ *kt.ele.* **pia roga** fanyia mtu ushirikina ili kumdhuru; sihiri

vis. tambika, gonya (KKK: 548)

roga /'rɔga/ *kt.ele.* **pia loga** fanyia mtu ushirikina kwa lengo la

kumdhuru au kuharibu mali zake; sihiri *vis.* tambika, wanga, cheza (KKK: 891)

gaagaa /gaagaa/ *kt (sie)* **pia garagara** kitendo cha mtu au mnyama

kujilaza sakafuni au nyasini au hata kitandani na kujizungushazungusha. (KEK: 159)

garagara /garagara/ *kt (sie)* **pia gaagaa** kosa utulivu hasa usingizini

na kujibingirishabingirisha. (KEK: 162)

Kulingana na mifano hii, vibadala vyote viwili vimeshughulikiwa kama anwani ya urejeleano, bali hakuna chanzo cha urejeleano. Hali hii ni kinyume na mihimili ya nadharia ya miundomedio na pia wataalamu kama vile Nkomo (2008) anayesema kuwa kwa sababu ya iktisadi ya kuokoa nafasi na kuepuka uradidi ni kabadala kimoja tu kinachopaswa kupewa hadhi kamili ya kileksikografia na kile kingine kuhusishwa kwa kutomia neno BONA, neno kutoka lugha ya isiZulu linalomaanisha TAZAMA.

Kwa kawaida, ingekuwa vyema iwapo watunzi wa kamusi hizi wangekiteua kabadala kimoja kuwa chanzo cha urejeleano na kingine kuwa anwani ya urejeleano. Kwa namna hiyo hakungekuwa na urudiaji wa maana ambayo inaonekana kuwa sawa kabisa katika kabadala cha pili.

Ufuatao ni mfano mwingine ulio tofauti na ile tuliyoitaja hapo juu.

Mfano 8:

glovu /glɔvu/ *nm* (i-zi) **pia glavu** kifaa kilichoshonwa kwa mpira au kiguo kivaliwacho mkononi ambacho kimetengenezwa kikiwa na nafasi ya kuvalisha kila kidole. (KEK: 169)

glavu – kabadala hiki hakikuingizwa kwenye kamusi hii.

Katika mfano huu, watunzi waliingiza kabadala kimoja tu licha ya kukitaja kile kingine. Shida inayoweza kutokea katika utaratibu wa aina hii ni kwamba watumiaji wa kamusi ambao wanakifahamu kabadala *glavu* tu watakikosa na hivyo kufikiria kuwa neno hili halikuingizwa kwenye kamusi.

Mfano unaofuata pia una utofauti wake.

Mfano 9:

dengrizi /deŋgrizi/ *nm* (i-zi) **taz. dangrizi.** (KEK: 99)

dangirizi /daŋgirizi/ *nm* (i-zi) **pia dangrizi** suruali iliyoshonwa kwa

kitambaa kigumu cha pamba mithili ya turubai yenye mishono mipana ya kuonekana kwa nje. (KEK: 95)

Mfano huu umefuata utaratibu unaofaa wa urejeleano wa vibadala. Hata hivyo, unapochunguza kwa makini utagundua kuwa kuna tofauti kati ya jinsi neno ambalo mtumiaji wa kamusi anaelekezwa kwalo, *dangrizi*, na kidahizo kilichoingizwa kwenye kamusi, *dangirizi*. Pia, katika anwani ya urejeleano kibadala kilichotangulizwa na neno **pia** ni *dangrizi* bali si *dengrizi* ambacho ndicho chanzo cha urejeleano.

2.2.2 Visawe

“Kisawe ni neno ambalo maana yake inakaribiana sana na neno au maneno mengine” (*Kamusi Kuu ya Kiswahili 2015: 467*). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2014: 250) inakifasiri kama “moja kati ya maneno mawili au zaidi yanayokaribiana kimaana”. Kuna visawe ambavyo vina maana inayoshabihiana kabisa na vingine vina maana zinazokaribiana. Kulingana na mihimili ya nadharia ya miundomedio, pale ambapo visawe vina maana zinazofanana kabisa hakuna haja ya kuvipa visawe kama hivyo hadhi sawa kama vitomeo katika kamusi. Hapa watunzi wanastahili kukichagua kidahizo ambacho kinatumika zaidi na kukitolea maelezo kwa ukamilifu unaofaa na hivyo kukifanya kama anwani ya urejeleano. Kwa mfano, maneno kama vile *ndovu/tembo*, *nyati/mbogo*, *tarakilishi/kompyuta*, na *mkokoteni/rukwama* ni visawe vya moja kwa moja. Nadharia ya miundomedio inasema kuwa katika

utaratibu kama huu kidahizo kimoja hutolewa taarifa zote huku kile kiingine kikikirejelea.

Kamusi zilizochanganuliwa katika utafiti huu zimeingiza visawe vingi. Hebu tuone, kupitia mifano ifuatayo, namna vidahizo sawa vilivyoshughulikiwa katika kamusi zilizochanganuliwa.

Mfano 10:

mbogo /'mbɔgɔ/ nm (∅) {a-/wa-} mnyama mkubwa wa porini mithili

ya ng'ombe mwenye pembe kubwa zilizokunjika mbele **mat.:**

Mbuga za Serengeti na Masai Mara zina ~ wengi. mse.: kuwa ~

= kuwa mkali **kis.:** **nyati** (KKK: 608)

nyati /'na:ti/ nm (∅) {a-/wa-} mnyama mkubwa wa nchi kavu jamii ya

ng'ombe anayeishi porini mwenye pembe zilizopinda kuelekea

juu **vis.:** **mbogo**, ng'ombe mwitu (KKK: 809)

mbogo /mbɔgɔ/ nm (-) [a-/wa-] ▀ **taz. nyati:** (ms) *Kuwa ~ kuwa*

mkali. (KKS: 329)

nyati /nati/ nm (-) [a-/wa-] mnyama wa porini anayefanana na

ng'ombe lakini mkubwa zaidi, ana pembe kubwa zilizopinda kuelekea mbele; **mbogo**. (KKS: 442)

mbogo /*mbɔgɔ/ nm* (a-wa) mnyama mkubwa wa porini anayefanana

sana na ng'ombe lakini mkubwa zaidi na mwenye uzito zaidi na mwenye pembe zilizokwenda chini kidogo kisha zikapinda na kuelekea juu zilizochongoka; **nyati**, ng'ombe mbitu. (KEK: 407)

nyati /*ɲati/ nm* (a-wa) mnyama pori anayefanana na ng'ombe ambaye

ni mkali na mwenye pembe ambazo huzitumia kuwa silaha; **mbogo**. (KEK: 539)

Katika mfano huu, kamusi zote tatu zimeonesha kuwa vidahizo hivyo ni visawe. Hata hivyo, ni *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* pekee iliyofuata utaratibu uliopendekezwa wa kuhusisha visawe kupitia urejeleano. Watunzi wa kamusi hii walikiteua kisawe *mbogo* kuwa chanzo cha urejeleano na kumwelekeza mtumiaji wa kamusi katika anwani ya urejeleano, *nyati*, palipo na maelezo. Kamusi hizo nyingine, kando na kuonesha uhusiano wa maneno hayo, vimevipa visawe vyote hadhi sawa kwa kuvitolea maelezo, jambo ambalo ni kinyume na mihimili ya nadharia ya miundomedio.

Hebu tuone tofauti inayojitokeza katika mfano ufuatao.

Mfano 11:

runinga /ru'ninga/ nm (Ø) {i-/zi-} **taz. televisheni.** (KKK: 896)

televisheni /televifeni/ nm (Ø) {i-/zi-} kifaa kinachonasa sauti,

maandishi na picha kutoka katika kituo maalumu cha matangazo na kuonyesha kwa watazamaji **kis.: runinga** (KKK: 996)

runinga /runinga/ nm (-) [i-/zi-] ▣ **taz. televisheni.** (KKS: 493)

televisheni /televifeni/ nm (-) [i-/zi-] 1 chombo kinachonasa picha,

sauti na maandishi kutoka kituo cha kurushia matangazo na kuvionyesha pamoja na kutoa sauti iliyonaswa; **runinga.** (KKS: 559)

runinga /runinga/ nm (i-zi) chombo cha kielektroniki aina ya kiboksi

kinachotangaza habari kwa kunyesha picha na sauti;
televisheni. (KEK: 600)

televisheni /televifeni/ nm (i-zi) chombo kinachonasa mawimbi ya picha

na yanayorushwa kwa njia ya satelaiti kutoka vituo mbalimbali
na kuonyesha picha na sauti kwa wakati huohuo; runinga.
(KEK: 679)

Katika mfano huu, KKK na KKS zimezingatia utaratibu unaopendekezwa na nadharia ya miundomedio kwa kuingiza fasili katika kidahizo kimoja ambacho kimepewa hadhi ya anwani ya urejeleano. Hata hivyo, KEK haikufanya hivyo. Kama inavyobainika, watunzi wake walivipa visawe vyote hadhi sawa na kuvitolea maelezo badala ya kutoa fasili katika kisawe kimoja na kisha kumwelekeza mtumiaji wa kamusi katika anwani ya urejeleano.

2.2.3 Vinyume

Maneno mengi huwa na vinyume na huwa bora zaidi iwapo uhusiano huu utaoneshwa katika kamusi. Iwapo hili litatendeka mtumiaji wa kamusi huweza kupata taarifa zaidi ya zile alizozikusudia. Miongoni mwa kamusi zilizochanganuliwa katika utafiti huu, ni *Kamusi Kuu ya Kiswahili* pekee ambayo imeonesha uhusiano huu kupitia urejeleano. Ishara ya urejeleano iliyotumiwa katika urejeleano huu ni **kiny**. Hebu tuone mifano michache ilivyoshughulikiwa.

Mfano 12:

haraka¹ /ha' raka/ nm (Ø) {i-/zi-} hali ya kufanya chapuchapu, kasi;

arubii *vis.*: hima, ajila, epesi *viny.*: **polepole, asteaste**. (KKK: 284)

Mfano 13:

furahi /fu'rahi/ *kit.sie* **a.** jawa na uchangamfu na bashasha moyoni **b.**

kuwa katika hali ya kuridhika **ch.** kuwa katika starehe *viny.*:

chukia, nuna, kasirika. (KKK: 231)

Mfano 14:

umaskini /umas'kini/ *nm* (Ø) {*u-*} hali duni ya kimaisha inayoweza

kumkuta mtu binafsi, shirika au nchi kutokana na kutokuwa na

mali *vis.*: ukata, ufukara, uchochole, ufefe, uhitaji *viny.*: **utajiri,**

ukwasi. (KKK: 1092)

Mtumiaji wa kamusi hii anayetafuta maana za maneno *haraka, furahi* na *umaskini* atapata taarifa zaidi kuhusu vinyume vya maneno hayo. Kwa mfano, ameelekezwa kuwa kinyume cha *haraka* ni *asteaste* na *polepole*, kinyume cha kitenzi *furahi* ni *chukia, nuna* ni *kasirika*, ilhali vinyume vya nomino *umaskini* ni *ukwasi* na *utajiri*. Hata hivyo, vinyume vyote vilivyoingizwa katika mifano hii mitatu havikutolewa vinyume pale vilipoingizwa kama vidahizo. Hii inamaanisha kuwa mtumiaji wa kamusi ambaye anatafuta maana za maneno *polepole* (KKK: 864) na *asteaste* (KKK: 44) hatapata taarifa zaidi kuhusu *haraka* kuwa kinyume cha maneno hayo. Vilevile, yule anayetafuta maana za maneno *ukwasi* (KKK: 1086) na *utajiri* (KKK: 1129) hatajua kuwa kinyume cha maneno haya ni *umaskini*, na anayetafuta maana za maneno *chukia* (KKK:

146) *kasirika* (KKK: 384) na *nuna* (KKK: 804) pia atakosa taarifa zaidi kuhusu *furahi* kuwa kinyume cha maneno haya.

2.2.4 Wingi wa nomino

Kinyume na lugha ya Kiingereza ambayo nomino zake hazibadiliki sana kimuundo katika umoja na wingi, nomino nyingi za Kiswahili huchukua mianzo mipya na hivyo kwa namna fulani kubadilisha umbo la nomino husika. Kamusi kwa kawaida huingiza nomino katika umoja kama vidahizo. Hata hivyo kuna wakati ambapo watunzi hulazimika kuingiza umbo la wingi la nomino kutegemea mambo mbalimbali, kama vile matumizi ya nomino husika. Hili hutokea pale ambapo watunzi wa kamusi huhisi kuwa umbo fulani, hata kama ni la wingi, hutumiwa zaidi na kwa hivyo kuna uwezekano wa watumiaji wa kamusi kulitafuta umbo hilo kwenye kamusi. Pia, kwa sababu hii, huenda kuna watumiaji wa kamusi wengine ambao hawajui iwapo kuna umbo jingine ambalo ni la umoja. Ili kuepuka kumvunja moyo mtumiaji wa kamusi kama huyu, huwa ni vyema kuyaingiza maumbo hayo. Hata hivyo, haimaanishi kuwa umbo la wingi linapoingizwa lile la umoja lisahaulike, la hashu! Yote yanastahili kuingizwa na fasili kutolewa katika umbo lile la umoja, ambalo aghalabu hupewa hadhi ya anwani ya urejeleano. Kamusi zilizochanganuliwa katika utafiti huu zimeingiza baadhi ya maumbo hayo, kama inavyooneshwa na mfano huu wa vidahizo sawa.

Mfano 15:

matako /ma'takɔ/ nm (Ø) {ya-} **taz. tako.** (KKK: 593)

tako /'takɔ/ nm (ma-) {li-/ya-} **a.** sehemu ya nyuma ya mwili wa mnyama au binadamu iliyo kati ya kiuno na mapaja na inayotumiwa kukalia **b.** sehemu ya chini ya kitu ambayo hutumiwa kukikalisha kitu hicho chini au juu ya uso wa kitu kingine. (KKK: 978)

matako /matakɔ/ nm (-) [ya-] ~~ta~~ **taz. tako.** (KKS: 320)

tako /takɔ/ nm (ma-) [li-/ya-] **1** sehemu ya nyuma ya mwili baina ya kiuno na paja inayotumiwa kwa kukalia. **2** sehemu ya chini ya kitu ambayo hutumiwa, agh. Kuwa ni kikalio. (KKS: 546)

matako /matakɔ/ nm (li-ya) sehemu ya nyuma ya mwili inayotumika kukaa. (KEK: 395)

tako /takɔ/ nm ma- (li-ya) **1** sehemu ya nyuma ya mwili wa binadamu iliyo chini ya kiuno ambayo aghalabu ina umbo tofauti na sehemu nyingine. **2** sehemu ya chini ya kitu kama kopo, chupa ambayo ndiyo kikalio cha vitu hivyo. (KEK: 664)

Mfano huu unaonesha nomino moja ambayo imeingizwa katika kamusi zote tatu zilizochanganuliwa. Watunzi wa kamusi hizi wameyaingiza maumbo yote

mawili, lile la umoja (tako) na lile la wingi (matako). Kamusi mbili, *Kamusi Kuu ya Kiswahili* na *Kamusi Sanifu ya Kiswahili*, ndizo zilizofuata utaratibu wa urejeleano unaopendekezwa, kwa kuingiza fasili mara moja tu katika umbo la umoja. Mtumiaji wa kamusi ambaye anatafuta neno matako anaelekezwa, kupitia ishara ya urejeleano, kutazama anwani ya urejeleano, *tako*. Hata hivyo, *Kamusi Elezi ya Kiswahili* imeyapa maumbo yote mawili hadhi sawa kwa kuingiza fasili katika vidahizo vyote viwili.

2.2.5 Methali, Nahau na Misemo

Svensen (1993) anasema kuwa fungu la maneno kama vile kirai linaweza kushughulikiwa katika kila neno linaloliunda fungu hilo, lakini kwa kawaida nafasi hupunguzwa iwapo maana itaingizwa katika neno moja na mtumiaji kurejeshwa palipo na taarifa hizi. Methali, nahau na misemo ni mafungu ya maneno.

Hakuna kamusi hata moja, kati ya tatu zilizochanganuliwa, ambayo imevihusisha vifungu hivi vya maneno (methali, nahau na misemo) kupitia urejeleano. Katika Sura ya Nne, tutaona kulingana na data iliyodondolewa moja kwa moja kutoka kwenye kamusi hizi, athari inayojitokeza kwa sababu ya kutokitumia kipengele cha urejeleano kuvihusisha vipengele hivi.

2.3 Hitimisho

Kama tulivyoona, kuna vipengele vingi ambavyo vinaweza kuhusishwa kupitia urejeleano. Watunzi wa kamusi zote tatu wamejaribu kuvihusisha baadhi ya vipengele hivyo kupitia urejeleano hata ingawa si kwa umakinifu unaofaa. Iwapo nadharia ya miundomedio itazingatiwa vyema, watunzi wa kamusi wanaweza kuokoa nafasi kubwa kwa kuepuka uradidi unaojitokeza iwapo urejeleano haukutiliwa maanani. Nafasi kama hiyo inaweza kutumiwa kwa taarifa zaidi ambazo zitaiboresha kamusi husika.

SURA YA TATU

MISHABAHA NA TOFAUTI ZA MATUMIZI YA UREJELEANO

KATIKA KAMUSI TEULE

3.0 Utangulizi

Katika Sura ya Pili, tumeonesha vipengele mbalimbali vya kamusi ambavyo kwa namna moja au nyingine, vinaweza kuhusishwa kupitia urejeleano. Tumeona kuwa kamusi zote tatu zimetumia urejeleano katika vipengele hivyo. Hata hivyo, pia tumeona kwamba kuna vipengele, hasa vile vilivyoundwa kwa zaidi ya neno moja, vikiwemo methali, nahau na misemo, ambavyo havikuhusishwa kwa namna hii.

Katika sura hii, tumeidondoa baadhi ya mifano ya vipengele hivyo na kuonesha jinsi watunzi wa kamusi hizi tatu walivyoshabihiana au kutofautiana katika kukihusisha kipengele cha urejeleano. Kuna mishabaha mingi inayojitokeza katika uwasilishaji wa kipengele cha urejeleano katika kamusi zote tatu. Mishabaha hii, kulingana na nadharia ya miundomedio, inaweza kuwa imezingatia utaratibu unaostahili, au ikawa mishabaha katika kutozingatia mihimili ya nadharia. Hapa tumedondoa mifano ya uwasilisho huo, moja kwa moja, kutoka kwenye kamusi zilizochanganuliwa. Ikumbukwe kuwa lengo letu hapa si kuangazia fasili za vidahizo husika kama zilivyowasilishwa na watunzi wa kamusi hizi. Pia hatujahariri chochote

kwenye manukuu haya kwani lengo letu hasa lilikuwa kuonesha jinsi mfumo wa urejeleano ulivyotumika. Hivyo, tumedondoa, k.m. fasili kama ilivyo katika kamusi husika.

3.1 Vibadala

Katika maelezo kwa mtumiaji, *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* na *Kamusi Kuu ya Kiswahili* zimeeleza kuwa uingizaji wa vibadala katika kamusi hizo umebainishwa kwa matumizi ya neno **pia**. Hii inamaanisha kuwa kidahizo husika kinaweza kuendelezwa kwa namna hizo zilizooneshwa hapo. Katika *Kamusi Elezi ya Kiswahili*, imetajwa tu kuwa “iwapo kuna neno badalia la kidahizo hicho kimatamshi nalo hufuatia” (uk. xix). Kamusi hii haikutaja matumizi ya neno **pia** hata ingawa utalii wayo unaonesha kuwa watunzi wamelitumia kuvibainisha vibadala.

Kama tutakavyoona kutokana na mifano ya vidahizo kwenye kamusi hizi tatu, ni dhahiri kwamba, kwa kiwango kikubwa, watunzi walifuata dira zao tofauti katika uwasilishaji wao wa urejeleano katika vidahizo vilivyo sawa. Ni maoni yetu kuwa iwapo wangufuata dira moja, bila shaka uwasilishaji wao ungekuwa sawa. Hebu tuangalie mifano ifuatayo:

Mfano 1: Desemba; Disemba

Desemba /de: 'semba/ nm. (Ø) {i-/zi-} nm **pia Disemba** mwezi wa

kumi na mbili kwa mwaka katika kalenda ya Kizungu **taz.**
Jedwali la miezi ya mwaka* (KKK: 165)

Disemba /di: ʔsemba/ *nm.* (Ø) {i-/zi-} **taz.** **Desemba.** (KKK: 174)

Desemba/dɛsemba/ pia **Disemba** /disemba/ *nm* (-) [i-/zi-] mwezi wa
kumi na mbili wa mwaka. (KKS: 87)

Disemba /disemba/ *nm* (-) [i-/zi-] **taz.** **Desemba.** (KKS: 92)

Desemba/dɛsemba/ *nm* (i-zi) pia **Disemba** mwezi wa kumi na mbili
katika kalenda ya Kirumi. (KEK: 100)

Disemba /disemba/ *nm* (i-) **taz.** **Desemba.** (KEK: 107)

Kulingana na mfano huu, kamusi zote tatu zimefuata utaratibu sawa kuonesha uhusiano wa vidahizo hivi. Huu ndio utaratibu unaopendekezwa katika nadharia ya miundomedio. *KKK, hata hivyo, imemwelekeza mtumiaji kulitazama “Jedwali la miezi ya mwaka”. Hata hivyo, utalii wetu wa kamusi hii unaonesha kuwa jedwali hili halikuingizwa popote – haliko katika vidahizo **mwezi** na **mwaka**; na pia orodha ya yaliyomo haina jedwali hili. Vile vile, haliko katika kiambatisho kilicho nyuma ya kamusi.

Hebu tuangalie mfano mwingine ulioshughulikiwa kwa namna tofauti.

Mfano 2 chubwi!; tubwi!

chubwi!¹ /ʔtʃubwi/ *kiel.* pia **tubwi!** mlio wa kitu kilichotumbukia

majini. (KKK: 144)

tubwi! /^ʔtubwi/ *kih.* tanakali sauti ya kitu kizito kinapotumbukia ndani
ya maji agh. yenye kina kirefu. (KKK: 1018)

chubwi!² /tʃubwi/ pia **tubwi!** /tubwi/ *ki* mlio wa kutumbukia kitu
kwenye maji. (KKS: 75)

tubwi! /tu^ʔbwi/ /tubwi/ *ki* taz. ▀ **chubwi!**² (KKS: 574)

chubwi!² /tʃubwi/ pia **tubwi!** /tubwi/ *ki* mlio wa kutumbukia kitu
majini. (KEK: 84)

tubwi! /tubwi/ *kl* taz. **chubwi!**². (KEK: 695)

Katika mfano huu tunaona kwamba kamusi zote tatu zimetumia mikondo tofauti. Kwanza, KKK imevipa vibadala hivi uzito sawa kama vitomeo kamili vyenye maana hata ingawa katika kidahizo **chubwi!**, tumeoneshwa uhusiano wa vibadala hivi kwa kutumia neno **pia**. Pili, kamusi hii, kando na kutueleza kuwa maneno hayo ni vibadala, imeyaainisha katika kategoria tofauti za maneno, yaani **chubwi!** kama kielezi na **tubwi!** kama kihisishi. KKS imezingatia mihimili ya nadharia kwa kuiweka fasili katika kidahizo **chubwi!** na katika **tubwi!**, ikamwelekeza mtumiaji pale palipo na fasili. Watunzi wametilia maanani kuwa kuna **chubwi!**¹ na **chubwi!**² na hivyo wakamwelekeza mtumiaji kwa anwani mwafaka ya urejeleano – **chubwi!**². Pia, kamusi hii inaonesha kuwa vibadala vyote viwili vimo katika kategoria moja ya neno – kihisishi. KEK imeingiza fasili katika kidahizo kimoja – **chubwi!**² – na katika **tubwi!**, ikamwelekeza mtumiaji wa kamusi palipo na fasili. Hata

hivyo, katika kidahizo **chubwi!** palipo na maana, uhusiano wa vibadala hivi haukuoneshwa. Pia kamusi hii ina kidahizo **chubwi!** kama homonimu kwani kuna **chubwi**¹ na **chubwi**². Katika kumwelekeza mtumiaji wa kamusi, watunzi hawakumpa anwani mwafaka kwani hawakujumuisha kipeo. Kama walivyofanya watunzi wa KKK, watunzi wa KEK wameviweka vibadala hivi viwili katika kategoria mbili tofauti za maneno – **chubwi!** (kielezi) na **tubwi!** (kihisishi).

Mfano ufuatao unaonesha kamusi zote zimezingatia namna moja ambayo ni kinyume na mihimili ya nadharia ya miundomedio.

Mfano 3: mafa; mava

mafa /'mafa/ *nm.* (Ø) {ya-} **pia mava** eneo maalumu la kuzikia watu
(KKK: 561)

mava /'mava/ *nm.* (Ø) {ya-} mahali ambapo maiti huzikwa **vis:**
makaburini, maziarani (KKK: 598)

mafa /mafa/ **pia mava** /mava/ *nm* (-) [ya-] mahali wanapozikwa wafu
(KKS: 303)

mava /mava/ *nm* (-) [ya-] makaburi; **mafa.** (KKS: 323)

mafa /mafa/ *nm* (i-zi) **pia mava** mahali pa wafu kuzikwa. (KEK: 371)

mava /mava/ *nm* (ya-) mahali ambapo watu waliokufa huzikwa;
makaburini, maziarani. (KEK: 399)

Kulingana na mfano huu, kamusi zote tatu zimetumia mtindo mmoja ambao unakinzana na mihimili ya nadharia ya miundomedio kwa kuingiza fasili katika vidahizo vyote, hata baada ya kutumia neno **pia** kuonesha kuwa vidahizo hivi ni vidadala. KKS pia imekiingiza kidadala **mafa** katika kidahizo **mava** kwa kuzingatia mtindo wa kamusi hii wa kuviingiza visawe.

Katika mfano ufuatao kamusi zote zimetumia mitindo tofauti.

Mfano 4: kifaru; faru

kifaru¹ /ki'fa:ru/ pia **faru** *nm* vi- {a-/wa-} **taz. faru** mnyama mfupi na

mwenye hasira, mwenye umbo kubwa linalofanana na kiboko; mwenye ngozi ngumu na rangi ya kijivu au nyeupe; ambaye huwindwa sana kutokana na pembe aliyonayo juu ya uso wake. (KKK: 416)

faru /'fa:ru/ *nm.* Ø {a-/wa-} pia **kifaru** mnyama mfupi na mwenye

hasira, mwenye umbo kubwa linalofanana na kiboko; mwenye ngozi ngumu na rangi ya kijivu au nyeupe; ambaye huwindwa sana kutokana na pembe aliyonayo juu ya uso wake. (KKK: 208)

kifaru¹ /kifaru/ pia **faru** /faru/ *nm* (vi-) [a-/wa-] mnyama mkubwa wa

porini, anayefananan na kiboko na mwenye kipusa usoni. (KKS: 223)

faru /faru/ *nm* (ma-) [a-/wa-] **taz. ▀ kifaru**¹. (KKS: 109)

kifaru /kifaru/ *nm* vi- (ki-vi) 1 mnyamapori aliye na kimo cha ng'ombe

ambaye ana pembe moja ndefu na nyingine fupi. (KEK: 275)

faru¹ /faru/ *nm* (a-wa) mnyama mkubwa wa msituni mwenye kipusa au pembe moja inayochomoza juu kidogo ya pua yake. (KEK: 134)

Katika mfano huu, KKK imeviingiza vibadala vyote viwili na kuvitolea maana ile ile, kwa maneno yale yale moja kwa moja. Katika kidahizo **kifaru**¹, kamusi hii imetumia neno **pia** na kifupisho **taz**. na kisha kuendelea kutoa fasili kamili. Kulingana na nadharia ya miundomedio, hili ni kosa. Huwezi kumwelekeza mtumiaji wa kamusi kutazama fasili kwingine ilhali iko palepale, isipokuwa kama ni taarifa zaidi. Kulingana na nadharia ya urejeleano, kile walichokifanya hapa ni kutumia kidahizo **kifaru**¹ kama chanzo na anwani ya urejeleano kwa wakati mmoja. Pia, katika vidahizo vyote watunzi wametumia neno **pia**, hatua ambayo inakinzana na nadharia. Katika vidahizo vyote, mchoro ule ule umetumika. KKS imetumia utaratibu mwafaka unaopendekezwa na nadharia ya urejeleano, yaani miundomedio. KEK imeingiza fasili katika vibadala vyote viwili. Kamusi hii haikuonesha uhusiano wowote kati ya maumbo haya mawili ya maneno ingawa fasili zote zinaonesha kwamba yana uhusiano. Pia, katika kidahizo **kifaru**, ni maoni yetu kwamba watunzi wangekishughulikia kama homonimu bali sio kama polisemi walivyofanya. Hii ni kwa sababu dhana mbili zinazojitokeza zinatofautiana na hakika zinaingia katika ngeli tofauti – dhana ya kwanza ni mnyama ilhali ile ya pili ni kifaa.

Hebu tuone upekee wa mfano ufuatao katika kamusi zote tatu.

Mfano 5: glavu; glovu

glavu /*gla:vu/ nm. (Ø) {i-/zi-}* **pia glovu** kifaa kinachotengenezwa kwa ama mpira, plastiki au nguo, kinachovaliwa kwenye mikono kwa lengo la kujikinga na ama kuchubuka au maambukizi. (KKK: 252)

glovu – Halikuingizwa (KKK: Ø)

glavu /*glavu/ nm. (-) (i-/zi-)* **taz. glovu.** (KKS: 135)

glovu /*glovu/ pia glavu* /*glavu/ nm. (-) (i-/zi-)* kitu kama soksi

kinachovaliwa mkononi ambacho hutengenezwa kwa mpira, ngozi au kitambaa na kwa kawaida huwa na nafasi kwa kila kidole. (KKS: 135)

glavu – Halikuingizwa. (KEK: Ø)

glovu /*glovu/ nm (i-zi)* **pia glavu** kifaa kilichoshonwa kwa mpira au

kiguo kivaliwacho mkononi ambacho kimetengenezwa kikiwa na nafasi ya kuvalisha kila kidole. (KEK: 169)

Katika mfano huu, KKK na KEK zimeingiza kabadala kimoja tu na kukiacha kingine licha ya kuwa kile kilichoachwa kimetajwa katika kile kilichoingizwa kwa kutumia neno **pia**. KKK imeingiza **glavu** na kuacha **glovu**, huku KEK ikiingiza **glovu** na kuacha **glavu**. KKS imezingatia mihimili ya nadharia kwa kuviingiza vidadala vyote, ikatoa fasili katika kimoja na kisha kumwelekeza mtumiaji katika kile kabadala kilichotolewa maana.

3.2 Visawe

Nadharia ya miundomedio inaviainisha vidahizo viwili vilivyo na uhusiano wa moja kwa moja kama ule wa visawe kama *chanzo cha urejeleano* na kile kingine kama *anwani ya urejeleano*. Hivyo basi inatarajiwa kuwa maelezo yatatolewa katika kidahizo kimoja, na katika kile kingine, kuwe na maelekezo ya pale maelezo yanapoweza kupatikana. Kama tutakavyoona katika mifano inayofuata, ni dhahiri kwamba kuna nyakati ambazo watunzi wa kamusi hizi wamezingatia mihimili ya nadharia hii na nyakati ambazo hawakufanya hivyo. Kwa kawaida, iwapo watunzi wote waliifuata mihimili hiyo, matokeo yake yangukuwa usawa katika jinsi walivyovishughulikia visawe, hasa vile vya moja kwa moja, katika kamusi hizi. Utafiti huu umevidondoa visawe ambavyo ni vya moja kwa moja, hasa nomino. Hebu tuone baadhi ya mifano ifuatayo. Mfano 6, 7 na 8 ina visawe vya majina ya wanyama.

Mfano 6: ndovu; tembo

ndovu /*ndovu*/ *nm.* (Ø) {a-/wa-} mnyama pori ambaye ni mkubwa sana, mwenye mkonga mrefu, pembe nyeupe na masikio mapana; **tembo** ... (KKK: 784)

tembo¹ /*tembo* / *nm.* (Ø) {a-/wa-} mnyama mkubwa wa porini wa rangi ya kijivu, mwenye masikio mapana, mkonga anaoutumia kama mkono na pembe mbili kubwa *kis.*: **ndovu**. (KKK: 997)

ndovu /*ndovu*/ *nm* (-) [a-/wa-] ▣ taz. **tembo**¹. (KKS: 427)

tembo¹ /*tembo* / *nm* (-) [a-/wa-] mnyama mkubwa wa nchi kavu mwenye

masikio makubwa na mapana, mkonga na pembe mbili mdomoni;
ndovu. (KKS: 560)

ndovu /ndɔvu/ nm (a-wa) mnyama nkubwa wa porini mwenye pembe mbili na
 mkonga, **tembo.** (KEK: 527)

tembo¹ /tɛmbɔ/ nm (a-wa) mnyama mkubwa wa rangi ya kijivu kilichokoza
 mwenye masikio makubwa, pembe mbili na mwiro au mkonga ambao
 anautumia kama mkono. (KEK: 680)

Mfano 7: nyati; mbogo

nyati /'ja:ti/ nm. (Ø) {a-/wa-} mnyama mkubwa wa nchi kavu jamii ya
 ng'ombe anayeishi porini mwenye pembe zilizopinda kuelekea
 juu vis.: **mbogo**, ng'ombe mwitu. (KKK: 809)

mbogo /'mbɔgɔ/ nm. (Ø) {a-/wa-} mnyama mkubwa wa porini mithili ya
 ng'ombe mwenye pembe kubwa zilizokunjika mbele ... kis.:
nyati. (KKK: 608)

nyati /pati/ nm (-) [a-/wa-] mnyama anayefanana na ng'ombe lakini
 mkubwa zaidi, ana pembe kubwa zilizopinda kuelekea mbele;
mbogo. (KKS: 442)

mbogo /mbɔgɔ/ nm (-) [a-/wa-] ▀ taz. **nyati.** (KKS: 329)

nyati /pati/ nm (a-wa) mnyama pori anayefanana na ng'ombe ambaye ni
 mkali na mwenye pembe ambazo huzitumia kuwa silaha; **mbogo.**
 (KEK: 539)

mbogo /mbɔgɔ/ nm (a-wa) mnyama mkubwa wa porini anayefanana sana

na ng'ombe lakini mkubwa zaidi na mwenye uzito mkubwa zaidi na mwenye pembe zilizokwenda chini kidogo kisha zikapinda na kuelekea juu zilikochongoka; **nyati**, ng'ombe mwitu. (KEK: 407)

Mfano 8: kinyonga; lumbwi

kinyonga¹ /ki'ɲɔŋga/ nm. (vi-) {a-/wa-} aina ya kiumbe spishi ya

reptilia, mwenye miguu yenye uwezo mkubwa wa kujishikiza katika mti, macho marefu na ulimi mrefu wa kukamatia wadudu pamoja na uwezo wa kujibadilisha rangi kutegemea na mazingira alipo. (KKK: 452)

lumbwi /lumbwi/ nm. (vi-) {a-/wa-} **taz. kinyonga.** (KKK: 552)

kinyonga /ki'ɲɔŋga/ nm (vi-) [a-/wa-] mnyama anayebadilika rangi ya

mwili wake ili ifanane na rangi ya mazingira alimo; **lumbwi.** (KKS: 241)

lumbwi /lumbwi/ nm (vi-) [a-/wa-] mnyama anayefanana na mjusi

anayejibadili rangi kulingana na rangi ya mazingira; **kinyonga.** (KKS: 298)

kinyonga /ki'ɲɔŋga/ nm vi (a-wa) **1** mnyama wa jamii ya mjusi aliye na

mazoea ya kubadililadili rangi kutegemea mazingira yake na ambaye huenda kwa mwendo wa polepole. (KEK: 300)

lumbwi /lumbwi/ nm (a-wa) **taz. kinyonga.** (KEK: 368)

Katika mfano 6 na mfano 7, ni KKS tu iliyozingatia mihimili ya nadharia.

Katika Mfano 6, KKS imeingiza fasili katika kisawe kimoja tu – **tembo**¹ na kumwelekeza mtumiaji anayetafuta maana ya neno **ndovu** kwenye kisawe hicho kilichopewa hadhi ya anwani ya urejeleano. Hata hivyo, KKK na KEK

zimevipa visawe hivi hadhi sawa kwa kuvitolea fasili vyote viwili. Katika KEK, kisawe *ndovu* hakikutajwa katika kidahizo *tembo*¹. Katika Mfano 7, KKS imeingiza fasili katika kisawe *nyati* na kuacha kisawe *mbogo* kuwa chanzo cha uejeleano. KKK na KEK zina fasili katika visawe vyote licha ya kuonesha uhusiano uliopo.

Katika mfano wa 8, KKK imezingatia mihimili ya nadharia. Hata hivyo, katika kidahizo *kinyonga*, *lumbwi* halikutajwa kama kisawe. Pia, kamusi hii ina michoro katika vidahizo vyote viwili. Kamusi hii pia imetumia neno *reptilia* ambalo halikuingizwa kama kidahizo kuelezea maana ya *kinyonga*. KKS imeingiza fasili katika vidahizo vyote viwili licha ya kuonesha kuwa maneno haya ni visawe. Pia, maelezo yaliyotolewa yanaonesha moja kwa moja yanafafanua kiumbe kilekile. KEK imefuata mihimili ya nadharia ingawa haikuingiza kisawe *lumbwi* katika kidahizo *kinyonga*.

Mfano ufuatao unaonesha visawe vinavyorejelea kifaa cha kiteknolojia.

Mfano 9: runinga; televisheni

runinga /ru'ninga/ nm. (Ø) {i-/z-} taz. **televisheni**. (KKK: 896)

televisheni /televi'feni/ nm. (Ø) {i-/z-} kifaa kinachonasa sauti,

maandishi na picha kutoka katika kituo maalumu cha matangazo na kuonyesha kwa watazamaji *kis.*: **runinga**. (KKK: 996)

runinga /runinga/ *nm* (-) [i-/zi-] ▀ taz. **televisheni**. (KKS: 493)

televisheni /televifeni/ *nm* (-) [i-/zi-] **1** chombo kinachonasa picha, sauti na maandishi kutoka kituo cha kurushia matangazo na kuvionyesha pamoja na kutoa sauti iliyonaswa; **runinga**. (KKS: 559)

runinga /runinga/ *nm* (i-zi) chombo cha kielektroniki aina ya kiboksi kinachotangaza habari kwa kuonyesha picha na sauti; **televisheni**. (KEK: 600)

televisheni /televifeni/ *nm* (i-zi) chombo kinachonasa mawimbi ya picha na yanayorushwa kwa njia ya satelaiti kutoka vituo mbalimbali na kuonyesha picha na sauti kwa wakati huohuo; **runinga**. (KEK: 679)

Katika mfano huu, KKK na KKS zimezingatia mihimili ya nadharia kwa kuiingiza fasili katika kidahizo kimoja tu, **runinga** na kukipa kile kingine, **televisheni**, hadhi ya anwani ya urejeleano. Hata hivyo, KEK imeingiza fasili katika vidahizo vyote licha ya kutaja kisawe katika kila kidahizo.

Hebu tuone jinsi kamusi zote zilipovishughulikia visawe vya nomino ya dhahania ifuatayo.

Mfano 10: hongo; rushwa

hongo /'hɔŋgɔ/ *nm*. (Ø) {i-/zi-} **a.** fedha au kitu cha dhamani anachotoa

mtu ilia pate huduma asiyostahili vs.: **rushwa** ... (KKK: 305)

rushwa /'ru:fwa/ nm. (Ø) {i-/zi-} mali, pesa au zawadi yoyote apewayo

mtu mwenye cheo au nafasi ya utawala, kiuchumi, kijamii au kisiasa ili kumtendea jambo ijapokuwa jambo hilo ni haki yake ... vis.: chai, **hongo** ... (KKK: 896)

hongo /hɔŋgɔ/ nm (-) (i-/zi-) 1 malipo au zawadi anayotoa mtu ili

kupata haki; **rushwa** ... (KKS: 162)

rushwa /rufwa/ nm (-) (i-/zi-) fedha au kitu cha thamani kinachotolewa

na kupewa mtu mwenye madaraka ya jambo fulani ili mtoaji apatiwe upendeleo; ... **hongo** ... (KKS: 493)

hongo /'hɔŋgɔ/ nm (i-zi) 1 kitu kinachotolewa kwa ajili ya

kumshawishi mtu akubaliane na matakwa yako hususani ya kimapenzi; **rushwa**. (KEK: 192)

rushwa /rufwa/ nm (i-zi) pesa au chochote kitolewacho ili

kumshawishi mtu fulani kutoa kitu au huduma fulani. (KEK: 600)

Katika mfano huu, kati ya kamusi zote zilizochanganuliwa, yaani KKK, KKS na KEK, hamna hata moja iliyofuata mihimili ya nadharia ya miundomedio au mapendekezo ya wataalamu ambao wanasema fasili inapaswa kuingizwa katika kidahizo kimoja, yaani anwani ya urejeleano, na kidahizo kile kingine kuwa chanzo cha urejeleano ambapo mtumiaji wa kamusi anaelekezwa palipo na maelezo kupitia ishara ya urejeleano. Katika kidahizo **rushwa**, KEK haikutaja **hongo** kama kisawe jambo ambalo linachangia urejeleano wa upande mmoja.

3.3 Vinyume

Kulingana na *Kamusi Elezi ya Kiswahili*, kinyume ni “jambo, hali au kitendo kinachokinzana au kisichofungamana au chenye mkabala tofauti na kingine” (uk. 300). Kama ilivyoelezwa katika Sura ya Pili, kati ya kamusi tatu zilizochanganuliwa katika utafiti huu ni *Kamusi Kuu ya Kiswahili* pekee ambayo imeonesha uhusiano wa vinyume vya maneno. Hebu tutazame mifano ifuatayo:

Mfano 11: tawanya; kusanya

tawanya /ta'wana/ kt.ele a sambaza vitu kila sehemu; eneza ... *viny.*:

kusanya, rundika (KKK: 993)

kusanya /ku'sana/ kt.ele weka au rundika pamoja vitu, watu au wanyama. (KKK: 526)

Mfano 12: jishusha; jikweza

jishusha /ji'fu:fa/ kit.sie. fanya jambo linalokupunguzia hadhi na

heshima katika jamii ama kwa makusudi au bila kukusudia *kis.*:
jitweza *kiny.*: **jikweza** (KKK: 345)

jikweza /ji'kwe:za/ kit.sie. jiona kuwa bora kuliko wengine (KKK:
340)

Mfano 13: umaskini; utajiri

umaskini /umas'kini/ nm. (Ø) {u-} hali duni ya kimaisha inayoweza

kumkuta mtu binafsi, shirika au nchi kutokana na kutokuwa na mali ... *viny.*: **utajiri, ukwasi** (KKK: 1092)

utajiri /uta'jiri/ nm. (Ø) {u-} mali nyingi inayomilikiwa na mtu, asasi

au nchi; milki, ukwasi ... (KKK: 1129)

Katika mifano hii, ambayo ni kielelezo cha namna watunzi walivyotumia mbinu ya urejeleano kuhusisha vinyume vya maneno, tunaona kwamba hali hii ya kinyume imeoneshwa upande mmoja tu. Kwa mfano, mtumiaji wa kamusi hii anayetafuta neno *tawanya*, *jishusha* au *umaskini*, atapata taarifa zaidi kuwa maneno hayo yana vinyume *kusanya*, *jikweza* na *utajiri* mtawalia. Hata hivyo, mwingine anayetafuta maelezo ya maneno *kusanya*, *jikweza* na *utajiri* hatapata taarifa za ziada kama hizo. Hali kama hii inasababisha ukosefu wa usawa kwa watumiaji wa kamusi kwani yule anayetafuta kidahizo kilichotolewa kinyume atafaidika zaidi kwa kupata msamiati zaidi ikilinganishwa na mtumiaji ambaye anatafuta kidahizo ambacho hakijatolewa kinyume. Itakuwa bora iwapo watunzi wataamua kuhusisha vinyume kupitia urejeleano wafanye hivyo pande zote mbili.

3.4 Umoja na wingi wa nomino

Kama ilivyoelezwa katika Sura ya Kwanza, wakati mwingine watunzi wa kamusi huingiza maumbo ya umoja na wingi ya nomino. Hapa tutadondoa mifano michache kwa lengo la kubaini iwapo kuna mifanano au tofauti zinazojitokeza kutokana na jinsi watunzi wa kamusi zilizochanganuliwa katika utafiti huu walivyokishughulikia kipengele hiki. Hebu tuangalie mifano 14, 15, 16 na 17 ifuatayo.

Mfano 14: vundevunde; mavundevunde (mavundevunde ni wingi wa

vundevunde)

vundevunde vunde+vunde /vunde'vunde/ nm. (ma-) {li-/ya-} mawingu

meupe yanayotokea katika anga na kusababisha kukosekana kwa nuru ... (KKK: 1158)

mavunde /ma'vunde/ nm. (Ø) {ya-} pia **mavundevunde a.** mawingu

mepesi yanayotanda mithili ya moshi (KKK: 599)

vundevunde /vundevunde/ nm (ma-) [li-/ya-] mawingu meupe

yanayotanda angani na kusababisha kuwepo kwa giza (KKS: 636)

mavundevunde /mavundevunde/ nm (ma-) [li-/ya-] mawingu mfano

wa moshi uliotanda (KKS: 324)

vundevunde /vundevunde/ nm (i-zi) mawingu meupe yanayosongea

nchi kavu na kufanya mandhari ya ukungu angani. (KEK: 745)

mavundevunde /mavundevunde/ nm (ya-) **1** mawingu mepesi

yaonekanayo kama moshi yenye kutawanyika kwa urahisi angani (KEK: 400)

Katika mfano huu, kamusi zote tatu zimeingiza fasili katika maumbo yote mawili jambo ambalo linakinzana na mihimili ya nadharia ya miundomedio na hivyo kutumia nafasi zaidi ambayo ingetumiwa kwa taarifa zaidi au kwa namna fulani kuongeza gharama ya uchapishaji.

Mfano 15: *upwa; pwa* (*upwa* ni wingi wa *pwa*)

pwa¹ /'pwa/ nm. (ma-) {li-/ya-} taz. **upwa**. (KKK: 875)

upwa¹ /u'pwa/ nm. (pwa) {u-/zi-} sehemu ya pwani kati ya eneo la nchi kavu maji yanapoishia wakati wa kujaa na ukomo wa maji yanapokupwa. (KKK: 1113)

pwa² /pwa/ nm (-) [zi-] ■ taz. **upwa**¹ (KKS: 480)

upwa¹ /upwa/ nm (pwa) [u-/zi-] sehemu ya pwani ambayo maji hujaa na kupwa; ufuko (KKS: 617)

Katika mfano huu kamusi zote mbili zimefuata utaratibu ulio sawa ambao unapendekezwa na nadharia. Hata hivyo, katika KKK, anwani ya urejeleano si dhahiri kwani umbo **upwa** limeingizwa kama homonimu; lina *upwa*¹ na *upwa*² na kipeo hakikutajwa katika urejeleano. Pili, katika kidahizo **pwa** ambacho ni wingi wa **upwa**, umbo la wingi limepewa kiano (*ma-*) kumaanisha umbo linalotarajiwa ni '*mapwa*'. Pia, ngeli imeingizwa kama (*li-/ya-*) ambayo inakinzana na ile iliyoingizwa katika anwani ya urejeleano; (*i-/zi-*).

Hebu tuangalie utofauti unaojitokeza katika mfano ufuatao.

Mfano 16: *gugu; magugu* (*magugu* ni wingi wa *gugu*)

magugu /ma'gugu/ nm. (Ø) {ya-} taz. **gugu**. (KKK: 565)

Unapolitafuta neno **gugu** katika kamusi hii, unapata kuwa ni homonimu na hivyo kuna *gugu*¹ na *gugu*² (KKK: 262). Nomino hizi mbili zina wingi

magugu. Hata hivyo, tatizo ni kwamba mtumiaji wa kamusi hajui anwani ya urejeleano iliyokusudiwa ni ipi. Iwapo ni dhana zote zilizo katika homonimu 1 na 2, basi ingekuwa bora iwapo watunzi wangelilingiza neno hilo *gugu* likiwa polisemi badala ya homonimu. Makenge (2019) amewanukuu wataalamu mbalimbali wanaofafanua polisemi kama neno lenye maana mbili tofauti au zaidi lakini zinazohusiana kimawazo au kimaana. Kwa msingi huu, neno *gugu* katika mfano huu lina sifa hizi zote na hivyo ni maoni yetu kuwa lingeingizwa katika kamusi hii kama polisemi badala ya homonimu. Iwapo wangepanya hivi basi utata unaojitokeza kupitia urejeleano wa wingi na umoja haungekuwepo.

Mfano ufuatao una upekee wake pia.

Mfano 17: *kufuru*; *makufuru* (makufuru ni wingi wa kufuru)

makufuru¹ /*maku'furu*/ nm (Ø) {*ya-*} taz. **kufuru**. (KKK: 573)

Katika KKK, kuna **kufuru**¹ (kitenzi) na **kufuru**² (nomino). Unapotazama chanzo cha urejeleano katika mfano huu utaona kwamba anwani ya urejeleano si dhahiri kwani haikuelekeza iwapo ni **kufuru**¹ na **kufuru**². Bila shaka inatarajiwa kuwa, kwa kuwa chanzo cha urejeleano ni nomino, basi anwani ya urejeleano itakuwa nomino pia. Hata hivyo, **kufuru**² iliyotarajiwa kuwa anwani ya urejeleano imeingizwa kuwa umbo lake katika umoja na wingi halibadiliki kwani limepewa ngeli ya (*i-/zi-*) ilhali nomino ambayo ni chanzo cha urejeleano imeoneshwa kuwa katika ngeli ya (*ya-*).

3.5 Vifungu vya maneno

Katika utafiti huu, vifungu vya maneno vinavyorejelewa ni vitatu: nahau, misemo na methali. Svenson (1993) anasema kuwa, kwa kuwa fungu la maneno lina maneno mengi, kwa kawaida linaweza kushughulikiwa katika kila neno linaloliunda fungu hilo, lakini ikifanyika hivyo basi maelezo hayo yatachukua nafasi kubwa. Hivyo ni vyema kukishughulikia kifungu hicho katika neno moja na kutumia mbinu ya urejeleano katika maneno yale mengine. Kiango (1996) anapendekeza kuzingatia neno la msingi au la kwanza katika kuingiza vifungu vya maneno kama vile nahau, misemo na methali. Hata hivyo, kama tulivyosema katika Sura ya Kwanza, hakuelekeza namna ya kuyarejelesha maneno mengine yanayoziunda tungo hizi. Pia, ametaja kuwepo kwa wanaleksikografia ambao wanapendekeza kuingiza methali, nahau au msembo chini ya kila neno linalotajwa katika mtungo huo, jambo analosema kuwa limeonekana kuchukua nafasi kubwa katika kamusi kwa sababu ya kurudiarudia.

Udurusu wa kamusi zote tatu unaonesha kuwa kuna watunzi walioviingiza vifungu vingi huku wengine wakiviingiza vichache. Hivyo, aghalabu inakuwa vigumu kupata kifungu kimoja ambacho kimeingizwa katika kamusi zote tatu.

3.5.1 Nahau

Kulingana na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu*, “nahau” ni fungu la maneno lenye maana maalumu isiyotokana na maana za kawaida za maneno

hayo. Kwa kawaida, nahau hutambulishwa na matumizi ya kitenzi katika fungu hilo, k.m. *kata kamba, kula mwata*, na kadhalika.

Kamusi zilizochanganuliwa katika utafiti huu zimeziingiza nahau nyingi. Hebu tuone jinsi watunzi walivyoziingulikia nahau kwa kuzingatia mifano ifuatayo tuliyoidondoa moja kwa moja.

Mfano 18: *piga mbizi*

piga (KKK: Ø)

mbizi zamisha mwili wote ndani ya maji. (KKK: 608)

piga zama chini ya maji k.v. baharini au mtoni (KKS: 468)

mbizi jizamisha majini; ogelea hali umefunikwa na maji (KKS: 329)

piga ogelea kwa kuzama majini (KEK: 572)

mbizi kuogelea kwa kuzama ndani ya maji au kuzama akilini mwako na kulifikiria au kuliwaza jambo kwa undani (KEK: 406)

Katika mfano huu, *Kamusi Kuu ya Kiswahili* imeingiza nahau hii katika kidahizo kimoja tu, *mbizi*. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* na *Kamusi Elezi ya Kiswahili* zote zimeingiza nahau hii katika maneno yote mawili na kuitolea maana katika kila neno, jambo ambalo linakinzana na nadharia ya urejeleano.

Mfano 19: *vunja rekodi*

vunja fanya vizuri zaidi (KKK: 1159)

rekodi (KKK: Ø)

vunja pita rekodi iliyokuwa imewekwa hapo awali (KKS: 637)

rekodi tia fora; vuka mpaka (KKS: 487)

vunja fanya vizuri zaidi kuliko waliowahi kufanya jambo hilo (KEK:
746)

rekodi (KEK: Ø)

Katika mfano huu, KKS imeingiza nahau hii katika maneno yote mawili na kuitolea maana katika kila neno, kinyume na inavyopendekeza nadharia. KKK na KEK zimeingiza katika neno moja tu, yaani *vunja* na kukosa kufanya hivyo katika neno rekodi. Hii ina maana kuwa mtumiaji wa kamusi anayetafuta neno *rekodi* hatapata nafasi ya kujua kuwa kuna nahau inayotumia neno hilo.

Hebu tuangalie mifano inayofuata tuone imechukua mtindo gani.

Mfano 20: *piga chafya*

piga chemua hewa chafu mapafuni (KKK: 856)

chafya toa pumzi kwa ghafla na kwa nguvu kupitia puani na mdomoni (KKK: 108)

piga chemua (KKS: 468)

chafya toa hewa puani/mdomoni kwa ghafla na bila kukusudia (KKS: 57)

Mfano 21: *fua dafu*

fua fanikisha jambo (KKK: 223)

dafu mudu kufanya jambo fulani (KKK: 153)

fua weza jambo; mudu; shinda (KKS: 117)

dafu thubutu kufanya jambo; weza jambo; mudu (KKS: 80)

Mfano 22: *vunja ungo*

vunja pata hedhi kwa mara ya kwanza (KKK: 1159)

ungo fikia hali ya kuweza kushika ujauzito (KKK: 1099)

vunja pata hedhi kwa mara ya kwanza (KKS: 637)

ungo baleghe, hasa kwa wasichana (KKS: 611)

Katika nahau *piga chafya, fua dafu* na *vunja ungo* KKK na KKS zimeingiza nahau hizi katika maneno yote mawili yanayoziunda kinyume na mapendekezo ya nadharia. KEK haikuziingiza nahau hizi. Kwa kuwa kamusi hii, yaani KEK, imeziingiza baadhi ya nahau, inaonekana kuwa watunzi wake hawakufuata utaratibu sawa walipovishughulikia vidahizo vyote. Matokeo ya hali hii ni kuwa watumiaji wa kamusi hii watakosa taarifa zaidi ambazo watumiaji wa kamusi zile nyingine wanapata.

Kama tulivyosema katika Sura ya Kwanza na inavyobainika katika mifano iliyo hapo juu ni kwamba hakuna kamusi hata moja kati ya tatu zilizochanganuliwa iliyozingatia mihimili ya nadharia ya miundomedio katika kuwasilisha nahau. Hii ndiyo sababu maelezo yametolewa katika maneno yote yanayoiunda nahau husika. Athari ya hatua hii itabainika katika sura inayofuata.

3.5.2 Misemo

Kulingana na *Kamusi Kuu ya Kiswahili*, msemu ni fungu la maneno lenye maana mahsusi ili kutoa fundisho kwa jamii. Kamusi zote tatu zilizochanganuliwa zimeingiza misemo ingawa michache. Hebu tuone kupitia mifano 24 – 29 jinsi watunzi wa kamusi hizi walivyoishughulikia misemo.

Mfano 23: *tupa jongoo na mti wake*

tupa² achana na jambo au kitu kwa muda mrefu (KKK: 1026)

jongoo sahau au acha jambo kabisa (KKK: 350)

Mfano 24 *nyota ya jaha*

jaha bahati kubwa (KKK: 326)

nyota² bahati nzuri (KKK: 815)

Mfano 25: *harusi imejibu*

arusi bibi arusi amekutwa kwamba ni bikira (KKK: 41)

harusi kuthibitika kwa hali ya ubikira kwa biharusi wakati wa harusi

kwa kutoka damu wakati wa kuingiliwa kimwili na bwanaharusi agh. katika utamaduni wa Waswahili (KKK: 286)

Mfano 26: kazi ya kijungu jiko

jiko kazi ya kumpatia mtu chakula bila ya kubakiwa na akiba (KKS: 179)

meko kazi ya kumpatia mtu chakula bila ya kubakisha (KKS: 340)

Mfano 27: mtoto wa kikopo

kikopo mhuni; mtovu wa haya (KKS: 231)

kopo³ mhuni (KKS: 274)

Mfano 28: ona cha mtema kuni

mtema kuni juta siku ya uzawa wako (KEK: 490)

ona patwa na mambo mabaya hasa kama adhabu ya kutenda maovu (KEK: 546)

Kulingana na mifano hii, mitatu kutoka KKK, miwili kutoka KKS, na mmoja kutoka KEK, hakuna kamusi hata moja kati ya zote tatu zilizochanganuliwa ambayo imezingatia mapendekezo ya nadharia ya miundomedio. Hii ni kwa sababu tunaona kuwa watunzi wameingiza maelezo ya misemo katika kila neno linaloiunda misemo hiyo. Iwapo wangezingatia mihimili ya nadharia wangeyaingiza maelezo ya msemu katika neno moja na pale pengine wakamwelekeza mtumiaji wa kamusi yalipo maelezo yale kupitia urejeleano.

Kwa namna hii wangepunguza uradidi na hivyo kuokoa nafasi, na pia kuepuka hali ambapo wanatoa maelezo yanayotofautiana kuhusu msembo uleule kama inavyoashiriwa na mifano hiyo.

3.5.3 Methali

Kamusi zote tatu zimeingiza methali mbalimbali. Kwa kawaida methali za Kiswahili ni mafungu ya maneno mawili au zaidi. Katika *Kamusi Kuu ya Kiswahili*, tuliweza kunukuu methali 38 ambazo zimetolewa maelezo katika maneno tofauti yanayoiunda methali husika. Katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* na *Kamusi Elezi ya Kiswahili*, tulinukuu methali 36 na nane mtawalia, ambazo zimetolewa maelezo katika maneno yalizoiunda. Hata hivyo, katika KKS, kati ya methali hizo, ni moja tu iliyotolewa maelezo katika maneno mawili. Inaonekana watunzi wa kamusi hii waliziorodhesha methali tu bila maelezo. Hapa tutatumia mifano mitano ambayo imo katika kamusi zote tatu kuonesha mifanano na tofauti katika urejeleano katika kamusi hizi.

Mfano 29: *Ada ya mja hunena muungwana ni kitendo.*

Mfano 30: *Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.*

Katika KKK, methali ‘Ada ya mja hunena muungwana ni kitendo’ imeingizwa katika kidahizo **ada**² (Thamani ya mtu ni vitendo sio wasifu), **mja** (Binadamu huthaminiwa kwa vitendo vyake na sio mwonekano wake) na **muungwana**

(Mtu mwema hutambulika kwa matendo yake, lakini domokaya kwa maneno matupu.) Katika KKS, methali hii imeingizwa katika vidahizo **ada**² na **muungwana** lakini haikutolewa maana. Katika KEK, imeingizwa katika **ada**² (Wema wa mtu hutambulika kwa vitendo, wala si kwa maneno.) na **muungwana** (Binadamu wana mazoea ya kusema tu lakini wachache walio waungwana husema na kutenda.).

Vilevile, KKK imeingiza methali ‘Mgaagaa na upwa hali wali mkavu’ hii katika **mgaagaa** (Mtu anayefanya jitihada za kutafuta riziki hufanikiwa.), **gaagaa** (Anayepita mahali penye riziki mara kwa mara, aweza kubahatika.) na **upwa** (Mtu apitaye penye matumaini hatoki mtupu.). KKS imeingiza methali hii katika vidahizo **gaagaa** na **mgaagaa**² lakini haikuitolea maana. KEK imeingiza katika **garagara**, ambacho wamesema ni kbadala cha **gaagaa** (Anayejitahidi katika jambo fulani mwishowe hufanikiwa.), na **mgaagaa**² (Mtu yeyote anayetia bidi japo kidogo katika jambo lolote, hufanikiwa.)

Kulingana na mifano hii miwili, tunaona kuwa KKK imeingiza kila methali katika vidahizo vitatu na kuitolea maana katika vidahizo vyote, KKS imeingiza kila methali katika vidahizo viwili bila kuitolea maelezo, na KEK ikaingiza kila methali katika vidahizo viwili na kuitolea maana katika vidahizo vyote viwili. Hii inamaanisha kuwa kamusi zote zinafanana katika kutozingatia mihimili ya nadharia ya miundomedio inayosisitiza neno moja liwe anwani ya urejeleano na mengine yanayoliunda fungu hilo kupewa sifa za vyanzo vya

urejeleano. Kama tulivyoona maelezo hayo yanachukua nafasi na hivyo bila shaka yatachangia ukubwa wa kamusi na hatimaye kuongeza gharama ya uchapishaji. Vilevile, tukiangalia kwa makini tunaona kuwa maelezo ya methali ileile yanayotolewa katika vidahizo tofauti yanatofautiana kwa namna moja au nyingine.

Mfano ufuatao una upekee wake.

Mfano 31: *Lila na fila havitangamani.*

KKK imeingiza methali hii katika **lila**¹, **fila** na **tangamana** na kuitolea maana mara moja tu katika kidahizo **fila** (Uadilifu na uovu havipatani). KKS imeingiza katika vidahizo **fila** (Wema na ubaya haviambatani.) na **lila** (Wema na ubaya haviafikiani.). KEK imeingiza katika **fila** (Zuri na baya hayawezi kuchangamana katika chungu kimoja.) na **lila** (Vitu vinavyokuwa pamoja kiuasilia si rahisi kutengana).

Katika mfano huu, KKK imeingiza methali hii mara tatu lakini ikatoa maelezo katika kidahizo kimoja tu. Hata hivyo mtumiaji wa kamusi hakuelekezwa palipo na maelezo ya methali. Hii inamaanisha kuwa mtumiaji wa kamusi anayetafuta neno *fila* tu ndiye atakayepata kujua maana ya methali hii. Wale wengine wataijua methali ila hawatajua maana yake. KKS na KEK zimeingiza methali hii katika vidahizo viwili kila moja na kuitolea maana katika vidahizo vyote viwili kinyume na mihimili ya nadharia ya miundomedio. Pia, maelezo

yaliyotolewa katika vidahizo vyote viwili vya KEK ni tofauti kabisa jambo linaloweza kuwapa watumiaji wawili tofauti wanayoyatafuta maneno hayo mawili picha mbili tofauti za methali moja.

Hebu tuangalie mfano mwingine ufuatao.

Mfano 32: *Mtaka cha mvunguni sharti ainame.*

Katika KKK, methali hii imeingizwa katika vidahizo **mvungu** (Ukitaka kitu fulani ni lazima uwe tayari kukisumbukia.) na **sharti**³ (Ili kupata mafanikio lazima kupitia misukosuko). Katika KKS, imeingizwa katika vidahizo **mtaka**, **sharti**³ na **mvungu** ila hakuna iliyotolewa maana. KEK imeingiza methali hii katika vidahizo vitano: **inama** (Mtu akila kitu cha tunu lazima afanye bidii.), **mtaka** (Atakaye kitu lazima ajikakamue.), **mvunguni** (Kufaulu katika jambo kunahitaji bidii.), **taka** (Ukitaka kufanikiwa kwenye jambo lolote ni lazima ujitume kwa kufanya kazi kwa bidii.), na **sharti**³ (Ili kupata mafanikio lazima kupitia misukosuko.).

Katika mfano huu tunaona kuwa KKK imeingiza methali hii katika vidahizo viwili na kuitolea maelezo katika vidahizo vyote viwili kinyume na mihimili ya nadharia ya miundomedio, KKS imeingiza methali hii katika vidahizo vitatu ila haikutolewa maana. Hii inamaanisha kuwa mtumiaji wa kamusi hii atajua kuwa kuna methali kama hii ila hatapata kufahamu maana ya methali hiyo. KEK, kwa upande wake, imeingiza methali hii mara tano, na katika kila

kidahizo maelezo ni tofauti. Hali hii inaenda kinyume na mihimili ya nadharia ya miundomedio na hatimaye kuwa na uradidi mwingi na hivyo kuongeza gharama ya uchapishaji ambayo itapitishwa kwa mtumiaji wa kamusi.

Hebu tuangalie mfano wa mwisho katika sehemu hii.

Mfano 33: *Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani.*

Katika KKK, methali hii imeingizwa katika vidahizo **marejeo** (Mtu hata akienda wapi atarudi nyumbani kwao.), **omo** (Ukienda mbele na nyuma utaishia katikati), **ngama**¹ (Mtu anayetangatanga huku na kule hatimaye atarudi nyumbani.) na **tezi**¹ (Kokote mtu atakapokwenda nyumbani ndio pahali bora zaidi.). Katika KKS, methali hii imeingizwa katika vidahizo **ngama**² na **marejeo** lakini haikutolewa maana. Katika KEK, imeingizwa katika **marejeo** (Aendaye huku na huku mara hujipata amerudi alikotoka.), **tezi**¹ (Kila anayetoka sehemu moja kwenda nyingine kwa ajili ya kuhangaika katika kutafuta maisha au mali baadaye hurudi palepale alipotoka.) na **omo** (Hata mtu fulani akaenda sehemu tofautitofauti hatimaye hurudi nyumbani kwao au hurudia watu wake.).

Katika mfano huu KKK imeingiza methali hii katika vidahizo vinne na kuitolea maana katika kila kidahizo, KKS imeingiza katika vidahizo viwili bila kuitolea maelezo, nayo KEK ikaiingiza katika vidahizo vitatu na kuitolea maelezo katika kila kidahizo. Hapa tunaona kuwa hakuna kamusi iliyozingatia

mihimili ya nadharia ya miundomedio wala mapendekezo ya wataalamu kuhusu urejeleano.

Mifano hii mitano kutoka katika kamusi hizi tatu ni dhihirisho kuwa watunzi hawakuzingatia mihimili ya miundomedio. Hii ndiyo sababu kuna fasili ya methali katika takriban kila neno linaloiunda methali husika. Inatarajiwa kuwa maelezo ya methali moja hayapaswi kubadilika katika kamusi moja. Hata hivyo, kama tulivyoona methali moja imetolewa maelezo yanayotofautiana.

Mifano zaidi kama hii iko katika sehemu ya Viambatisho.

3.6 Hitimisho

Katika sura hii, tumenukuu mifano mbalimbali ya vipengele vinavyoweza kuhusishwa kupitia urejeleano. Tumeona kuwa kuna baadhi ya vipengele ambavyo watunzi wa kamusi zilizochanganuliwa walivishughulikia kwa njia sawa na vingine ambavyo walifuata mikondo tofauti. Katika kufanya hivyo, kuna taratibu ambazo zimezingatia mihimili ya nadharia ya miundomedio na nyingine ambazo hazikufanya hivyo. Kutozingatia mihimili ya nadharia kuna athari ambazo zimeshughulikiwa katika sura inayofuata.

SURA YA NNE

ATHARI YA UREJELEANO NA MAPENDEKEZO YA KUBORESHA UREJELEANO

4.0 Utangulizi

Katika Sura ya Pili na ya Tatu, tumeonesha vipengele ambavyo vinaweza kuhusishwa kupitia urejeleano, na mishabaha na tofauti za matumizi ya urejeleano katika kamusi teule, mtawalia. Vilevile, katika Sura ya Tatu tumebainisha kuwa kwa kiwango kikubwa watunzi wa kamusi hizi hawakutumia vigezo sawa katika kukishughulikia kipengele cha urejeleano. Kwa hakika, inaonekana kuwa hawakuongozwa na mihimili ya nadharia ya miundomedio. Ni maoni yetu kuwa iwapo walikuwa wameongozwa na nadharia hii, bila shaka kungekuwa na ukuruba fulani katika uwasilishaji wa vipengele vilivyohusishwa kupitia urejeleano.

Sura hii imeangazia athari ambazo zinaibuka kutokana na matumizi ya urejeleano kama unavyojitokeza katika kamusi zilizochanganuliwa, na kwa jumla, athari ambazo zinaweza kujitokeza iwapo urejeleano hautaegemezwa kwenye mihimili ya nadharia ya miundomedio, na pia mapendekezo ya kuboresha urejeleano katika kamusi za Kiswahili za lugha moja. Hivyo basi, katika sura hii tamerejelea kwa kifupi matumizi yanayofaa na yasiyofaa ya urejeleano kama tulivyoyabainisha katika sura zilizotangulia na kuonesha

athari zinazojitokeza kutokana na matumizi hayo, na pia jinsi athari hizo zinavyoweza kuepukwa kupitia mapendekezo yetu.

4.1 Athari

Kulingana na *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2015 :45), athari ni “matokeo mazuri au mabaya yampatayo mtu au kitu baada ya kupitia hatua fulani”. Fasili hii inaashiria kuwa athari zinaweza kuwa chanya au hasi. Kulingana na matokeo ya utafiti tulioufanya kuna athari chanya zinazojitokeza kutokana na matumizi ya urejeleano kwa namna inayofaa. Vilevile, kuna athari nyingi hasi zinazotokana na matumizi yasiyofaa ya urejeleano. Athari hizi zinawaathiri wachapishaji na watumiaji wa kamusi kwa njia moja au nyingine. Hebu tuone jinsi athari hizi zinavyowaathiri wahusika hawa.

4.1.1 Athari Chanya

Hizi ni athari nzuri zinazotokana na matumizi yanayofaa ya urejeleano. Athari hizi zinatokea pale watunzi wa kamusi wametumia urejeleano kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya miundomedio.

4.1.1.1 Athari Chanya kwa Wachapishaji

Kulingana na Meneja Mchapishaji wa Oxford University Press East Africa, mchakato mzima wa uchapishaji, kutoka kwa hatua ya kuuandika mswada, uhariri hadi uchapaji wa kamusi huwachukua wachapishaji muda mrefu na pia

kuwagharimu hela nyingi. Haya ni maoni ambayo yaliungwa mkono na Meneja Mzalishaji katika shirika hilo ambaye alisema kuwa kwa kawaida, gharama ya uhariri na uchapaji hukadiriwa kikurasa kwani malipo yake hulipwa kikurasa. Kwa msingi huu basi, ukubwa wa kitabu unaotokana na idadi za kurasa bila shaka huelekeza gharama itakayohusika kukichapisha kitabu hicho. Kulingana naye, iwapo kitabu kina kurasa nyingi ndivyo kitakavyohitaji pesa nyingi kukichapisha, na vivyo hivyo iwapo kitabu kina kurasa chache ndivyo gharama ya kukichapisha itakavyokuwa ya chini. Kwa msingi huu, wachapishaji hutilia maanani ukubwa wa vitabu ili waweze kuidhibiti gharama ya uchapishaji. Kulingana nao, bei ya kitabu sokoni pia hutegemea gharama ya uchapishaji. Iwapo gharama ya kukichapisha ilikuwa juu, bila shaka bei ya kitabu hicho itakuwa juu, jambo ambalo huenda likawafanya watumiaji wasikinunue kwa wingi na hivyo mchapishaji kupata hasara. Kando na ukubwa wa kitabu unaotokana na wingi wa kurasa, wataalamu hawa wa uchapishaji walisema kuwa idadi ya nakala zinazochapishwa kwa mkupuo mmoja, uteuzi wa matbaa ya kuchapa, idadi ya michoro, idadi ya rangi zinazotumiwa katika kitabu, kiwango cha ubora wa uchapaji wenyewe, kiwango cha mrabaha kwa wandishi, pamoja na kiwango cha faida kwa wachapishaji pia huchangia pakubwa gharama ya uchapishaji ambayo hupitishiwa watumiaji wa vitabu.

Kiuhalisia, kamusi huwa na taarifa nyingi kuliko vitabu vya kawaida na hivyo huwa kubwa. Changamoto kubwa ambayo huwakumba wachapishaji hapa ni jinsi ya kuwa na kamusi yenye taarifa nyingi lakini bila ya kuongeza gharama

ya uchapishaji. Katika utunzi wa kamusi, kando na matumizi ya lugha kienzo na fonti ndogo ya maandishi, kipengele cha urejeleano husaidia pakubwa kufanikisha hili kwani kupitia kwacho, nafasi ambayo ingetumika hupunguzwa kwa kutoyaingiza maelezo katika kidahizo fulani iwapo maelezo yayo hayo yameingizwa katika kidahizo kingine kinachohusiana nacho. Svenson (1993) anasema kuwa mojawapo ya sababu kuu za kutumia urejeleano inavyofaa ni kupunguza nafasi ambayo ingetumiwa na taarifa ambazo zinaweza kupatikana katika sehemu nyingine. Nkomo (2008) anasema kuwa mwanaleksikografia ataokoa nafasi kwa kuepuka uradidi pale ambapo maneno yaliyo na uhusiano yameingizwa katika sehemu tofauti katika kamusi.

Iwapo basi watunzi wa kamusi wataepuka uradidi wa taarifa bila shaka watapunguza ukubwa wa kamusi, ambao huathiri pakubwa gharama ya uchapishaji. Kwa mfano, pale ambapo maneno ni vidadala, au visawe vya moja kwa moja, kama tulivyokwisha kuona, hakuna haja ya kuyapa uzito sawa katika kamusi. Maelezo yanapaswa kutolewa tu katika anwani ya urejeleano kama nadharia ya miundomedio inavyoelekeza.

Kwa kiasi kikubwa, kama tulivyobainisha katika Sura ya Pili, kipengele cha urejeleano kimetumiwa vyema katika baadhi ya vidadala na visawe vya moja kwa moja, jambo ambalo limepunguza nafasi iliyotumika na hivyo moja kwa moja kuwapunguzia wachapishaji gharama ya uchapishaji.

4.1.1.2 Athari Chanya kwa Watumiaji wa Kamusi

Katika Sura ya Kwanza tumewanukuu Gouws na Prinsloo (2005) wakimnukuu Wiegand anayesema kuwa lengo la urejeleano katika utunzi wa kamusi ni kufanikisha mtandao mwafaka wa vipengele vya lugha vinavyohusiana. Mtandao kama huu unalengwa kumfaidi mtumiaji wa kamusi. Pale ambapo urejeleano umefanywa kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya miundomedio, mtumiaji atapata taarifa zaidi na sahihi na pia kujua uhusiano uliopo baina ya maneno husika. Kwa mfano, iwapo visawe na vibadala vimeingizwa vizuri bila shaka yule mtumiaji atafaidika.

Kulingana na watumiaji waliorudisha hojaji zetu, kamusi zote tatu zilizochanganuliwa katika utafiti huu zinajulikana na zinatumika, ingawa kwa viwango tofauti tofauti. Kwa mfano, asilimia sitini na nane (68%) ya waliorudisha hojaji walitumia *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, asilimia saba (7%) walitumia *Kamusi Kuu ya Kiswahili* na asilimia tatu (3%) walitumia *Kamusi Elezi ya Kiswahili*. Wengine (asilimia ishirini na mbili 22%) walitaja kamusi ambazo ziko nje ya mipaka ya utafiti huu.

Takribani wahojiwa wote walitaja kuwa kando na fasili za maneno, kamusi walizozitumia zina taarifa nyingine nyingi zikiwemo namna ya kutamka, aina za maneno, mifano ya matumizi, uelekezi wa vitenzi, wingi wa nomino, visawe, vibadala, methali, nahau na misemo. Taarifa hizi, kulingana nao, ziliziboresha kamusi hizo na kuwafaidi sana.

Kama tulivyokwisha kuona, kamusi zilizochanganuliwa zina utaratibu wa kubainisha visawe na vibadala vilivyoingizwa. Utaratibu huu, kulingana na wahojiwa, ulirahisisha kwa namna moja au nyingine kuelewa uhusiano uliopo baina ya maneno. Kutokana na urejeleano wa visawe, kwa mfano, mtumiaji wa kamusi anaimarisha kanzi yake ya msamiati wa lugha ya Kiswahili, jambo ambalo, kulingana na wahojiwa linachangia pakubwa katika upanukaji wa msamiati wao. Kwa mfano, mtumiaji anajulishwa kuwa *tembo*, *mbogo*, *tarakilishi*, *mlo* na *mja* ni visawe vya *ndovu*, *nyati*, *kompyuta*, *chakula* na *mtu*, mtawalia.

Kama tulivyoona katika Sura ya Pili na Sura ya Tatu, ni *Kamusi Kuu ya Kiswahili* pekee iliyotumia urejeleano kuhusisha vinyume vya maneno. Kulingana na wahojiwa waliotumia kamusi hii, hii ni hatua muhimu sana katika kupanua uelewa wa uhusiano wa maneno kwa mtumiaji wa kamusi. Hii ni kwa sababu mtumiaji wa kamusi anaweza kujua antonimu za maneno ambayo yametolewa vinyume kupitia urejeleano, jambo ambalo linamfaidi sana.

4.1.2 Athari Hasi

Hizi ni athari mbaya zinazotokana na matumizi yasiyofaa ya urejeleano. Athari hizi zinaibuka pale ambapo watunzi wa kamusi hawakuuegemeza urejeleano

kwenye mihimili ya nadharia ya miundomedio. Hebu tuone athari hizi kwa wachapishaji na watumiaji wa kamusi.

4.1.2.1 Athari Hasi kwa Wachapishaji

Katika Sura ya Pili tumemnukuu Svenson (1993) anayesema kuwaona kuwa mojawapo ya dhima ya urejeleano ni kupunguza nafasi inayotumiwa na maelezo. Katika sura hii pia tumemnukuu Nkomo (2008) anayesema vivyo hivyo. Bila shaka, iwapo nafasi itapunguzwa inamaanisha kamusi itakuwa na kurasa chache na hivyo kupunguza gharama ya uchapishaji.

Kama tulivyodokeza awali kutokana na mahojiano na baadhi ya wachapishaji, mojawapo ya vipengele vinavyochangia gharama ya uchapishaji ni ukubwa wa kitabu. Kwa sababu hii, ili kupunguza gharama hii wachapishaji hutafuta mbinu ambazo wanaweza kutumia kupunguza ukubwa wa kitabu bila kuathiri ubora wa kitabu kile. Mbinu moja ya kufanya hivi ni kutumia urejeleano. Hata hivyo, kama tulivyokwisha kuona kwingineko katika tasnifu hii ni kwamba pale ambapo urejeleano haukuegemezwa kwenye mihimili ya nadharia ya miundomedio bila shaka kunakuwa na uradidi mwingi wa maelezo na hatimaye kuchangia katika ukubwa wa kamusi na hivyo kupandisha gharama ya uchapishaji.

Kulingana na mifano iliyobainishwa katika Sura ya Tatu ya tasnifu hii, kwa kiwango kikubwa watunzi wa kamusi zilizochanganuliwa hawakuuegemeza

urejeleano kwenye mihimili ya nadharia ya urejeleano. Kwa sababu hii tunapata vibadala na visawe vya moja kwa moja vimepewa uzito sawa kama vitomeo. Kwa mfano, kwa nini tuwe na fasili kamili katika vibadala kama vile *pweteka/bweteka; rodi/lodi; roga/loga; mluzi/mruzi; mava/mafafa; bushti/bushuti; chubwi/tupwi; kifaru/faru; ipua/epua; lubega/rubega; glavu/glovu* au *akina/kina*? Pia, kuna visawe ambavyo ni vya moja kwa moja, kama vile nomino zinazotaja watu, wanyama au vitu mbalimbali. Kwa mfano, tazama mifano tuliyoifafanua katika Sura ya Tatu, kama vile *mbogo/nyati, tembo/ndovu, kompyuta/tarakilishi, na televisheni/runinga*. Isitoshe, kuna sehemu ambazo, kando na kuyarudia maelezo, michoro pia imeingizwa katika vidahizo vyote na hivyo kutumia nafasi zaidi. Uradidi huu, ambao haumpi mtumiaji wa kamusi taarifa zaidi, umechangia ukubwa wa kamusi. Kulingana na mihimili ya nadharia ya miundomedio, hakuna haja ya kuyaingiza maelezo katika kila kibadala au kisawe cha moja kwa moja kwani dhana ni ileile. Kutozingatia mihimili ya nadharia hii kumepelekea matumizi ya nafasi zaidi ambayo imechangia ukubwa wa kamusi na hivyo kuathiri moja kwa moja gharama ya uchapishaji.

Kama tulivyoona kamusi zote tatu zilizochanganuliwa zimetumia urejeleano. Hata hivyo, imedhihirika kupitia mifano anuwai kuwa kuna sehemu ambazo watunzi hawakuelekezwa na nadharia ya miundomedio na hivyo kuchangia ukubwa wa kamusi, jambo ambalo lingepukika iwapo wangeizingatia kwa makini nadharia hiyo. Kati ya kamusi zote tatu, *Kamusi Kuu ya Kiswahili* ndiyo kubwa zaidi ikiwa na kurasa 1,302. *Kamusi Elezi ya Kiswahili* ina kurasa

828, nayo *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* ina kurasa 704. Bei ya kamusi hizi sokoni ni tofauti. Hata hivyo, kama ilivyoelezwa katika sehemu ya 4.1.1.1 ya tasnifu hii, gharama ya uchapishaji huchangiwa na vipengele vingine vingi kando na ukubwa wa kitabu unaotokana na wingi wa kurasa. Kwa sababu hii, si ajabu kupata kamusi ambayo ina kurasa nyingi ikiuzwa kwa bei ya chini ikilinganishwa na nyingine ambayo ina kurasa chache kuliko, au iliyo na kurasa chache ikiuzwa kwa bei ya juu ikilinganishwa na ile iliyo na kurasa nyingi.

Pale ambapo watunzi wa kamusi wanaamua kuyaingiza mafungu ya maneno kama vile nahau, misemo na methali katika kamusi ni sharti wawe makini ili wasitumie nafasi kubwa kupitia uradidi. Katika Sura ya Kwanza tumewanukuu wataalamu kama vile Kiango (1996) anayesema kuwa kuyaingiza mafungu ya maneno katika kila neno linaloliunda fungu hilo kumeonekana kuchukua nafasi kubwa katika kamusi kwa sababu ya kurudiarudia. Kwa mfano, tukiangalia Sura ya Tatu, tunaona kwamba watunzi wa kamusi zilizochanganuliwa hawakukitilia maanani kipengele cha urejeleano ili kuweza kuhusisha maneno yanayoyaunda mafungu haya. Hatua hii, kama tulivyoona, inakinzana na maoni ya wanaleksikografia tuliowataja na pia nadharia ya miundomedio inayoelekeza kuwa maelezo yawe tu katika kidahizo kimoja kilichopewa hadhi ya anwani ya urejeleano huku kidahizo kile kingine kikipewa hadhi ya chanzo cha urejeleano. Hii ndiyo sababu tumeona maana zikijirudia katika kila umbo la neno linaloliunda fungu husika. Methali, kwa mfano, ambazo zimeundwa

kwa maneno mengi zimetumia nafasi kubwa sana ambayo ingetumiwa na vipengele vingine. Kwa mfano, hebu tazama methali zifuatazo:

Mfano 1: *Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.*

Mfano 2: *Mtaka cha mvunguni sharti ainame.*

Kama tulivyoona katika Sura ya Tatu, methali *Mgaagaa na upwa hali wali mkavu* imeingizwa mara tatu katika KKK kwenye vidahizo *mgaagaa, gaagaa* na *upwa* na kutolewa maana ambazo hazifanani; mara mbili katika KKS kwenye vidahizo *mgaagaa* na *gaagaa* ila haikutolewa maana; na katika KEK imeingizwa mara mbili katika *garagara* na *mgaagaa* na kutolewa maana. Vivyo hivyo, methali *Mtaka cha mvunguni sharti ainame* imeingizwa mara mbili katika KKK kwenye vidahizo *mvungu* na *sharti*³ na kutolewa maana katika kila kidahizo; mara tatu katika KKS kwenye vidahizo *mtaka, mvungu* na *sharti*³ bila kutolewa maana; na mara tano katika KEK kwenye vidahizo *inama, mvunguni, taka, mtaka* na *sharti*¹ na kutolewa maana katika kila kidahizo. Kulingana na mihimili ya nadharia ya miundomedio ingefaa maana kuingizwa mara moja na kisha mbinu ya urejeleano kutumiwa kuyahusisha maneno hayo mengine na pale ilipo maana hiyo. Kwa namna hii, ile athari ya ukubwa wa kamusi inayotokana na uradidi wa taarifa zinazofanana ingeweza kuepukika kwa kiwango fulani na hivyo kumpunguzia mchapishaji gharama ya uchapishaji.

4.1.2.2 Athari Hasi kwa Watumiaji wa Kamusi

Ni ukweli ulio dhahiri kuwa kitabu chochote huandikwa na kuchapishwa ili kiweze kusomwa. Hivyo basi ni bayana kamusi hutungwa na kuchapishwa ili iweze kumfaidi mtumiaji. Kamusi ni kitabu cha marejeleo na huwa kimbilio la watumiaji wengi ambao wametatizika na neno au dhana fulani ili kupata ufafanuzi zaidi. Kwa msingi huu kamusi inapaswa kuepuka utata wowote ambao huenda ukawaelekeza watumiaji wayo isivyofaa.

Iwapo urejeleano umefanywa kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya miundomedio huweza kuwafaa watumiaji wa kamusi kwa namna moja au nyingine kama tulivyoona. Hata hivyo, iwapo urejeleano haukuegemezwa kwenye mihimili ya nadharia huenda ukawa na athari hasi kwa watumiaji. Urejeleano wa aina hii huenda ukawatatiza au hata kuwapotosha watumiaji wa kamusi. Hebu tuone baadhi ya athari hasi zinazojitokeza katika kamusi zilizochanganuliwa kutokana na matumizi yasiyofaa ya urejeleano.

4.1.2.2.1 Athari Hasi katika Taarifa za Kisarufi

Kama ilivyo desturi ya kamusi za lugha, kamusi zote tatu zilizochanganuliwa zimeingiza taarifa nyingi za kisarufi katika vidahizo husika. Taarifa za kisarufi zilizoingizwa ni kama vile kategoria za maneno, ngeli za nomino, wingi wa nomino, na uelekezi wa vitenzi. Taarifa hizi, hasa kategoria za maneno na aina za ngeli, zilizo katika vidahizo ambavyo ni vyanzo vya urejeleano na vile ambavyo ni anwani za urejeleano, aghalabu huweza kumkanganya mtumiaji

wa kamusi iwapo hazilingani kwa namna inayotarajiwa. Zifuatazo ni baadhi ya aina za athari za kisarufi zinazojitokeza katika kamusi zilizochanganuliwa.

4.1.2.2.1.1 Athari Hasi kutokana na Kubadilisha Kategoria ya neno

Watumiaji wa kamusi hukanganyika pale ambapo watunzi wa kamusi wameiwasilisha kategoria ya neno tofauti na inavyotarajiwa katika vidahizo vinavyohusiana. Kama tulivyoona, neno moja linaweza kuwa na tofauti ndogo za kimaendelezo na hivyo kuzalisha vibadala. Kwa kawaida, vibadala huwa katika kategoria sawa ya maneno. Vilevile, maneno ambayo ni visawe bila shaka yatakuwa katika kategoria moja ya maneno. Kwa mfano, katika kuvishughulikia vibadala na visawe, iwapo kategoria ya kidahizo kilicho chanzo cha urejeleano ni nomino, inatarajiwa kuwa kidahizo katika anwani ya urejeleano ni nomino vilevile, isipokuwa pale ambapo taarifa zinazokusudiwa ni za ziada. Hata hivyo, kuna baadhi ya vibadala na visawe katika kamusi zilizochanganuliwa vilivyobadilishiwa kategoria. Hebu tuone mifano ifuatayo:

Mfano 3:

Kutoka kwa vidahizo **baku** (KKK: 59) na **sherehi** (KEK: 624) ambavyo ni vitenzi, mtumiaji wa kamusi anaelekezwa kutazama maneno **baka**¹ (KKK: 58) na **sherehe**² (KEK: 624) mtawalia, ambayo ni nomino. Ikumbukwe kuwa **baka** na **baku**, na **sherehi** na **sherehe** ni vibadala hivyo bila shaka vinapaswa kuwa katika kategoria moja ya neno. Hali kama hii inapotokea inamweka mtumiaji wa kamusi katika njia panda asijue kategoria ya kweli ya neno hili ni ipi.

4.1.2.2.1.2 Athari Hasi kutokana na Kubadilisha Ngeli za maneno

Kuna baadhi ya nomino ambazo zina vibadala na visawe. Mara nyingi maumbo ya nomino hizi huwa katika ngeli ile ile. Kwa mfano, ni kawaida kuwa visawe *ndovu* na *tembo*, ambavyo vinamrejelea mnyama, vitakuwa katika ngeli sawa ya *a-/wa-*. Hata hivyo, kuna nomino nyingine kama hizi ambazo zimewekwa katika ngeli tofauti wakati ambapo zinastahili kuingizwa katika ngeli moja. Hili linapotokea mtumiaji wa kamusi bila shaka atachanganyikiwa na kushindwa aitumie ngeli ipi. Hebu tuone mfano ufuatao.

Mfano 4:

Katika *Kamusi Elezi ya Kiswahili*, urejeleano umetumiwa katika vibadala **Disemba** na **Desemba**. Hata hivyo, ukiangalia kwa makini utaona maneno haya yamepewa ngeli tofauti; *Disemba (i-)* na *Desemba (i-/zi)*. Bila shaka, mtumiaji atajipata katika njiapanda hapa asijue ngeli hasa ya mwezi huu ni ipi.

4.1.2.2.2 Athari Hasi kutokana na Uainishaji Potovu wa Vibadala na

Visawe

Wakati mwingine, mwanafunzi wa Kiswahili anaweza kuambiwa avitaje vibadala au visawe vya maneno fulani na kisha akataja visawe kuwa vibadala na vibadala kuwa visawe. Katika Sura ya Pili, tumeonesha utaratibu uliotumiwa na watunzi wa kamusi zilizochanganuliwa katika kuainisha visawe na vibadala. Katika kuainisha vibadala, wametumia neno **pia** kuonesha namna tofauti ya kukiendeleza kidahizo fulani. Visawe vimeorodheshwa katika

sehemu ya mwisho ya kila kitomeo. Aghalabu, kuna sehemu ambapo maneno ambayo ni vidadala yamesawiriwa kama visawe na yale ambayo ni visawe kusawiriwa kama vidadala. Mfano wa kosa hili ni wazi pale ambapo watunzi wanatumia utaratibu wa kuviingiza vidadala katika kuviingiza visawe, na vilevile kutumia utaratibu wa kuviingiza visawe katika kuviingiza vidadala. Hali kama hii inapotokea, aghalabu humkanganya na humpotosha mtumiaji wa kamusi ambaye huenda akasema kidadala cha neno fulani ni kisawe au kisawe ni kidadala. Hebu tuone mifano ifuatayo:

Mfano 5:

tochi pia **kurunzi** (KKK: 1009); **wakala** pia **ajenti** (KKK: 1165);
hewaukaa pia **kabonimonoksaidi** (KKK: 296); **hudhurisho** pia
wasilisho (KKK: 307)

Bila shaka, jozi hizi za maneno ni visawe bali sio vidadala. Kwa msingi huu basi, matumizi ya neno **pia** hayafai. Pia, maneno hayo yanayofuata neno **pia**, yaani **kurunzi**, **ajenti**, **kabonimonoksaidi** na **wasilisho**, hayangekuwa pahali pale bali yangeingizwa baada ya fasili kama ulivyo utaratibu wa kuviingiza visawe katika kamusi hizi. Vinginevyo, utaratibu huu utawapotosha watumiaji wa kamusi hizi ambao wamezipitia sehemu za utangulizi za kamusi hizi kwani huenda wakafikiri kuwa maneno haya ni vidadala jambo ambalo siyo.

Hebu tuone mfano ufuatao ambapo kidadala kimeingizwa katika kamusi kwa kuzingatia mtindo wa visawe.

Mfano 6:

mafa /mafa/ **pia mava** ... (KKS: 303)

mava /mava/ *nm (-) [ya-]* ... ; **mafa**. (KKS: 323)

Bila shaka, maneno **mafa** na **mava** ni vibadala bali sio visawe. Katika mfano huu, tunaona kuwa kwenye kidahizo **mava**, KKS imekiingiza kibadala **mafa** kwa kuzingatia mtindo wa kamusi hii wa kuviingiza visawe, jambo ambalo linaweza kuchangia ufasiri usiofaa kuwa **mafa** ni kisawe cha **mava** na hivyo kumfanya mtumiaji wa kamusi hii kupotoka.

4.1.2.2.3 Athari Hasi kutokana na Urejeleano Uliokufa

Athari nyingine hasi inayoweza kumfika mtumiaji wa kamusi inatokana na urejeleano uliokufa. Katika Sura ya Pili tumeeleza maana ya urejeleano uliokufa kama ambapo mtunzi wa kamusi anamwelekeza mtumiaji wa kamusi kutoka kwenye kidahizo ambacho ni chanzo cha urejeleano, kutazama kidahizo ambacho ni anwani ya urejeleano ambacho hakikuingizwa kwenye kamusi. Katika Sura ya Pili tulitoa mifano ya urejeleano kama huu. Hebu tutazame mifano hii na kuona athari inayojitokeza:

Mfano 7:

chudere taz. **chudere** (KKK: 145), **horwaho!** taz. **holwaho!**, **ging'ingi** taz. **kiningi** (KKK: 252), (KKK: 305), **kalab!** taz. **kelb!** (KKK: 366), **matafuni** taz. **vitafunwa** (KKK: 593), na **molekyuli** taz. **molekuli** (KKK: 683); **ujalali**

taz. **ujalalati** (KKK: 1072), **ujalati** taz. **ujalalati** (KKK: 1072), **chwale** taz. **chuwale** (KEK: 89), **degle** taz. **daga** (KEK: 98), **dengrizi** taz. **dangirizi** (KEK: 99), **harusi** taz, **arusi** (KEK: 187); **mumunyika** taz. **fyonzeka** (KEK: 500) **nyasa** taz. **uwasa** (KEK: 539); **nyie** taz, **nyinyi** (KEK: 540), **shupatu** taz. **supatu** (KEK: 631), **sio²** taz. **siyo** (KEK: 639), **stua** taz. **shitua** (KEK: 649).

Katika mifano hii, maneno *chaudere, holwaho!, kiningi, kelb!, vitafunwa, molekuli, ujalalati, chuwale, daga, dangirizi, arusi, fyonzeka, uwasa, nyinyi, supatu, siyo*, na *shtua*, ambayo yanatarajiwa kuwa anwani za urejeleano, hayakuingizwa kwenye kamusi. Kwa hakika, urejeleano hufanya kazi kama mfumo wa simu. Iwapo utampigia simu mtu na awe hapatikani bila shaka hautakuwa umefanikiwa kwa kuwa lengo lako la kupiga simu halitakuwa limetimia. Mtumiaji wa kamusi hufikiria amedanganywa kwa kuwa amepewa ahadi ambayo haikutimizwa. Mwishowe, mtumiaji huyu wa kamusi hatapata kile ambacho alikuwa akikitafuta licha ya kuelekezwa eneo fulani.

4.1.2.2.4 Athari Hasi kutokana na Urejeleano Mzunguko

Katika Sura ya Pili, dhana ya urejeleano mzunguko imeelezwa kama pale ambapo mtumiaji huelekezwa kutoka kwenye chanzo cha urejeleano kukitazama kidahizo fulani, yaani anwani ya urejeleano, ili kupata taarifa, na anapofika pale anaelekezwa tena kurudi pale alipoanzia bila kupata anachokitafuta. Hebu tazama mifano hii miwili kutoka *Kamusi Kuu ya Kiswahili*:

Mfano 8:

ngeo taz. **ngeu**¹ (KKK: 792); **ngeu**¹ taz. **ngeo** (KKK: 793)

afueni taz. **ahueni** (KKK:12); **ahueni** taz. **afueni** (KKK:15)

Kutokana na mifano hii, mtumiaji wa kamusi hatakuwa amefaidika kwa vyovyote vile kwani, kando na ishara ya urejeleano, hakuna taarifa zozote zilizoingizwa katika vidahizo hivi. Kwa kweli, vidahizo vyote vimepewa hadhi moja ya chanzo cha urejeleano, kwa kuwa hata kile kidahizo ambacho mtumiaji wa kamusi anatarajia kiwe anwani ya urejeleano hakikupewa sifa zinazokitambulisha kuwa anwani ya urejeleano. Ikumbukwe kwamba sifa kuu ya anwani ya urejeleano ni kuwepo kwa taarifa inayotarajiwa kulingana na chanzo cha urejeleano. Bila shaka mtumiaji wa kamusi hatakuwa amefaidika kwa vyovyote vile licha ya kuzungushwa.

4.1.2.2.5 Athari Hasi kutokana na Urejeleano katika Kidahizo kilekile

Watunzi pia huweza kufanya makosa ya kukitumia kidahizo kimoja kuwa chanzo cha urejeleano na anwani ya urejeleano wakati uleule. Kwa namna hii, urejeshaji hufanywa kwenye kidahizo kile kile. Hebu tutazame mifano hii:

Mfano 9:

jahira taz. **jahira** (KKK: 326)

mshereheshi taz. **mshereheshi** (KKK: 705)

Ukiangalia mifano hii miwili, utaona kuwa vyanzo vya urejeleano ni **jahira** na **mshereheshi** mtawalia. Vilevile, ukiangalia anwani za urejeleano ambazo mtumiaji wa kamusi anaelekezwa kuzitazama ili kupata taarifa zaidi utagundua kuwa ni vidahizo vilevile, yaani **jahira** na **mshereheshi** mtawalia. Hii inamaanisha kuwa mtumiaji hatatoka palepale na hivyo hatapata taarifa zozote alizozikusudia na hivyo kwake itakuwa ni kama hakuwa na kamusi.

4.1.2.2.6 Athari Hasi kutokana na Urejeleano Usiobainisha Anwani

Mwafaka ya Urejeleano

Katika uhalisia wa maisha, maelekezo sahihi humwezesha mtu kufika alikotarajia na kupata alichokikusudia kwa urahisi. Hebu fikiria iwapo mtu ataelekezwa kufika katika jengo fulani lenye ofisi nyingi na huku mtu huyu alihitaji kuingia mojawapo ya ofisi hizo. Bila shaka atataabika asipoelekezwa katika ofisi mahususi, na huenda akabisha takribani ofisi zote kabla ya kupata aliyoikusudia. Vivyo hivyo, kuna baadhi ya vidahizo ambavyo ni homonimu, na watunzi wamevibainisha kwa vipeo kama vile 1, 2 na 3, kwa mfano *tembo*¹ na *tembo*². Iwapo mtumiaji wa kamusi hataelekezwa kutoka katika chanzo cha urejeleano kwenda kwenye anwani mahususi ya urejeleano, bila shaka atakanganyika na huenda asipate alichokitarajia, au vinginevyo akaichukulia anwani iliyo ya kwanza kuwa ndiyo sahihi wakati ambapo siyo, au akaachwa kubahatisha anwani ambayo ni sahihi. Hebu tutazame mifano ifuatayo:

Mfano 10:

nishaa² taz. **wanga** (KKK: 799); **kuges**i taz. **kikuku** (KKK: 517); **dhima**² taz. **kazi** (KEK: 103)

Unapoyatafuta maneno **wanga**, **kikuku** na **kazi** kama tunavyoelekezwa na vyanzo vya urejeleano, utagundua kuwa yameingizwa kama homonimu, yaani **wanga**¹, **wanga**², **wanga**³ na **wanga**⁴; **kikuku**¹, **kikuku**², **kikuku**³, **kikuku**⁴, na **kikuku**⁵; na **kazi**¹, **kazi**², **kazi**³, na **kazi**⁴ mtawalia. Bila shaka, mtumiaji wa kamusi anapofika katika anwani kama hizi atachanganyikiwa kabisa na kubaki akibahatisha anwani iliyokusudiwa. Hali kama hii huenda ikamwacha yule mtumiaji akiichukua dhana ambayo siyo.

4.1.2.2.7 Athari Hasi kutokana na Urejeleano wa Upande Mmoja

Urejeleano ni kama mfumo wa simu. Haijalishi ni upande upi mtumiaji wa kamusi anapoanzia, iwapo ataanzia katika neno fulani ni sharti aelekezwe palipo lile jingine iwapo maneno hayo yana uhusiano fulani. Kwa mfano, iwapo yuko katika kidahizo X, na aelekezwe kutazama kidahizo Y, ni sharti anapofika katika Y auone uhusiano huo katika X. Ikiwa hivyo, iwapo kuna watumiaji wawili, mmoja atafute neno X na mwingine atafute neno Y, bila shaka kila mmoja wao ataelezwa kuwa maneno hayo mawili yana uhusiano. Iwapo katika kidahizo kimoja kile kingine hakikutajwa kwa vyovyote vile, basi kuna uwezekano kuwa aliyelitafuta neno hilo hatapata kujua kuwa maneno yale yana uhusiano wowote. Katika kamusi zilizochanganuliwa kuna mifano

chungu nzima ambapo neno moja katika mfumo kama huu halikutajwa. Hebu tuone baadhi ya mifano hii:

Mfano 11:

hozai taz. **nabii** (KKK: 306); **ihmali** taz. **uzembe** (KKK: 314); **hudhurisho** pia **wasilisho** (KKK: 307); **injinia** nm [...]; **mhandisi** (KEK: 201); **mhandisi** nm [...]; (KEK: 431)

Katika anwani za urejeleano **nabii**, **uzembe** na **mhandisi** mtawalia, maneno **hozai**, **ihmali** na **injinia** hayakutajwa. Hii inamaanisha kuwa mtumiaji wa kamusi anayelitafuta neno **hozai** hatajua kuwa neno hili lina uhusiano wowote na neno **nabii**, yule anayetafuta neno **uzembe** hatajua kuwa neno **ihmali** ni kisawe cha **uzembe** kwani katika kidahizo **uzembe** neno **ihmali** halikutajwa. Vilevile, yule anayetafuta neno **mhandisi** hatajua kuwa neno hili lina kisawe **injinia** kwani neno **injinia** halikutajwa katika kidahizo **mhandisi**. Pia, kando na kuwa neno **pia** halistahili kutumiwa katika kitomeo **hudhurisho**, neno **hudhurisho** halikutajwa katika kidahizo **wasilisho**. Hivyo, mtumiaji wa kamusi anayetafuta neno **wasilisho** hatapata fursa ya kujua kuwa neno hili lina kisawe **hudhurisho**. Hali hizi zinamnyima mtumiaji wa kamusi wa upande mmoja nafasi ya kupanua msamiati wake.

Kama ilivyoelezwa katika Sura ya Kwanza, ni *Kamusi Kuu ya Kiswahili* tu ambayo imetumia urejeleano kuonesha uhusiano wa vinyume vya maneno. Hata hivyo, watunzi wa kamusi hii walionesha uhusiano huu katika upande

mmoja tu. Kwa mfano, wameonesha kuwa kitenzi X kina kinyume Y, lakini katika kitenzi Y hawajasema iwapo kina X kama kinyume chake. Tatizo linalojitokeza ni kwamba anayefaidika na taarifa zaidi ni yule mtumiaji aliyekitafuta kitenzi X kwani atajua kinyume cha kitenzi kile. Yule anayetafuta kitenzi Y, hatajua iwapo X ni kinyume kwani taarifa hii haikuingizwa pale. Hebu tuone mifano ifuatayo.

Mfano 12:

Mtumiaji wa kamusi hii anayetafuta maana za maneno **haraka** (KKK: 284), **furahi** (KKK: 231) na **umaskini** (KKK: 1092) atapata taarifa zaidi kuhusu vinyume vya maneno hayo. Kwa mfano, ameelekezwa kuwa kinyume cha **haraka** ni *asteaste* na *polepole*, kinyume cha kitenzi **furahi** ni *chukia*, *nuna* na *kasirika*, na vinyume vya nomino **umaskini** ni *ukwasi* na *utajiri*. Hata hivyo, vinyume vyote vilivyoingizwa katika mifano hii mitatu havikutolewa vinyume pale vilipoingizwa kama vidahizo. Hii inamaanisha kuwa mtumiaji wa kamusi ambaye anatafuta maana za maneno *polepole* (KKK: 864) na *asteaste* (KKK: 44) hatapata taarifa zaidi kuhusu **haraka** kuwa kinyume cha maneno hayo. Vilevile, yule anayetafuta maana za maneno **ukwasi** (KKK: 1086) na **utajiri** (KKK: 1129) hatajua kuwa kinyume cha maneno haya ni **umaskini**, na anayetafuta maana za maneno **chukia** (KKK: 146) **kasirika** (KKK: 384) na **nuna** (KKK: 804) pia atakosa taarifa zaidi kuhusu **furahi** kuwa kinyume cha maneno haya.

4.2 Mapendekezo ya Kuboresha Urejeleano katika Kamusi za Kiswahili za Lugha Moja

Katika sehemu hii tunatoa mapendekezo ya kuboresha urejeleano katika kamusi za Kiswahili za lugha moja. Mapendekezo haya yanatokana na matokeo ya utafiti wetu. Ni matumaini yetu kuwa mapendekezo haya yakizingatiwa na watunzi na wachapishaji wa kamusi za Kiswahili kutakuwa na ukuruba katika kamusi zote kuhusu matumizi ya urejeleano. Pia, athari hasi tulizozibainisha katika sura hii zitaepukwa. Kwa jumla, iwapo mapendekezo haya yatazingatiwa bila shaka kamusi zitakazochapishwa baadaye zitakuwa bora zaidi zikilinganishwa na zile zilizochanganuliwa.

4.2.1 Msingi wa Urejeleano uwe Nadharia ya Miundomedio

Kama ilivyobainika katika utafiti huu, takribani athari zote hasi kuhusu urejeleano zinatokana na kutozingatia mihimili ya nadharia ya miundomedio kama inavyoelekezwa na waasisi wake. Hebu tuone jinsi baadhi ya mihimili hiyo inavyoelekeza na jinsi ambavyo inaweza kuzingatiwa ili kuepuka athari tulizozibainisha.

Nadharia ya miundomedio inasisitiza kuwepo kwa chanzo cha urejeleano, ishara ya urejeleano na anwani ya urejeleano. Hii ni mihimili mitatu ya nadharia ya miundomedio ambayo inaonesha mfumo kamili wa urejeleano. Iwapo pana chanzo cha urejeleano ni sharti pawe na anwani ya urejeleano inayoashiriwa kupitia ishara ya urejeleano. Tayari tumekwisha kuona athari

hasi zinazotokana na mfumo huu pale ambapo kuna chanzo cha urejeleano huku, aidha anwani ya urejeleano haikuingizwa, kile tulichokiita urejeleano uliokufa, au anwani mahususi haikuoneshwa, hasa pale kidahizo kilicho anwani ya urejeleano kimeingizwa kama polisemi.

Ili kuepukana na tatizo kama hili tunapendekeza, katika mchakato mzima wa uchapishaji, waandishi na wahariri wachukue nafasi ya mtumiaji wa kamusi na kufuata maelekezo wanayoyatoa kwa mtumiaji wa kamusi kupitia ishara ya urejeleano. Kwa mfano, pale ambapo wanamwelekeza mtumiaji wa kamusi atazame kidahizo fulani, wafanye hivyo wenyewe na kuhakikisha kuwa kile wanachomwaahidi mtumiaji ki pale. Wakifanya hivi bila shaka watabaini iwapo wamemwelekeza mtumiaji wa kamusi katika anwani mwafaka na iwapo taarifa walizozikusudia pale zimeingizwa au la. Kwa namna hii wataepuka kuwepo kwa urejeleano uliokufa, urejeleano mzunguko na urejeleano kwenye kidahizo kilekile.

4.2.2 Kuepuka Uradidi

Tumshaona kupitia wanaleskografia mbalimbali kuwa mojawapo ya dhima za kimsingi za urejeleano ni kuepuka uradidi wa maelezo ambayo tayari yanaweza kupatikana katika kidahizo kingine na hivyo kupunguza nafasi inayotumiwa na maelezo hayo. Kwa mfano, tumeona maelezo yameingizwa katika vibadala, visawe vya moja kwa moja, na hata katika maneno mbalimbali yanayoviunda vifungu vya maneno, kama vile methali. Pia, tumeona hata

michoro ileile ikirudiwa katika visawe vya moja kwa moja. Hali hii imechangia ukubwa wa kamusi, hatua ambayo inaathiri moja kwa moja gharama ya uchapishaji.

Ili kuepuka uradidi huu na hivyo kupunguza gharama ya uchapishaji, ni pendekezo letu kwamba watunzi na wachapishaji wazingatie maelekezo ya wanaleksikografia na kuingiza fasili katika kidahizo kilicho anwani ya urejeleano tu na kumwelekeza mtumiaji ilipo maana hiyo. Pia, waepuke kuingiza michoro katika vidadala na visawe vya moja kwa moja kwani mchoro ni uleule.

4.2.3 Kuwe na Urejeleano wa Pande zote mbili

Kama tulivyokwisha kuonesha, urejeleano ni kama mfumo wa simu, pale ambapo watu wawili wanaweza kupigiana simu. Mtu A anaweza kumpigia Mtu B simu, na Mtu B anaweza kumpigia Mtu A simu. Itakuwa vigumu kuwa na mawasiliano mwafaka iwapo ni mtu mmoja tu anaweza kupiga simu na yule mwingine hawezi. Tumeona pia kuna sehemu nyingi ambapo mtumiaji mmoja wa kamusi anayetafuta neno fulani atafaidika zaidi akilinganishwa na mwingine anayetafuta neno jingine iwapo maneno yote yana uhusiano kama ule wa vidadala, visawe, vinyume au wingi na umoja wa nomino.

Ili kuwafaidi watumiaji kama hawa wote, tunapendekeza urejeleano uhusishe maneno yote mawili yanayohusiana kutoka kila upande. Kwa mfano, mtumiaji

wa kamusi anayetafuta neno *ndovu* anapaswa kufahamishwa kuwa lina kisawe *tembo*, na vilevile, yule anayetafuta neno *tembo* anastahili kuoneshwa neno *ndovu* ambalo ni kisawe cha neno hilo. Kwa kufanya hivi, mtumiaji anayetafuta neno *ndovu* na yule anayetafuta neno *tembo* wote watakuwa na taarifa sawa.

4.2.4 Kuwe na Utafiti Mwafaka kuhusu Uhusiano wa Maneno

Kama tulivyoona katika Sura ya Kwanza ya tasnifu hii, maneno ya lugha huhusiana kwa namna moja au nyingine. Mojawapo ya dhima za urejeleano ni kuonesha uhusiano uliopo baina ya maneno ya lugha. Maneno ya lugha yanaweza kuwa na uhusiano kama ule wa vidadala, visawe na antonimu.

Tumeona athari zinazoweza kujitokeza kutokana na kutoelewa uhusiano mwafaka baina ya maneno ya lugha. Kwa mfano, tumeona pale ambapo watunzi wa kamusi zilizochanganuliwa wamevibainisha visawe kama vidadala, na vidadala kama visawe. Kwa kawaida, hili huenda lilitokana si na kutojua tofauti ya vidadala na visawe hivyo bali kwa sababu ya kutozingatia utaratibu walioeleza wa kuvibainisha. Kwa mfano, wameeleza kuwa vidadala vinabainishwa kwa neno **pia** ilhali visawe vinaorodheshwa baada ya fasili mwishoni mwa vitomeo.

Ili kuepuka hali kama hii tunapendekeza watunzi na wachapishaji wazingatie kwa makini utaratibu wanaombainishia mtumiaji wa kamusi. Iwapo neno ni

kisawe au kibadala wahakikishe kuwa limeingizwa kwa kuzingatia utaratibu walioubainisha, yaani wawe waaminifu kwa maelekezo yao wenyewe. Kwa namna hii ule utata unaojitokeza kwa mtumiaji wa kamusi wa kuvitambua visawe na vidadala utaepukwa.

4.2.5 Kuwe na Umakinifu zaidi katika Udurusu na Uhariri wa Miswada

Katika Sura ya Kwanza tumewaona Gouws na Prinsloo (2005) wakimnukuu Wiegand anayesema kuwa kamusi ni chombo kinachobeba matini za aina mbalimbali ambazo zinahusiana kwa namna moja au nyingine. Kauli hii inaonesha kuwa kamusi ni kitabu changamano na hivyo kinastahili kushughulikiwa kwa umakinifu unaostahili.

Baadhi ya athari hasi tulizozibainisha katika kamusi zilizochanganuliwa katika tasnifu hii zinaashiria, kwa kiwango fulani, hali ambapo watunzi na wahariri hawakuyamakinikia masuala haya kikamilifu, kwa mfano pale ambapo maneno yameainishwa katika ngeli tofauti na aina za maneno tofauti. Ni maoni yetu kwamba iwapo kulikuwa na umakinifu unaotakikana, hali kama hizi zingegunduliwa mapema katika mchakato wa uchapishaji na hivyo kuepukwa.

Kutokana na hali hii tunapendekeza mashirika ya uchapishaji yasisitize utunzi wa kamusi ufanywe na wataalamu wa lugha. Wahariri wawe pia wanaelewa sanaa ya utunzi wa kamusi ili waweze kuwaelekeza watunzi pale wanapopotoka kwani ni vigumu kutoa maelekezo ya kufika pahali ambapo

hupajui. Pia, kazi changamano kama hii inahitaji wahusika kadhaa kuvishughulikia vipengele mbalimbali katika hatua tofauti za mchakato mzima wa uchapishaji. Kwa namna hii, iwapo kuna kosa ambalo halikupatikana na mhusika mmoja katika hatua ya kwanza, basi yule mwingine atalipata katika hatua inayofuata.

4.2.6 Kuwe na Usawazishaji wa Vipengele vyote kabla ya Uchapaji wa Kamusi

Mara nyingi wataalamu wa kamusi hupewa herufi mbalimbali za kamusi kuzitafutia maneno na kuyasawidi. Hii inamaanisha kuwa kila mtaalamu atayashughulika maneno ya herufi yake kikamilifu, ikiwa ni pamoja na kuyatolea fasili na kuyaandamanisha na vipengele vingine vyote ambavyo huunda kitomeo kamilifu, ikiwa ni pamoja na vibadala, visawe, nahau, misemo na methali zinazoandamana na neno husika. Aghalabu, uradidi mwingi unaojitokeza katika kamusi ambazo zilichanganuliwa unatokana na hali hii, pale ambapo kazi za wahusika wote zinaletwa pamoja na kujumuishwa. Ikumbukwe kuwa mahusiano ya baadhi ya maneno yanapatikana nje ya mipaka ya herufi inayoanzisha neno fulani. Kwa mfano, visawe *ndovu* na *tembo*, *nyati* na *mbogo*, na *tarakilishi* na *kompyuta* vinapatikana katika herufi tofauti. Hivyo, iwapo mtunzi mmoja alishughulikia maneno yanayoanza kwa herufi /n/ atashughulikia neno *ndovu*. Mwingine anayeshughulikia maneno yanayoanza kwa herufi /t/ atashughulikia neno *tembo* ambalo ni kisawe cha *ndovu*. Hebu fikiria iwapo katika kidahizo *ndovu* yule mtunzi aliingiza methali

zote zinazoambatana na neno hilo, pamoja na mchoro, na yule aliyeshughulikia kidahizo ndovu akafanya vivyo hivyo. Iwapo hakutakuwa na kikao cha kuhusisha uhusiano kati ya maneno haya bila shaka kutakuwa na uradidi usiotakikana.

Kutokana na hali hii tunapendekeza kuwepo kwa upitiaji wa mswada mzima kwa pamoja na wahusika wote na kusawazisha vipengele vyote inavyotakikana. Katika kufanya hivyo, wataalamu hawa watauona uradidi huu na hatimaye kujaribu kuuepuka. Pia, katika kufanya hivyo, kwa kuwa watu wote hawatoshani, na kuegemea ukweli kwamba lugha ya Kiswahili ina tanzu nyingi ambazo zina wapenzi waliozizamia, wataweza kukosoana panapostahili na hivyo kuhakikisha kuwa kamusi watakayoitoa ina ubora wa juu zaidi.

4.3 Hitimisho

Katika sura hii, tumeangazia athari mbalimbali ambazo zinaweza kutokana na kutozingatia urejeleano inavyotakikana. Tumeziainisha athari hizi kama zile zinazowaathiri wachapishaji na zile zinazowaathiri watumiaji wa kamusi. Kupitia mifano mbalimbali tumeweza kuonesha jinsi ambavyo wahusika hawa wataathirika. Kwa sababu ya kutozingatia mihimili ya nadharia ya miundomedio tumeona kuwa kuna uradidi mwingi wa vipengele vilevile kwenye kamusi zilizochanganuliwa, jambo ambalo linaongeza kurasa za kamusi na hivyo kuathiri moja kwa moja gharama ya uchapishaji. Gharama hii hatimaye hupitishwa kwa watumiaji wa kamusi husika. Kwa kiwango fulani, hasa kwa watumiaji wasiokuwa na umilisi wa juu wa lugha ya Kiswahili,

huenda wakaona kana kwamba urejeleano hufanya kamusi kama hizi, ambazo ni za watumiaji wa kiwango cha juu, kuwa changamano. Huenda ingekuwa bora kwao kama kipengele hiki hakingetumiwa na hivyo kuwasilisha dhana zote pamoja na uradidi unaohusika. Hata hivyo, utaratibu kama huu, kama tulivyokwisha kuona utakuwa unakinzana na mihimili ya nadharia ya miundomedio na pia kuwaongezea wachapishaji gharama ya uchapishaji ambayo itapitishwa kwao kama watumiaji.

Tumeona kuwa kupitia uwasilishaji usiofaa wa urejeleano, mtumiaji wa kamusi huenda akatatizika na kukanganyika hasa pale vipengele vya lugha vinasawiriwa visivyo. Kutokana na kutotumia utaratibu sawa katika kuvishughulikia vipengele vinavyoweza kuhusishwa kupitia urejeleano tumeona kuwa kuna sehemu ambapo mtumiaji wa kamusi anasikia kusalitika kwa kukosa taarifa alizoahidiwa au kuzungushwa na hatimaye kukosa alichohadiwa. Pia, tumeona kuwa kuna baadhi ya watumiaji wa kamusi ambao watafaidika zaidi kuliko wengine kutegemea kile kidahizo ambacho kitachukuliwa kama chanzo cha urejeleano.

Pia, kuzingatia matokeo ya utafiti wetu tumetoa mapendekezo mbalimbali ambayo kwa maoni yetu, iwapo yatazingatiwa na watunzi na wachapishaji wa kamusi, kamusi ambazo zitachapishwa baadaye zikuwa bora zaidi kwa manufaa ya wachapishaji na watumiaji. Tumefanya hivi kwa kuirejelea athari husika na kisha kupendekeza kile ambacho kinafaa kufanywa ili kuiepuka.

SURA YA TANO

MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

5.0 Utangulizi

Tasnifu hii imeshughulikia kwa kina kipengele cha urejeleano katika kamusi za Kiswahili za lugha moja. Tumezichanganua kamusi tatu (*Kamusi Kuu ya Kiswahili, Kamusi ya Kiswahili Sanifu na Kamusi Elezi ya Kiswahili*) na kupitia mifano iliyonukuliwa moja kwa moja kutoka katika kamusi hizi tukaona jinsi ambavyo watunzi wa kamusi hizi walivyokishughulikia kipengele cha urejeleano.

5.1 Muhtasari wa Utafiti

Katika Sura ya Kwanza tumeeleza kwa kina kuhusu usuli wa mada ya utafiti wetu, malengo, sababu zetu za kuichagua mada hiyo, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa na wengine kuhusu kipengele cha urejeleano na tukaeleza kwa mapana kuhusu nadharia ya miundomedio (mediostuctures) ambayo iliuelekeza utafiti wetu, pamoja na mbinu zilizotumiwa katika utafiti huu.

Katika Sura ya Pili tumevibainisha vipengele mbalimbali ambavyo vinaweza kuhusishwa kupitia urejeleano, kama vile vibadala, visawe, umoja na wingi wa

nomino, vinyume, nahau, misemo na methali. Pia, tumezishughulikia dhana muhimu zinazotumiwa katika urejeleano, kama vile chanzo cha urejeleano, anwani ya urejeleano, alama ya urejeleano, uhusiano wa kiurejeleano, urejeleano mzunguko, na urejeleano uliokufa.

Katika Sura ya Tatu, kwa kunakili mifano moja kwa moja katika kamusi teule, tumeonesha jinsi ambavyo watunzi wa kamusi teule walivyovihusisha vipengele hivyo. Katika kufanya hivyo tumeona jinsi ambavyo watunzi wote walivyoshabihiana na pia kutofautiana katika namna walivyokishughulikia kipengele cha urejeleano. Tumeonesha kuwa kuna sehemu ambapo wameelekezwa na mihimili ya nadharia na mapendekezo ya wataalamu kuhusu urejeleano, na pia kuna pale ambapo hawakuzingatia maelekezo hayo.

Katika Sura ya Nne tumeonesha athari ya urejeleano katika kamusi teule na mapendekezo ya kuboresha urejeleano katika kamusi za Kiswahili za lugha moja. Tumeona kuwa athari hizi zinaweza kuwa hasi au chanya kutegemea iwapo watunzi na wachapishaji walielekezwa na nadharia ya miundomedio au la. Pale ambapo walielekezwa na nadharia, athari zinakuwa chanya na pale ambapo hawakuelekezwa na nadharia, athari zinakuwa hasi. Pia, tumeona kuwa athari hizi zinaweza kuwa kwa watunzi wa kamusi na watumiaji wa kamusi. Katika sura hii pia tumetoa mapendekezo kwa kila athari hasi tuliyoionesha, ambayo iwapo yatazingatiwa basi tutapata kamusi bora zaidi zitakazochapishwa baadaye.

5.2 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulipania kuchunguza jinsi kipengele cha urejeleano kilivyotumiwa katika kamusi tatu za Kiswahili za lugha moja zilizoteuliwa (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu, Kamusi Kuu ya Kiswahili, Kamusi Elezi ya Kiswahili*), ikiwa ni pamoja na kubainisha vipengele vya urejeleano vilivyotumiwa, kulinganisha na kulinganua matumizi ya urejeleano katika kamusi hizo, kujadili athari ya urejeleano kama ulivyotumiwa katika kamusi hizo, na hatimaye kupendekeza, kutegemea matokeo ya utafiti, namna ya kuboresha urejeleano katika kamusi za Kiswahili za lugha moja. Katika kujaribu kutimiza malengo haya, matokeo mbalimbali yaliyojadiliwa hapa chini yalibainika

5.2.1 Vipengele vya Urejeleano katika Kamusi Zilizochanganuliwa

Utafiti huu umeonesha kuwa kuna vipengele vingi ambavyo vinaweza kuhusishwa kupitia urejeleano, na kuwa kamusi zilizochanganuliwa zimevihusisha vipengele kama vile vibadala, visawe, umoja na wingi wa nomino, vinyume vya maneno, nahau, misemo na methali kupitia urejeleano. Tumeona kuwa ni *Kamusi Kuu ya Kiswahili* pekee iliyovishughulikia vinyume vya maneno. Pia, tumetaja kuwa *Oxford Advanced Learner's Dictionary 9th edition* imekishughulikia kipengele cha jinsia kupitia urejeleano, ambacho hakikushughulikiwa na watunzi wa kamusi zilizochanganuliwa.

5.2.2 Mifanano na Tofauti za Matumizi ya Urejeleano

Kupitia mifano anuwai tumeonesha mifanano na tofauti za jinsi urejeleano ulivyotumiwa na watunzi wa kamusi zote tatu zilizochanganuliwa ili kuonesha uhusiano uliopo baina ya vipengele mbalimbali katika kamusi. Tumeona kuwa watunzi wa kamusi zote tatu hawakuizingatia nadharia ya miundomedio kikamilifu na hivyo kuishia kuwa na namna tofauti za matumizi ya urejeleano. Kwa mfano, tumeona pale ambapo walielekezwa na mihimili ya nadharia hii wamefuata mkondo sawa na ulio sahihi. Pale ambapo hawakuizingatia tumeona ama wamefanana kwa kutoizingatia au kila mmoja akachukua mkondo wake mwenyewe.

Tumeona kuwa, kwa kuwa nadharia huelekeza jinsi ya kufikia hali fulani, bila shaka iwapo watunzi wangeizingatia kwa makini, kungekuwa na usawa katika jinsi walivyokishughulikia kipengele cha urejeleano katika kamusi zao na hivyo kuepuka utata tulioudhihirisha katika Sura ya Nne ya tasnifu hii.

5.2.3 Athari ya Urejeleano

Katika tasnifu hii tumewanukuu wataalamu wakisema kuwa urejeleano ni kipengele ambacho iwapo kitatumiwa vyema kitawezesha kuunda mtandao wa maneno katika kamusi ambao utamfaidi mtumiaji wa kamusi. Kwa kiwango kikubwa na kwa kutumia mifano mbalimbali tumeonesha kuwa watunzi wamefanikiwa kufanya hivyo. Hata hivyo, pia tumeona kuna sehemu nyingi ambazo kwa sababu ya kutokimakinikia kipengele cha urejeleano, mfumo huu

umechangia kuwepo kwa athari hasi mbalimbali ambazo zinamkanganya au kumpotosha mtumiaji wa kamusi.

Tumeonesha, kupitia mifano, kuwa kuna athari chanya na hasi kwa wachapishaji na watumiaji wa kamusi iwapo nadharia ya urejeleano ilizingatiwa au la. Kwa mfano, kupitia mahojiano na wataalamu wa uchapishaji tumeona kuwa ukubwa wa kitabu huchangia gharama ya uchapishaji wa kitabu. Tumeona pia pale ambapo watunzi hawakuongozwa na nadharia kuna uradidi mwingi unaotokana na kurudiarudia maelezo yale yale katika vidahizo mbalimbali hali ambayo inachangia ukubwa wa kamusi na hatimaye kuongeza gharama ya uchapishaji.

Tumbainisha kuwa pale ambapo nadharia ya miundomedio imetumiwa kama dira, athari zinakuwa chanya kwa watumiaji kwani wanapata taarifa zaidi na zilizo sahihi na bila kupoteza wakati na kubahatisha. Kwa upande mwingine utafiti huu umeonesha kuwa athari zinakuwa hasi kwa watumiaji wa kamusi pale ambapo watunzi hawakutilia maanani mihimili ya nadharia. Kutokana na hali hii tumeona shida ambazo zitamkumba mtumiaji wa kamusi ikiwemo kutojua ngeli mwafaka ya neno, iwapo maneno husika ni vibadala au visawe, na kutopata taarifa kabisa hasa pale ambapo pana urejeleano uliokufa.

5.2.4 Namna ya Kuboresha Urejeleano katika Kamusi za Kiswahili za

Lugha Moja

Katika Sura ya Nne tumezinukuu athari hasi za urejeleano zinazojitokeza katika kamusi zilizochanganuliwa na kupendekeza namna ambavyo athari hizo zinaweza kuepukwa katika kamusi za Kiswahili zitakazochapishwa baadaye. Kwa namna hii, kamusi zitakazochapishwa baadaye zitakishughulikia kipengele cha urejeleano kwa namna sawa na iliyo sahihi na hivyo basi kuhakikisha kuwa wale wanaozitumia kamusi tofauti watapata taarifa zilizo sawa.

5.3 Mapendekezo ya Utafiti

Katika kufanya utafiti wetu, tuligundua masuala yafuatayo ambayo yalikuwa nje ya mipaka ya utafiti wetu na hivyo ni maoni yetu kwamba watafiti wengine wanaweza kuyachunguza.

5.3.1 Ishara tofauti za Urejeleano

Katika Sura ya Pili tumeona kuwa watunzi wametumia ishara tofauti za urejeleano. Itakuwa bora utafiti zaidi kufanywa kuona iwapo ishara hizi tofauti zinawakanganya watumiaji wa kamusi, na iwapo panastahili kuwepo na ishara zinazofanana za urejeleano.

5.3.2 Matumizi ya Lugha Kienzo

Katika utunzi wa kamusi, lugha kienzo, yaani lugha ya mkato, ufupisho pamoja na ishara nyingi, hutumiwa ili kupunguza nafasi. Kwa kawaida matumizi haya huwa tofauti na matumizi ya lugha ya kila siku. Ni maoni yetu kwamba utafiti zaidi unahitajika kuchunguza iwapo matumizi kama haya yana athari zozote kwa watumiaji wa kamusi.

5.3.3 Uainishaji wa Homonimu na Polisemi

Katika uchanganuzi wetu wa kamusi teule tulikumbana na sehemu nyingi ambapo kamusi tofauti zimeliainisha neno fulani kama polisemi na nyingine kama homonimu. Itakuwa bora iwapo watunzi wa kamusi watafanya utafiti zaidi na kuainisha mipaka kamili ya vipengele hivi muhimu katika taaluma ya semantiki. Utafiti wa Makenge (2019) umelishughulikia suala hili kwa kina.

5.3.4 Matumizi ya Programu za Kompyuta

Kadri teknolojia inapopiga hatua, kunatokea programu mbalimbali zinazorahisisha jinsi ya kufanya mambo. Hivyo, itakuwa vizuri iwapo watunzi na wachapishaji wa kamusi za Kiswahili watawekeza katika programu ambazo zinaweza kuhusisha vipengele vya lugha kupitia urejeleano. Programu kama hizi kwa kawaida hufanya kazi vizuri iwapo zitaendeshwa na wataalamu wanaoelewa vizuri jinsi ya kuzitumia. Itakuwa vyema iwapo mashirika ya uchapishaji yatawekeze kwenye watu wenye ujuzi wa aina hii. Uzuri wa

teknolojia kama hii ni kuwa itapunguza muda wa kufanya urejeleano na pia kupunguza makosa ambayo yanatokana na ukosefu wa umakinifu na pia uchovu.

5.4 Hitimisho

Kamusi ni kitabu cha marejeleo ambacho hutumiwa na takribani kila mtu ili kupata maana za maneno au ufafanuzi zaidi wa dhana fulani. Katika sura hii tumetoa muhtasari wa utafiti tulioufanya, matokeo ya utafiti na pia kupendekeza utafiti ambao kwa maoni yetu unafaa kufanywa. Ni matumaini yetu kuwa utafiti huu utakuwa wa manufaa kwa watunzi wa kamusi za Kiswahili za lugha moja na wachapishaji kwa jumla ili kuweza kukitumia kipengele cha urejeleano inavyostahili kwa manufaa yao wenyewe na zaidi, kwa manufaa ya watumiaji lengwa wa kamusi.

MAREJELEO

- Alberts, M. (2007). *Dictionary Structures and Dictionary Making Skills*. [Power Point Presentation]. Pan South Africa Language Board (PanSALB). Soshanguve. South Africa.
- Bakhressa, K. S. (1992). *Kamusi ya Maana na Matumizi*. Nairobi: Oxford University Press.
- BAKITA. (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.
- BAKIZA. (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.
- Bergenholtz, H. and Gouws, R.H. (2012). What is Lexicography? *Lexikos* 22 (AFRILEX-reeks/series 22): 31-42.
- Chiduo, F. K., Habwe, J., Chimerah, R., Kaoneka, M. Yahaya, R. na Attas A. (2016). *Kamusi Elezi ya Kiswahili*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Geeraerts, D. (2016). Lexicography and Theories of Lexical Semantics. *The Oxford Handbook of Lexicography*. doi:10.1093/oxfordhb/9780199691630.013.32. Accessed on 20th April 2018.
- Gouws, R.H. (1998). Cross-Refencing as a Lexicographic Device. *The Lexikos* Series 8, 17–36.
- Gouws, R.H. and Prinsloo, D.J. (2005). *Principles and Practice of South African Lexicography*. Stellenbosch: Sun Press.

Grimes, E.J. (1984). *Denormalization and Cross-referencing in Theoretical Lexicography*. DMLL, Moril Hall, Cornell University.

Hornby, A. S. (2015). *Oxford Advanced Learners's Dictionary (9th edition)*. Oxford: Oxford University Press.

ITLC. (1939). *A Standard English–Swahili Dictionary*. Nairobi: Oxford University Press.

Islam, K. I., Matei, A. K. Kyovi, P. K. (2011) *Kamusi ya Watoto*. Nairobi. Oxford University Press.

ITLC. (1939). *A Standard Swahili–English Dictionary*. Nairobi: Oxford University Press.

Johnson, F. (1935). *Kamusi ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press in association with Sheldon Press.

Kiango, J. G. (1996). Usawidi wa Vitomeo vya Kamusi. Dar es Salaam. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. *Mulika* Na 23, 75-94.

Kiango, J. G. (2006). Uingizaji wa Vinyambuo-Nomino katika Kamusi za Kiswahili. Dar es Salaam. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. *Mulika* Na. 27, 60-77.

Kiango, J. G., Lodhi, A. Y. na I. Nassir. (2007). *Kamusi ya Shule za Msingi*. Nairobi: Oxford University Press.

Kiango, J. G., Lodhi, A. Y. na I. Nassir. (2016). *Kamusi Sanifu ya Msingi*. Nairobi: Oxford University Press.

- Kobia, J. M. (2015). *Kamusi Bora ya Watoto*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.
- Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods & Techniques*. New Delhi: New Age International Publishers.
- Makenge, J. A. (2019). *Utata wa Kubainisha Homonimu na Polisemi katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu na Kamusi ya Karne ya 2*. Unpublished Master's Thesis. Kenyatta University.
- Mdee, J. S. (1997). *Nadharia na Historia ya Leksikografia*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Mdee, J. S., Njogu, K. na Shafi, A. (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.
- Modiba, M. C. (2011). *A Comparative Analysis of Cross-referencing with Special Reference to Northern Sotho Monolingual Dictionary and Northern Sotho-English Bilingual Dictionaries*. Unpublished Master's Thesis. University of Limpopo. Turfloop.
- Mugenda, O. A. na Mugenda, A. G. (2003). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi. Act Press.
- Mugenda, A. G. na Mugenda, O. A. (2012). *Research Methods Dictionary*. Nairobi: Act Press.
- Ndalu, E. A. (2011). *Kamusi Angaza kwa Shule za Msingi*. Nairobi: East Africa Education Publishers Limited.

- Ndalu, E. A., Babusa, H, na Mirikau, A. S. (2014). *Kamusi Teule ya Kiswahili*. Nairobi: East Africa Education Publishers Limited.
- Nkomo, D. (2007). Some Deficiencies in the Mediostructures of Isicha zamazwi SesiNdebele. *Lexikos*. 17, 372–384.
- Nkomo, D. (2008). *Towards a Theoretical Model for LSP Lexicography in Ndebele with Special Reference to a Dictionary of Linguistic and Literary Terms*. Unpublished Master's Thesis. Stellenbosch University.
- Prinsloo, D. J. (2009). Current Lexicography Practice in Bantu with Specific Reference to the Oxford Northern Sotho School Dictionary. *International Journal of Lexicography*, Volume 22, Issue 2, 151–178.
- Siepmann, D. (2006). Collocation, Colligation and Encoding Dictionaries. Part II: Lexicographical Aspects. *International Journal of Lexicography*, Volume 19, Issue 1, 1–39.
- Snoxall, R. A. na Mshindo, H. B. (2002). *A Concise English-Swahili Dictionary*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Svensen, B. (1993). *Practical Lexicography: Principles and Methods of Dictionary-making*. New York: Oxford University Press.
- Tarp, S. (1999). Theoretical foundations of the so-called cross-reference structures. *Lexicographica*, no. 15, 114-137.
- TUKI. (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- TUKI. (2006). *English–Swahili Dictionary*. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research, Dar es Salaam University.

TUKI. (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu 3rd edition (Updated)*. Nairobi: Oxford University Press.

TUKI. (2014). *Kamusi ya Kiswahili–Kiingereza*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Wamitila, K.W. (2016). *Kamusi Pevu ya Kiswahili*. Nairobi: Vide Muwa.

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO CHA KWANZA: MIFANO ZAIDI YA DATA

Mifano zaidi ya vibadala kutoka kamusi zilizochanganuliwa

lubega; rubega

lubega /lu'beɡa/ *nm.* (Ø) {i-/zi-} aina ya uvaaji ambao nguo k.v. shuka au kitenge huvaliwa kwa kupitishwa chini ya kwapa la mkono mmoja na kufungwa fundo juu ya bega la mkono mwingine. (KKK: 549)

rubega /ru'beɡa/ *nm.* (Ø) {i-/zi-} taz. **lubega.** (KKK: 893)

lubega /lubega/ **pia rubega** / rubega/ *nm* (-) [i-/zi-] mvao wa nguo k.v.

shuka, ambao upande mmoja hupitishwa chini ya kwapa la mkono mmoja, kupitia mbele ya kifua, na upande mwingine kufungiwa juu ya bega la mkono mwingine, kupitia mgongoni. (KKS: 297)

rubega /rubega/ *nm* (-) [i-/zi-] taz. **lubega.** (KKS: 491)

lubega /lubega/ *nm*[i-zi] vazi livaliwalo kwa kupitisha kwenye kwapa

ya bega moja hadi ya juu ya bega upande mwingine wa bega. (KEK: 363)

rubega /rubega/ *nm* [i-zi] **pia lubega** vazi ambalo huvaliwa kifuani na

hupita juu ya bega moja na kuacha jingine wazi. (KEK: 599)

akina; kina

akina /a'kina/ nm. (Ø) {i-/zi-} **pia akina** neno linalotumika kutaja wingi wa watu ... (KKK: 21)

kina⁴ /kina/ kiel. **pia akina** neno linaloonesha watu wenye nasaba zinazofanana kijinsia, kiuchumi, kitabaka, kijamii ... (KKK: 445)

akina /akina/ kl **taz. kina**¹. (KKS: 9)

kina¹ /kina/ **pia akina** /akina/ kl neno la kuelezea watu wenye uhusiano wa jinsia, ukoo, ujamaa, tabia au hali ... (KKS: 237)

akina /akina/ nm (a-wa) tamshi linalotanguliziwa kundi la watu wenye fungamano moja. (KEK: 10)

kina² /kina/ nm (wa-) **pia akina 1** neno litumiwalo kutaja kundi fulani la watu kutangulia jina la kundi hilo hili kuonyesha heshima ... **2** hutumiwa kuonyesha wingi wa watu katika kundi. (KEK: 295)

loga; roga

loga /'loga/ kt. ele. **pia roga** fanyia mtu ushirikina ili kumdhuru; sihiri. (KKK: 548)

roga /'roga/ kt. ele. **pia loga** fanyia mtu ushirikina kwa lengo la kumdhuru au kuharibu mali zake; sihiri. (KKK: 891)

loga /loga/ kt ele ▣ **taz. roga**. (296)

roga /roga/ **pia loga** /loga/ kt ele dhuru kwa uchawi ... (KKS: 490)

loga /lɔga/ *kt* (ele) dhuru kwa uchawi. (KEK: 362)

roga /rɔga/ *kt* (ele) **pia loga** fanyia uchawi; athiri mtu kwa uchawi.
(KEK: 597)

kinukamito; kirukamito

kirukamito kiruka+mito /kiruka'mito/ *nm.* (vi-) {a-/wa-} **pia**

kinukamito mwanamume anayekosa utulivu katika ndoa, anayeo na kuacha mara nyingi (KKK: 464)

kinukamito /kinuka'mito/ *nm.* (vi-) {a-/wa-} **pia kirukamito (b)**

mwanamume asiyeweza kuishi na mwanamke mmoja kwa muda mrefu, mwenye tabia ya kuoa na kuacha (KKK: 450)

kirukamito /kirukamito/ *nm.* (vi-) [a-/wa-] taz. ▀ **kinukamito.** (KKS: 249)

kinukamito /kinukamito/ **pia kirukamito** /kirukamito/ *nm* (vi-) [a-/wa-]

mtu anayehamama au kuacha mke na kuoa mwingine mara kwa mara; mtu asiye makini katika ndoa. (KKS: 240)

kirukamito /kirukamito/ *nm.* vi- (a-wa) 2 mwanamume mwenye tabia ya kuoa na kuacha wanawake. (KEK: 310)

kinukamito /kinukamito/ *nm.* vi- (a-wa) **pia kirukamito** mwanamume asiye na makini katika ndoa hivi kwamba huacha ndoa moja na kuhamia nyingine. (KEK: 299)

mruzi; mluzi

mruzi /m'ruzi/ *nm.* (mi-) {u-/i-} **pia mluzi** sauti inayotolewa kwa

kubenua midomo na kutoa hewa kwa nia ya kuigiza wimbo au kumpa mtu ishara fulani; mbinja. (KKK: 698)

mluzi /m'luzi/ *nm.* (mi-) {u-/i-} **pia mruzi** sauti nyembamba inayotokea kwenye tundu jembamba inayotokana na mkunjo na mbananisho wa midomo miwili iliyochongolewa kwa mbele *kis:* winja. (KKK: 674)

mluzi /mluzi/ **pia mruzi** *nm* (mi-) [u-/i-] sauti nyembamba ya pumzi inayotoka baina ya midomo miwili iliyochongolewa na kubanwa na kuachwa nafasi ndogo; mbinja. (KKS: 370)

mruzi /mruzi/ *nm* (mi-) [u-/i-] taz. ▀ **mluzi.** (KKS: 383)

mluzi /mluzi/ **pia mruzi** *nm* mi- (u-i) sauti nyembamba au hata nene inayosababishwa na upepo kulazimishwa kutoka kwenye midomo iliyofinywa kimakusudi na kuachwa tundu jembamba; mbinja. (KEK: 456)

mruzi /mruzi/ *nm* mi- (u-i) taz. **mluzi.** (KEK: 473)

bushiti; bushuti

bushiti /buʃiti/ *nm* (ma-) {i-/ya-} taz. **bushuti.** (KKK: 100)

bushuti /buʃu:ti/ *nm* (ma-) {i-/ya-} **pia bushiti** joho lililovaliwa na wanaume ambalo hutariziwa kwa nyuzi za rangi ya kuvutia mikononi, mgongoni na kifuani. (KKK: 100)

bushiti /buʃiti/ *nm* (-) (i-/zi-) taz. ▀ **bushuti.** (KKS: 52)

bushuti /buʃuti/ **pia bushiti** /buʃiti/ *nm* (-) (i-/zi-) vazi la kiume kama joho lishonwalo kwa zari nyingi, hasa mgongoni na kifuani. (KKS: 52)

bushti – Halikuingizwa. (KEK: Ø)

bushuti /buʃuti/ *nm* ma- (li-ya) **pia bushti** joho lililotariziwa kwa zari shingoni, mikononi hadi kitovuni. (KEK: 54)

epua; ipua

epua¹ epu.a /e'puwa/ *kit. ele.* **pia ipua** toa chombo k.v. sufuria, chungu au kikaango kilichobandikwa jikoni. (KKK: 198)

ipua /i: 'puwa/ *kit. ele.* **pia epua** toa jikoni chombo kinachopikwa. (KKK: 320)

epu.a¹ /epuwa/ **pia ipua** /Ipuwa/ *kt. [ele]* ondoa chombo k.v. chungu au sufuria kutoka kwenye jiko au mafiga. (KKS: 104)

ipua.a /Ipuwa/ *kt. [ele]* ▀ *taz.* **epua**¹. (KKS: 169)

epua/epua/ **pia ipua** *kt. (ele)* **1** toa chombo mekoni kama vile chungu, sufuria. (KEK: 126)

ipua/ipua/ *kt. (ele)* ondoa chungu au sufuria kutoga mafigani au jikoni. (KEK: 202)

Mifano zaidi ya visawe katika kamusi zilizochanganuliwa

mbochi; nekta

mbochi /'mbotʃi/ *nm.* (Ø) {ya-} majimaji ya maua yenye ladha ya sukari yanayotumiwa na nyuki kutengeneza asali. ... *kis.:* **nekta** (KKK: 608)

nekta /'nekta/ *nm.* (Ø) {i-/zi-} majimaji ya maua yenye ladha ya sukari

yanayofyonzwa na nyuki kutengeneza asali *vis.*: **mbochi** (KKK: 786)

mbochi /mbɔtʃi/ *nm* (-) [i-] majimaji matamu yanayotengenezwa na maua na kukusanywa na nyuki kutengeneza asali; **nekta**. (KKS: 329)

nekta /nekta/ *nm* (-) [i-] **taz. mbochi**. (KKS: 428)

mbochi /mbɔtʃi/ *nm* (i-zi) majimaji matamu yanayowavutia nyuki katika maua; uki, **nekta**. (KEK: 406)

nekta – Halikuingizwa. (KEK: Ø)

tarakilishi; kompyuta

tarakilishi /taraki'liʃi/ *nm*. (ma-) {i-/zi-} **taz. kompyuta**. (KKK: 988)

kompyuta /kɔ'mpju:ta/ *nm*. (Ø) {i-/zi-} mashine ya kielektroniki inayotumika kuendeshea mitambo, kuchanganua, kuhifadhi na kukokotoa data zilizotunzwa humo. (KKK: 505)

tarakilishi /tarakiliʃi/ *nm* (-) [i-/zi-] **taz. kompyuta**. (KKS: 553)

kompyuta /kɔmpjuta/ *nm* (-) [i-/zi-] mashine ya elektroniki ya kuhifadhi na kuchanganua taarifa zilizoingizwa, kukokotoa na kuongoza mitambo; **tarakilishi**. (KKS: 271)

tarakilishi /tarakiliʃi/ *nm* (i-zi) kompyuta kubwa ya mezani. (KEK: 673)

kompyuta /kɔmpjuta/ *nm* (i-zi) mashine iliyo na umbo la kisanduku kidogo ya kupiga chapa na kuhifadhi habari pamoja na kufanya michakato mbalimbali pamoja na mawasiliano katika mtandao; **tarakilishi**. (KEK: 335)

friji; jokofu

friji /f'ri:ʃi/ *nm*. (ma-) {li-/ya-} kifaa cha kuhifadhia chakula ambacho

kina mashine ya kutengeneza baridi; **jokofu**. (KKK: 223)

jokofu /ʒɔ' kɔfu/ *nm.* (*ma-*) '{*a-/wa-*}' chombo chenye vyumba kama kabati linalotumika kupozesha na kuhifadhi a vyakula na vinywaji *kis.:* **friji**, jirafu. (KKK: 350)

friji /friji/ *nm* (-) [i-/zi-] chombo mfano wa kabati chenye mtambo wa kuleta baridi, cha kuhifadhia agh. vyakula; **jokofu**, jirafu. (KKS: 117)

jokofu /ʒɔkɔfu/ *nm* (-) [i-/zi-] ─ taz. **friji**, jirafu. (KKS: 183)

friji /friji/ *nm* (i-zi) kifaa chenye milango na vyumba ndani yake ya kuhifadhia vyakula aina aina ili visipate kuharibika na vilevile kugandishia maji yawe barafu; **jokofu**. (KEK: 145)

jokofu /ʒɔkɔfu/ *nm* ma- (li-ya) chombo kinachotumika kutunzia vyakula visiharibike na kuvifanya vipoe na kuwa na baridi; **friji**, jirafu. (KEK: 224)

kenda; tisa

kenda /'kenda/ *nm.* (∅) {i-/zi-} namba tisa '9' katika orodha ya tarakimu au idadi ... (KKK: 394)

tisa /'tisa/ *nm.* (∅) {i-/zi-} namba nzima iliyo kati ya nane na kumi; '9' *kis.:* **kenda** (KKK: 1008)

kenda /kenda/ *nm* (-) (i-/zi-) ─ taz. **tisa**. (KKS: 210)

tisa /tisa/ *nm* (-) (i-/zi-) tarakimu '9' au idadi ya hesabu baina ya nane na kumi; **kenda**. (KKS: 568)

kenda¹ /kenda/ *nm* (i-) nambari kuu iliyo baina ya nane na kumi; **tisa**. (KEK: 258)

tisa /tisa/ *nm* (i-zi) namba kamili inayofuata baada ya nane; **kenda**. (KEK: 688)

saratani; kansa

saratani¹ /sara'tani/ nm. (Ø) {i-/zi-} ugonjwa unaotokana na uotaji wa

seli damu usio wa kawaida mwilini unaosababishwa na ama athari za vyakula, mazingira au kurithi vinasaba nyenye kasoro
kis.: **kansa** (KKK: 911)

kansa /'kansa/ nm. (Ø) {i-/zi-} **pia kansa; saratani** mujumuiko wa

maradhi mengi yanayosababishwa na mgawanyiko mbaya wa seli za mwili zinazovamia tishu nyingine za mwili kwa njia ya damu na kusababisha uvimbe au kutoka kwa seli hizo mwilini bila kikomo na agh. hatima yake huwa ni kifo. (KKK: 376)

saratani³ /saratani/ nm (-) [i-/zi-] ▀ taz. **kansa**. (KKS: 502)

kansa /kansa/ nm (-) [i-/zi-] uvimbe au uotaji usio wa kawaida wa seli

katika mwili wa binadamu ambao huweza kusababisha kifo;
saratani. (KKS: 198)

saratani² /saratani/ nm (i-zi) ugonjwa unaosababisha kuzaliana kwa

seli zisizo za kawaida mwilini; **kansa**. (KEK: 611)

kansa /kansa/ nm (i-zi) **pia kansa** maradhi ya aina yanayosababishwa

na virusi ambapo kunakuwa na uongezekaji wa seli kiholela mwilini; **saratani**, seratani. (KEK: 246)

Mifano zaidi kutoka kwenye kamusi zilizochanganuliwa**Kamusi Kuu ya Kiswahili**

	Methali	Kidahizo ilipoingizwa	Maana
1.	Adhabu ya kaburi aijuaye maiti	Adhabu	Ø
		Kaburi	Asiyefikwa na shida hajui adha yake.

2.	Bandu bandu humaliza gogo.	Bandu	Ufanyaji wa jambo kidokidogo hatimaye <i>kukamilisha</i> jambo zima.
		gogo ¹	Hatua kwa hatua jambo hukamilika.
3.	Bura yangu sibatili kwa rehani.	Bura	Mwanadamu hastahili kutupa kitu cha thamani ndogo alichonacho kwa kutamani kizuri cha mwenzake.
		Rehani	Usidharau kitu chako hata kama ni kibaya.
4.	Hamadi kibindoni silaha iliyo mkononi.	hamadi!	Kitakachokusaidia ni kile ambacho unacho kwa wakati huo.
		kibindo ¹	Kitu kinachoweza kukusaidia wakati wa shida <i>na</i> kile ulichonacho.
5.	Hakuna masika yasiyokuwa na mbu.	Mbu	Hakuna kitu kisichokuwa na kasoro.
		masika	Hakuna kitu kisichokuwa na kasoro.
6.	Hasira hasara	Hasira	Matokeo ya hasira wakati wote huwa mabaya
		Hasara	Hasira husababisha au upotevu wa vitu au hali, na mali
7.	Kifo cha wengi ni harusi.	Arusi	Machungu yanapowapata wengi uzito wake hupungua.
		Harusi	Hasara ya wengi haina majuto.
		Kifo	Tatizo likiwapata wengi lina nafuu kuliko lile linalompata mtu mmoja peke yake
8.	Kila mwamba ngoma huvutia kwake.	mwamba ³	Yeyote anayefanya jambo, hujali sana manufaa yake binafsi kwanza.
		wamba ¹	Kila mtu hujipendelea yeye kwanza.
9.	Kilimia kikizama	kilimia	Hubashiri majira ya kilimo.

	kwa jua huzuka kwa mvua	zama ¹	Kitu ulani chenye manufaa hata kama kitapotea kwa muda fulani baadaye kitapatikana.
10.	Kukopa harusi kulipa matanga	Kopa	Kupata kitu unachoazima kwa mtu ni jambo linalompa mtu furaha, lakini kurejesha ni mhali
		matanga	Kuazima ni furaha, lakini kurejesha ni majonzi.
		tanga ²	Ø
		Arusi	Ø
11.	Kuzima koleo si mwisho wa uhunzi	mwisho	Kupumzika sio kuacha kazi.
		Koleo	Kuachwa kwa jambo sio mwisho wa jambo hilo, huenda likaeendelea.
		uhunzi	Kupumzika si kuacha kazi kabisa.
		tangamana	Ø
		fila ¹	Uandilifu na uovu havipatani.
12.	La kuvunda halina ubani	ubani ¹	Jambo linapokwenda kombo, huwa limekosa mwongozaji.
		Vunda	Kitu kikishatokea au kitu kikishaharibika huna namna ya kukizuia.
13.	Majuto ni mjukuu.	majuto	Ø
		mjukuu	Masikitiko hufuata muda kitambo baada ya tukio kutokea.
14.	Mcha mungu si mtovu.	cha ³	Mtu anayeomba Mungu hana ukosefu wa heshima.
		Mcha	Ampendaye Mungu, hatendi dhambi.
15.	Mchama ago hanyeli huenda akawia papo	ago ²	Ø
		chama ²	Aliyejenga kambi mahali kisha akahama huwa hachafui mahali hapo kwani huenda akaparudia tena.

		Uya	Si jambo nzuri kumdharau mtu aliyekusaidia kwani huenda siku nyingine ukamrudia.
16.	Mchovya asali hachovyi mara moja.	Asali	Anayeonja raha, atataka aendelee kuipata daima.
		maral ¹	Ukionja kitu kizuri utazoea kufanya hivyo.
17.	Mfa maji haachi kutapatapa.	Mfa	Mtu aliyepata tatizo fulani gumu hatakosa kutafuta njia za kujinasua hata kama hazitamsaidia.
		tapatapa	Mtu akipatwa na shida hutumia njia yoyote ili kujinusuru.
18.	Mkate mkavu wa nyumbani ni bora kuliko nyama nzuri ya shuwa ya pengine	Mkate	Ni afadhali mkate wa nyumbani kuliko nyama nzuri yenye mafuta ya mahali pengine.
		Shuwa	Kitu ulichokizoea ni rahisi kukitumia kuliko kigeni.
19.	Mkuki kwa nguruwe kwa binadamu u mchungu.	mkuki	Ubaya, afanyiwe mwingine; ukifanyiwa wewe hupendi
		nguruwe	Usimfanyie mtu mabaya usiyoyapenda hata wewe.
20.	Mstahimilivu/Mvum ilivu hula mbivu.	mstahimilivu	Uvumilivu hadi mwisho unahitajika katika kufikia mema.
		mvumilivu	Mtu anayevumilia taabu na shida nyingi hupata mafanikio maishani.
21.	Mwana wa mhunzi asiposana hufukuta.	mhunzi	Mtoto wa fundi fulani asipounda au kutengeneza kitu, basi atakuwa akimsaidia mzazi wake kufanya kazi ndogondogo zinazokamilisha kazi hiyo.
		vuvia	Mtoto wa fundi fulani asipounda au kutengeneza kitu, basi atakuwa akimsaidia mzazi wake kufanya kazi ndogondogo

			zinazokamilisha kazi hiyo.
22.	Mwenye matende hana paja.	matende	Ni vigumu kutenganisha kati ya muundi na mguu kwa mguu wenye ugonjwa wa matende.
		tende ²	Anayepatwa na shida huwa hawazi kama binadamu wenzie.
23.	Nazi mbovu harabu ya nzima.	harabu ²	Nazi moja mbovu huwez kuharibu nyingine nzima; mtu mbaya anaweza kuambukiza wengine au kusababisha madhara makubwa.
		nazi ¹	Mtu mwenye tabia mbaya huweza kuwaathiri kitabia wengine wanaomzunguka.
		uharabu	Mtu mwenye tabia mbaya huweza kuwaadhiri kitabia wengine wanaomzunguka.
24.	Ng'ombe mwenye tume ndiye achinjwaye	ng'ombe,	Anayejifanya mjanja wa kukwepa balaa ndiye humfika.
		tume ²	Ø
25.	Ngoja ngoja yaumiza matumbo	matumbo	Kuchelewa kufanya jambo huleta madhara.
		Ngoja	Tabia ya kuchelewa kufanya jambo huenda ikaleta madhara.
26.	Paka akiondoka panya hutawala	paka ¹	Kuondoka kwa mwenye nguvu ni nafuu au furaha kwa mnyonge.
		ondoka	Mkubwa akiondoka, mdogo hufanya apendavyo.
27.	Pilipili usiyoila yakuwashiani?	pilipili	Usiingilie mambo yasiyokuhusu.
		washa ²	Ø
28.	Usiache mbachao kwa msala upitao.	mbacha	Usihadaike na upya wa kitu ukadharau chako cha zamani.

		msala ²	Usidharau kitu cha zamani hudumu kuliko vya sasa.
29.	Ukubwa ni jaa.	jaa ¹	Mtu mkubwa au kiongozi hupata lawama au sifa za kila aina.
		ukubwa	Wakuu au wakubwa hutupiwa lawama zote.
30.	Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.	Nguvu	Ni vizuri kushirikiana na vinadamu wenzio.
		udhaifu ²	Umuhimu wa kushirikiana na binadamu wenzio katika mambo unayofanya.
		Umoja	Ø
		utengano	Jambo likifanywa kwa pamoja litakuwa na matokeo mazuri.
31.	Yaliyopita si ndwele tugange yanjayo.	ndwele	Pambana na yanayokuja badala ya yaliyopita.
		Pita	Ø
32.	Sheria ni msumeno (hukata mbele na nyuma)	msumeno	Ø
		sheria	Sheria humhusu kila mtu.
33.	Usipoziba ufa utajenga ukuta.	Ufa	Usiposhughulikia tatizo litakugharimu.
		ziba	Ukidharau tatizo dogo, litaongezeka na kuwa kubwa zaidi.

Kamusi ya Kiswahili Sanifu

	Methali	Kidahizo	Maana
1.	Akipenda chongo huita kengeza.	chongo ¹	Ø
		penda ¹	Ø
2.	Baada ya dhiki faraja.	dhiki ¹	Ø

		baada	Ø
3.	Baninani mbaya kiatu chake dawa.	baniani	Ø
		kiatu	Ø
4.	Bura yangu sibadili kwa rehani.	badili ¹	Ø
		bura ¹	Ø
		rehani	Ø
5.	Dau la mnyonge haliendi joshi.	dau ¹	Ø
		joshi ³	Ø
6.	Fuata nyuki ule asali.	asali	Ø
		fuata	Ø
7.	Heri nusu shari kuliko shari kamili.	nusu	Ø
		shari	Ø
8.	Kazi mbi si mchezo mwema.	mbi	Ø
		kazi ¹	Ø
9.	Kidole kimoja hakivunji chawa.	chawa	Ø
		kidole	Ø
10.	Kila ndege huruka kwa ubawa wake.	kila ²	Ø
		ruka ¹	Ø
11.	Kipyaa kinyemi ingawa kidonda.	kinyemi	Ø
		-pya	Ø
12.	Kukopa harusi kulipa matanga.	harusi	Ø
		kopa ³	Ø
13.	Kutoa ni moyo usambe ni utajiri.	moyo	Ø
		toa	Ø
14.	Kwa mwoga huenda kicheko, kwa shujaa kilio.	mwoga	Ø
		shujaa	Ø
15.	Maji ya nazi yatafuta mvugulio.	maji	Ø
		nazi	Ø

16.	Mbio za sakafuni huishia ukingini.	mbio ²	Ø
		sakafu	Ø
17.	Mcha Mungu si mtovu.	mcha	Ø
		cha ¹	Ø
18.	Mchimba kisima huingia mwenyewe.	chimba ¹	Ø
		mchimba	Ø
19.	Mie nyumba ya udongo sihimili kishindo.	mie	Ø
		nyumba	Ø
20.	Mkono mtupu haulambwi.	lamba	Ø
		mkono	Ø
21.	Mla ni mla leo, mla jana kalani?	leo	Ø
		mla	Ø
22.	Mwana wa yungi hulewa kaifa wa mlimwengu.	kaifa ²	Ø
		mwana	Ø
23.	Mwanzo wa ngoma ni lele.	lele	Ø
		mwanzo ¹	Ø
24.	Mwenda pole hajikwai.	enda	Ø
		pole ²	Ø
25.	Mwosha huosha.	mwosha	Ø
		osha	Ø
26.	Nazi mbovu harabu ya nzima.	harabu	Ø
		nazi	Ø
27.	Ng'ombe mwenye tume ndiye achinjwaye.	ng'ombe ¹	Ø
		tume ²	Ø
28.	Sheria ni msumeno.	sheria ¹	Ø
		msumeno	Ø
29.	Ukiona ambari na zinduna i papo.	ona	Ø
		ambary	Ø
30.	Ukuukuu wa kamba si upya	kuukuu	Ø

	wa ukambaa (kuukuu)	kamba ¹	Ø
31.	Umekuwa pweza wajipalia makaa.	paa	Ø
		pweza	Ø
32.	Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti.	mkakasi ²	Ø
		uzuri ¹	Ø

Kamusi Elezi ya Kiswahili

	Methali	Vidahizo	Maana
1.	Adhabu ya kaburi aijuwaye maiti.	Adhabu	Ubaya wa kitu aujuaye ni anayehusika nacho.
		kaburi	Mtu awezaye kulifahamu jambo vizuri ni yule aliyefikwa nalo wala si mwingine.
2.	Ahadi ni deni.	ahadi ¹	Ukitoa ahadi unawajibika kulitekeleza jambo uliloliahidi.
		Deni	Ukiahidi jambo unalazimika kulitimiza.
3.	Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.	Guu	Anayeasi mawaidha ya wazee mwishowe hukumbwa na hasara maishani mwake.
		sikia	Usipofuata ushauri wa watu wanaojua mambo mazuri na mabaya utaharibikiwa katika maisha.
4.	Jogoo la shamba haliwiki mjini.	jogoo	Tuwapo ugenini hatuwezi kufanya mambo kwa uhuru.
		shamba	Mtu asiyejua mambo mengi ya kisasa hawezi kutamba anapokutana na werevu.

KIAMBATISHO CHA PILI: KIONGOZI CHA MAHOJIANO**Mahojiano na wachapishaji**

1. Wadhifa wako ni upi katika shirika lako la uchapishaji?
2. Umekuwa katika shirika ili kwa muda gani?
3. Je, shirika lenu huchapisha kamusi za Kiswahili? Iwapo ndio:
 - a) Mnachapishia kiwango gani cha watumiaji?
 - b) Kamusi hizo ni zipi na zilichapishwa lini?
4. Ni changamoto zipi mnazokumbana nazo katika mchakato mzima wa uchapishaji wa kamusi?
5. Je, nini ambacho huathiri gharama ya uchapishaji wa kamusi?
6. Mnatumia mbinu gani kupunguza gharama ya uchapishaji bila kuathiri ubora wa kamusi?

**KIAMBATISHO CHA TATU: HOJAJI KWA WATUMIAJI WA
KAMUSI**

(Taarifa utakazozitoa zitatumika tu katika kufanikisha utafiti wa kimasomo.)

1. Mimi ni: *(Tia alama X panapostahili.)*

a) Mwalimu ()

b) Mwanafunzi ()

2. Iwapo wewe ni mwalimu unafunza masomo gani?.....

3. Iwapo wewe ni mwanafunzi, uko katika kidato gani?.....

4. Shule yenu inaitwaje?

5. Je, unajua kamusi zipi ambazo unatumia kwa marejeleo?

.....

6. Je, kamusi unayoitumia ina taarifa kama zipi ambazo zinakupendeza?

.....

.....

7. Je, ni rahisi kuzipata taarifa hizo katika kamusi hiyo? *(Tia alama X panapostahili.)*

a) NDIO ()

b) LA ()

c) Iwapo jibu lako ni NDIO, ni nini kinachangia hilo?

d) Iwapo jibu lako ni LA, ni nini kinachangia hilo?

8. Maneno ya Kiswahili yanahusiana sana. Kwa mfano, kuna maneno ambayo ni vibadala, visawe na vinyume. Je, uhusiano huu umeoneshwa katika kamusi unayoitumia?

a) NDIO () LA ()

b) Uhusiano huo umeoneshwa katika kamusi?

9. Je, kamusi unayoitumia ina vifungu hivi vifuatavyo vya maneno? (*Tia alama X panapostahili kama ishara ya NDIO.*)

a) Methali ()

b) Nahau ()

c) Misemo ()

10. Pale ambapo vifungu vilivyotajwa katika swali la 8 vimeingizwa katika kamusi:

a) Je, vimeingizwa katika neno moja linalokiunda kifungu hicho au katika maneno zaidi?

.....

b) Ni athari gani inayotokana na mtindo ulioutumiwa kuviingiza vifungu hivyo katika kamusi?

.....

Asante sana kwa muda wako.

KIAMBATISHO CHA NNE: MAKADIRIO YA MATUMIZI

Shughuli	Kiwango (Shilingi za Kenya)
Mawasiliano	3,000
Uchapishaji (upigaji chapa, uhariri, utoaji wa nakala)	35,000
Mtandao	12,000
Usafiri	10,000
Matumizi mengine	10,000
Jumla	70,000